

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILINO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Saba – Tarehe 6 Novemba, 2013

(Mkutano Ulianza saa Tatu Asubuhi)

DUA

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwatangazia kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 30(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Aprili, 2013 na Ibara ya 91 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete anakusudia kulihutubia Bunge siku ya Alhamisi tarehe 7 Novemba, 2013 kuanzia saa 10.00 jioni. Wote mnaombwa kuwepo ukumbini siku hiyo ili kumsikiliza Mheshimiwa Rais.

Katibu!

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu Mzumbe kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 [*The Annual Report and Accounts of Mzumbe University for the Year ended 30th June, 2012*].

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Namwita Mheshimiwa Vicent Joseph Nyerere aulize swali lake.

Na. 82

Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mara

MHE. VICENT J. NYERERE aliuliza:-

Kwa miaka miwili mfululizo Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, lakini mpaka sasa kazi haijaanza.

Je, ni nini kimekwamisha ujenzi huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ulianza kupitia nguvu za wananchi mwaka 1980 na kusimama mwaka 1987, baada ya wananchi kushindwa kuendeleza ujenzi huo kutokana na kuongezeka kwa gharama za ujenzi. Baada ya juhudi za kumpata mwendelezaji kutokufanikiwa, mwaka 2010 hoja ilijengwa kupitia Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) na kukubaliwa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya gharama za kukamilisha ujenzi yaliingizwa katika mpango wa miaka mitano wa maendeleo wa Mkoa wa Mara kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 hadi 2016/2017 inayokadiriwa kuwa Shilingi bilioni 37 mpaka utakapokamilika. Mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya Shilingi bilioni 2.1 zilitengwa na kutolewa na Serikali, na mwaka 2013/2014 zilitengwa ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba, 2013 Shilingi milioni 500 zimetolewa kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]

ajili ya kuendeleza mradi. Kazi nyingine zinazofanyika ni ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Hospitali kwa gharama ya Shilingi milioni 250 kupitia bajeti ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, awali Mkoa uliomba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya *TASAF* ndiyo wajenge. Hata hivyo, mfuko haukuweza kuafikiana na Mkoa kwa kuwa walikuwa na miradi mingine ya ujenzi inayoendelea. Hivyo, hatua zilizochukuliwa na Mkoa ni kutangaza zabuni ili kumpata Mkandarasi ambapo Zabuni ilitangazwa katika gazeti la *Daily News* la Tarehe 21 Mei, 2013. Taratibu za kumpata Mkandarasi ziko katika hatua za mwisho.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa, Serikali inatumia fedha nyingi sana kuwatibu watu nje nikiwemo mimi mwenyewe, na Hospitali ya Apollo ilionyesha nia ya kuwekeza katika Hospitali hapa Tanzania; kwa nini Serikali isiwasiliane na watu wa Apollo kwa ajili ya kuwapo Hospitali hii ili shughuli ya ujenzi wa Hospitali iende haraka?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vicent Nyerere kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba tunatumia gharama kubwa sana kupeleka wagonjwa nje na kwa sasa hivi Serikali iko katika hatua za kuziboresha hospitali zetu kuhakikisha kwamba magonjwa mengi ambayo yanawapeleka wagonjwa nje yanatibiwa humu humu ndani. Yeye mwenyewe ni shahidi kwamba sasa hivi Muhimbili wanafanya *operation* ya moyo na hata vitengo vingi ambavyo wagonjwa wetu walikuwa wanapelekwa nje vimeimarishwa. Ukienda Moi sasa hivi huduma nyingi kwa kweli, kwa kiasi kikubwa zinapatikana Muhimbili na katika hospitali zetu za Rufaa za Bugando na *KCMC*.

SPIKA: Mheshimiwa Conchesta nimekuona!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, yako majengo mengi ambayo yamejengwa katika Hospitali za Mikoa na yamekamilika bila kutumika. Kwa mfano, Hospitali ya Mkoa wa Singida, kuna jengo la Hospitali ya Tumbi lakini pia kuna jengo la Siha. Ni lini Serikali sasa itaruhusu au kutoa pesa ili majengo haya yaweze kutumika ili huduma ziwepo kwa ajili ya wananchi? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante kwa swali zuri. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna majengo mengi yamekamilika na yanahitaji kutumika na Mheshimiwa aliyeuliza swali, mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI na ana ushahidi kwamba katika bajeti ya mwaka huu Tumbi, Hospitali ya Singida na Siha tumezitengea pesa ambazo zitawawezesha kununua vifaa ili ziwewe kutumika.

SPIKA: Naomba tuendeleo na swali linalofuata, Mheshimiwa Diana Chilolo.

Na. 83

Ujenzi wa Kituo cha Afya Shelui

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Wakati wa kampeni za Urais mwaka 2010, Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga Kituo cha Afya Kata ya Shelui na tayari wananchi chini ya uongozi wa Kata hiyo walishaanza kuchangia mfuko wa ujenzi huu na kufyatua tofali; na ahadi hii Serikali imeiachia Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ambayo ina mapato madogo sana kupitia vyanzo vyake:-

[MHE. D. M. CHILOLO]

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa fedha kupitia Mfuko wa MMAM ulioko Halmashauri?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya huibuliwa na wananchi wenyewe kupitia Mpango wa Fursa na Vikwazo katika Maendeleo (*O&OD*) na kutekelezwa kwa ubia wa wananchi na Halmashauri. Halmashauri huchangia gharama kidogo za utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa pamoja na usimamizi. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa kushirikiana na wananchi, imeanza ujenzi wa Kituo hicho cha Afya ambapo vifaa yakiwemo matofali 3,000 na mifuko ya Saruji 70 vimeandaliwa na ujenzi upo katika hatua ya msingi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Halmashauri imetenga Shilingi milioni 80 kutokana na fedha za ruzuku ya maendeleo katika Serikali za Mitaa (*LGCDG*) kwa ajili ya ujenzi huo. Wananchi watachangia Shilingi milioni 40 ili kukamilisha utekelezaji wa mradi huu ambapo unatarajiwa kugharimu Shilingi milioni 120 katika awamu ya kwanza. Aidha, katika mwaka huu Halmashauri imeweka kipaumbele kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba tano za watumishi katika Zahanati za Mwendui, Gembena na Kisharita kwa gharama ya Shilingi milioni 75.0, kukamilisha majengo ya wagonjwa wa nje (*OPD*) katika Zahanati tatu za Kata ya Urughu kwa gharama ya Shilingi milioni 60.0 na kukamilisha majengo ya Zahanati za Misuna na Kisimba kwa gharama ya Shilingi milioni 50.5.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba itaendelea kutenga fedha kila mwaka kadri zitakavyopatikana ili kukamilisha ujenzi huo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Diana Chilolo swali la nyongeza.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, changamoto ya kujenga Kituo cha Afya hiki ilitokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais kuahidi kujenga Kituo cha Afya hapo; na kwa kuwa jitihada hizi alizozisema Mheshimiwa Waziri, mpaka sasa hivi wananchi wana tofali 6,000 mpaka leo hii na wana Shilingi milioni tano za kuchangishana wenyewe na ahadi ya Serikali ilikuwa itenge kuanzia bajeti hii ambayo tunaitumia sasa: Je, kwa kusubiria bajeti ya mwaka kesho, hatuoni kwamba wananchi hawa tunawakatisha tamaa na wanakuwa hawana imani na ahadi ya Mheshimiwa Rais? Je, Serikali itakuwa tayari kutafuta pesa popote kuweka nguvu ya ujenzi wa Kituo hiki cha Afya kwenye Mji? Shelui ni mji mdogo...

SPIKA: Aise! Uliza swali.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ni kweli ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na inavyotakiwa ahadi za Mheshimiwa Rais tuweke katika mipango yetu na hapo hapo Serikali inaangalia kwamba inatoa pesa kutoka katika vyanzo gani.

Katika jibu langu la msingi, nimesema katika bajeti ambayo tunayo ya mwaka 2013/2014 Halmashauri imetenga Shilingi milioni 80 kutoka katika pesa za ruzuku ya Serikali za Mitaa. Ukishasema ruzuku, maana yake inatoka Serikali kuu na siyo kutoka vyanzo vya Halmashauri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge napenda nikuhakikishie kwamba ahadi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]*

ya Mheshimiwa Rais inatekelezwa na Serikali imeanza kutoa pesa. Katika bajeti hii imeanza imeanza kwa Shilingi milioni 80 na bajeti zinazofuata pia itaendelea kutenga.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Zambzi, swali la nyongeza.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais aliweka ahadi nyingi katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Afya na kule Mkoani Mbeya Mheshimiwa Rais aliweka ahadi pia ya kujenga hospitali kutoka Kansamba ambapo pana Kituo cha Afya, Mheshimiwa Rais kwa mazingira yale aliahidi kwamba atahakikisha kwamba panajengwa Hospitali yenyewe; lakini pia na maeneo mengine. Nataka kujua, leo ni miaka mitatu ahadi hizi nyingi hazijatekelezwa. Ni lini hasa ahadi zote za Mheshimiwa Rais tutegemee kwamba zitatekelezwa na Serikali kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa ahadi nyingi na kati ya ahadi hizo pia nyingi zimeshatekelezwa na nyingi zilizobaki zipo katika mchakato wa kutekelezwa.

Ninachosema ni kwamba Mheshimiwa Rais akitoa ahadi, sisi tuliopo katika Wilaya na Mkoa ndiyo tunaopaswa sasa kuziweka katika vipaumbele vyetu, kama na sisi tunazona ahadi za Mheshimiwa Rais ni kwa manufaa yetu. Kwa hiyo, naomba kila Wilaya na kila Mkoa, zile ahadi ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa, kila tunapopanga mipango yetu tuziweke katika vipaumbele vyetu, kwa sababu kila mwaka Serikali inatenga pesa za afya, barabara na kila kitu katika maeneo yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]

Sasa tusifikirie kwamba kuna pesa za miradi ya maendeleo peke yake halafu kuna pesa zitaletwa peke yake kwa ajili ya kutekelezwa ahadi. Ndiyo maana nikasema kwa suala la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo kwamba Mheshimiwa Rais alitoa ahadi na wananchi wenyewe wakaona umuhimu ile ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba iwe ni miongoni mwa vipaumbele vyao, wakaweka katika mpango wao, wenyewe wakaanza kuchangia na Halmashauri ikaweka katika mpango wake na Serikali kwa kuanzia mwaka huu imepeleka Shilingi milioni 80.

Kwa hiyo, nawaomba na wananchi wa Kansamba waone umuhimu wa mradi huo ambao Mheshimiwa Rais ameuhidi, waweke katika bajeti yao ya mwaka huu wa fedha unaoanza.

SPIKA: Mheshimiwa Suzan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa ni sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kujenga Vituo vya Afya katika kila Kata, lakini sera hii bado haijatekelezwa katika maeneo mbalimbali hususan maeneo ya Mijini, naomba kujua Serikali inatambua kwamba katika Kata ya Kinondoni, Wilaya ya Kinondoni na Jimbo la Kinondoni hakuna Kituo cha Afya? Kama wanajua wana mpango gani kuhakikisha kwamba maeneo ya mijini nayo yanapatiwa Vituo vya Afya?

SPIKA: Swali hilo ni jipya, lakini Waziri anaweza kujibu. Au sivyo!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeahidi kujenga Zahanati kila Kata na kila Wilaya na kila Halmashauri na yenyewe inajipangia wapi waanze na wapi wamalizie. Mheshimiwa Susan Lyimo nadhani ni Mbunge ambaye ni Diwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni. Kwa hiyo, siyo suala la kuiuliza Serikali, tuwaulizeni mliopo Kinondoni kwamba katika vipaumbele vyenu, Kinondoni mmeiweka ianze lini? Kwa sababu kama TAMISEMI

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]

hatupangi mipango ya kila Halmashauri, lakini pamoja na hivyo, katika Kata za Mjini ni tofauti na Kata za Halmashauri ya Wilaya.

Kata za Vijijini zinaweza, kila Kata ikawa na Kituo chake cha Afya. Lakini Kata za Mijiji zenyewe kwa muundo wake mnaweza mkaamua hata Kata mbili mkawa mna-share. Lakini mnapangaje kwamba kila Kata iwe, ipi ianze na ipi imalizie, nadhani Mheshimiwa Mbunge hilo linabaki mikononi mwenu. Ndiyo maana ya kusema tumegatua madaraka kupeleka kwa wananchi ili wenyewe waweze kuamua kwamba waanze kipi na wamalize na kipi.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Selemani Said Bungara. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Rajab Mbarouk.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Selemani Said Bungara Bwege naomba swali lake Na. 84 sasa lijibiwe. *(Kicheko)*

SPIKA: Jina la nne ameongeza yeye, humu halipo. *(Kicheko)*

Na. 84

Mji wa Kilwa Kivinje Kufanyuwa Mji Mdogo

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE. SELEMANI SAID BUNGARA aliuliza:-

Mji wa Kilwa Kivinje ni mkongwe na una umaarufu mkubwa wa mambo ya kale na una hospitali ya Wilaya, Shule za Sekondari, Makao Makuu ya Kata na Tarafa na idadi ya wakazi 10,000.

Je, ni lini Serikali itatangaza rasmi Mji huo kuwa Mji Mdogo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu, jina la nne ameongeza yeye lakini humu halipo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, almaarufu Bwege, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ipo kazi ya ukuaji wa idadi ya watu katika Mji wa Kilwa Kivinje ambayo inaleta changamoto katika utoaji wa huduma za jamii katika eneo hilo. Kwa kuzingatia hilo, Serikali ilitangaza Mji huu kuwa eneo la mipango kupitia Tangazo la Serikali namba 176 la tarehe 9 Agosti, 1996 ili kuzuia ukuaji holela, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa ili kupandishwa hadhi eneo hilo la Kilwa Kivinje kuwa mamlaka ya Mji Mdogo kutategemea kukamilika kwa taratibu na vigezo na maombi hayo kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ili kupata ridhaa yake.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rajab, swali la nyongeza.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya kutia moyo ya Mheshimiwa Waziri ambaye na yeye ni mmoja kati ya watu ambao wanatoka katika maeneo haya, Mheshimiwa Bwege alitaka kujua, ni lini sasa hayo yatakuwa yamekamilika?

Mheshimiwa Spika, pili, hivi sasa uanzishwaji wa Miji Midogo umekua kwa kasi katika nchi yetu kiasi ambacho Miji Midogo hii huhitaji fedha kwa ajili ya kujiendesha, fedha ambazo huwa zinatoka katika Halmashauri husika. Halimashauri zetu nchini hivi sasa nchini, *average* ya uwezo wake wa kujitegemea ni 10% tu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMED]

Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni muda mwafaka wa kukaa na kufanya tathmini ili kuona hali halisi ya huu uanzishwaji wa Miji Midogo pamoja na baadhi ya Halmashauri hapa nchini? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bwege kauliza kwamba ni lini; mimi nasema, itategemea kwanza tupate maombi kutoka Halmashauri husika suala ambalo hatujalipata. Ili walete maombi ni lazima kwanza waanze mchakato kuanzia katika Kijiji hicho cha Kilwa Kivinje na kwenda kwenye Kata, wakitoka kwenye Kata waende kwenye Halmashauri, waende kwenye *DCC*, waende Mkoani na ndiyo watuletee maombi. Baada ya kupata maombi sisi tutakwenda kuhakiki kama vigezo vimekamilika ndipo tuweze kuwapa.

Kwa hiyo, siwezi kusema lini wakati sijapokea maombi yao. Kwa hiyo, sijui kama wana vigezo au hawana. Kwa hiyo, kuhusu itategemea lini; Mheshimiwa Mbunge ndiye anajua lini atakapoleta maombi yake ili na sisi tuweze kujipanga lini tutaweza kumkamilishia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuanzisha Miji Midogo na kwamba kuna gharama kubwa za uendeshaji wa Miji Midogo. Kwanza Miji Midogo yenyewe ni kitu cha mpito kwamba unapokuwa na Mji Mdogo ni kwamba unajiandaa kuwa na Halmashauri ya Mji. Kwa hiyo, Mji Mdogo gharama yake na matumizi yake yote yanabebwa na Halmashauri mama. Ndiyo maana hata yule Mtendaji Mkuu katika Mji Mdogo cheo chake wala hakitambuliki mahali popote. Ni cheo cha kupewa tu pale pale katika Halmashauri.

Kwa hiyo, kuwa na Mji Mdogo hakuongezi gharama yoyote kwa sababu bado ule mji unahitajika kuhudumiwa. Kitu cha msingi, tunaweka Mji Mdogo ili uwe Halmashauri ya Mji kuuwezesha upangwe na usijengwe kiholela. Hata hivyo,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]

labda suala la kuangalia ni jinsi gani tunavyoanzisha Halmashauri za Miji au Wilaya na siyo Miji Midogo.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni lini Serikali itakamilisha na kutangaza Mji wa Kishapu kuwa mamlaka ya Mji Mdogo?

SPIKA: Umemsikia? Mheshimiwa Waziri wa Nchi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, suala la mji wowote kukamilika kuwa Mji Mdogo, kuwa Halmashauri, inategemea pande mbili, kwa upande wa Kishapu na sisi TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, mpaka ninavyozungumza hatujapokea ombi lolote kutoka Kishapu. Kwa hiyo, siwezi kujua ni lini tutakamilisha kuwa Mji Mdogo wakati hatuna maombi mezani.

SPIKA: Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atauliza swali hilo na kwa niaba yake namwona Mheshimiwa Victor Mwambalasa.

Na. 85

Uzalishaji na Matumizi ya Mkaa Nchini

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. ANNE K. MALECELA) aliuliza:-

Utafiti umeonesha kuwa Tanzania inazalisha kiasi cha tani milioni moja za Mkaa na kwamba asilimia hamsini (50%) ya mkaa huo hutumika Mkoani Dar es Salaam:-

(a) Je, Taifa linapata athari gani kwa kuzalisha mkaa kiasi kikubwa hiki?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. V. K. MWAMBALASWA]

(b) Je, Serikali haioni kuwa Mkoa wa Dar es Salaam hauna haja ya kutumia kiasi hiki cha mkaa kwa kuwa nyumba nyingi zina umeme kuliko Mikoa mingine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Taifa linapata athari kubwa katika kuzalisha mkaa wa kiasi kikubwa kwa kuwa Tanzania inapoteza hekta za misitu zipatazo 400,000 kwa mwaka. Hii huchangiwa na shughuli mbalimbali zisizo endelevu ikiwemo ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa na kuni. Hata hivyo, takwimu zinaonesha pia asilimia 90% ya matumizi ya nishati Tanzania inapatikana kutoka kwenye kuni na mkaa ambapo mkaa hutumika zaidi Mijini kama Dar es Salaam na kuni hutumika vijijini. Athari tunayoipata kwa kuzalisha mkaa kwa wingi ni pamoja na kusababisha mmomonyoko wa udongo, kupungua kwa malisho, kupungua kwa mvua, ongezeko la hewa ukaa, ambapo huchangia ongezeko la joto duniani na hatimaye matokeo yake ni mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bionuwai ambapo wanyama na baadhi ya mimea vinatoweka.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la Mkoa wa Dar es Salaam kuacha kutumia mkaa kwa kuwa nyumba nyingi zina umeme kuliko Mikoa mingine linaweza kuwa sahihi kwa watu wachache tu. Hii ni kwa sababu gharama za umeme ni kubwa kwa wananchi wa kawaida hasa kwa matumizi ya kupikia. Ili uweze kutumia umeme kwa kupikia, itamlazimu mwananchi wa kawaida anunue jiko la umeme na vifaa vyake vya kupikia ambavyo vyote upatikanaji wake ni wa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa nishati ya umeme nchini bado ni mdogo sana. Takribani asilimia 20 tu ya jamii ya Watanzania wamefikiwa na huduma hiyo. Hata hivyo,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS]

Serikali inaendelea kuhimiza wananchi kutumia nishati mbadala kama gesi ya kupikia *LPG*, majiko banifu na majiko yanayotumia nguvu za jua, yaani *solar power* hususan kwa wakazi wa Mijini ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwambalaswa, swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, misitu ni raslimali ya nchi kama zilivyo raslimali nyingine ambazo Tanzania tumejaliwa. Hekta 400,000 za misitu kwa mwaka ina maana ni miti na magogo mengi sana yanahusika. Sasa swali: Je, hii *industry* thamani yake kwa mwaka ni kiasi gani na inachangia kiasi gani katika mapato ya Serikali kwa njia ya maduhuli au kodi?

Swali la pili; ili kupunguza uvunaji wa misitu hii ambayo inaharibu hata hali ya hewa ya dunia: Je, Serikali ina mpango wowote wa kuwe ku-*recycle* vumbi la kwenye matanuri kule misituni na kwenye masoko ya mkaa huku mjini ambalo unaweza uka-*recycle* ukatengeneza matofali au *cakes* za mkaa, zikapikiwa na kupunguza uvunaji wa misitu?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Spika, kwanza labda niseme tu kwamba, kwa hapa sina takwimu sahihi ambazo zinaweza kuonesha thamani halisi ya *industry*, lakini tukiitoka hapa naomba tukutane ili niweze kukutana na wataalam niweze kumpatia takwimu sahihi kwa sababu kwa hapa sasa hivi sinazo.

Kuhusu ku-*recycle* vumbi zitokanazo na mabaki ya mbao katika maeneo mbalimbali, hili linawezekana kabisa na katika sehemu nyingine utakuta wanachukua lile vumbi la mbao wana-*compress* na kutengeneza vitu kama matofali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS]

na mbao laini au *ceiling board*. Kwa hiyo, hiki ni kitu kinachowezekana. Hivyo namwombe tu Mheshimiwa Mbunge ashirikiane nasi pale ambapo ataona kwamba kuna umuhimu wa kufanya suala hilo tuweze kuona utaalum au teknolojia inayowezekana ili kushirikiane kuitumia teknolojia hiyo. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, siyo siri kwamba tusipochukua hatua za haraka nchi yetu itageuka jangwa. Sasa napenda kujua, kwanini Serikali isichukue hatua za makusudi kusambaza haya majiko banifu kwa sababu ni kweli kwamba majiko banifu kipande kidogo tu cha kuni kinatosha kupika mlo katika familia na ukawa mzuri tu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Spika, ni kweli majiko banifu yanasaidia sana katika kupunguza matumizi ya kuni na miradi mingi katika maeneo mbalimbali inaendelea ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Monduli na hata Wilaya ya Hai kuna miradi ambayo inaendelea kwa ajili ya majiko banifu.

Hata hivyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mipango yetu ya Miji na kwa Sheria yetu ya mazingira Na. 4 ya mwaka 2004 Na. 20, na mkakati tuliojiwekea wa kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira wa mwaka 2006, Halmashauri zimeombwa ziweze kutambua maeneo ambayo zinaweza kuhakikisha kwamba zinalinda mazingira yake ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi ambayo itawasaidia wananchi kutotumia kuni au mkaa.

Namwomba sana Mheshimiwa Mbunge tusaidiane katika maeneo hayo kwa kuweza kutambua maeneo katika Halmashauri zetu.

SPIKA: Mheshimiwa Jafo, swali la nyongeza.

MHE. SELEMAN S. JAFU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi sasa na ukiangalia matumizi makubwa ya mkaa katika nchi yetu inaonesha dhahiri kwamba hakuna *commitment* ya uhakika hasa katika kudhibiti suala zima la uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sasa hivi, takwimu za mvua zinatunyesha, maeneo mengine yaliyokuwa yanapata milimita 1,500 kwa mwaka, sasa hivi yanapata milimita 750. Kwa mfano, ukija katika misitu ya Kazimzumbwi na Ruvu Chini, Kamati ya Maliasili na Mazingira inajua ni jinsi gani imeathirika. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuona kwamba huku juu tumeshindwa suala la utunzaji wa misitu hii lirudishwe katika Halmashauri husika ili mradi tuweze kusimamia kwa karibu zaidi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Kwa kifupi na wewe.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uharibifu wa mazingira ni mkubwa, lakini tutambue kwamba kuna mkakati wa kuhakikisha kwamba tunatunza ardhi na vyanzo vya maji ambao umetambua umuhimu wa kuweka madaraka katika Wilaya zetu.

Ukiangalia Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 imeelekeza kabisa kuanzia Vijiji, Kata, Halmashauri za Wilaya, Sekretarieti za Mikoa, kwamba ndizo zenye wajibu wa kuhakikisha zinatunza mazingira. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge aangalie hiyo sheria na aweze kutekeleza lile ambalo amelipendekeza.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Ritta Kabati, atauliza swali.

Na. 86

Mafao ya Wafanyakazi wa Kiwanda cha Almasi Iringa

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Mwaka 1988 Serikali ilikifunga kiwanda cha Almasi Iringa lakini waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho hawajalipwa mafao yao hadi leo:-

Je, Serikali italipa lini mafao yao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Kukata na Kuchonga Almasi – *Tanzania Diamond – Cutting Company* (ikijulikana kwa kifupi *TAN-CUT*- Almasi) ilianzishwa katika miaka ya 1970. Kampuni hii ilianzishwa ili kuiongezea thamani Almasi yetu iliyokuwa ikichimbwa Mwadui ili isiendeleo kuuzwa ikiwa ghafi. Wafanyakazi wa *TAN – CUT* Almasi kama ilivyokuwa kwa watumishi wengine wa Mashirika ya Umma, hawakuwa Watumishi wa Serikali Kuu bali walikuwa ni watumishi wa Kampuni husika.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, sauti.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kulipa mafao ya Watumishi wa Mashirika ya Umma ulichukuliwa wakati wa Sera ya Kurekebisha Mashirika ya Umma katika miaka ya 2000 baada ya makubaliano baina ya wafanyakazi, Serikali na Wawekezaji. Wawekezaji walipenda kuchukua makampuni bila kuwa na mgogoro wa malipo ya watumishi. Malipo hayo hayakutokana na bajeti ya Serikali bali mapato yaliyotokana na kuuza Mashirika, yaani *Privatisation Proceeds* ambayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

yalisimamiwa na *Parastatal Sector Reform Commission – PSRC*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kampuni ya *TAN-CUT-Almasi* ilifungwa mapema zaidi ya miaka 10 kabla ya zoezi la urekebishaji wa Mashirika ya Umma kuanza, hivyo haikuwepo wakati wa kurekebisha mashirika; na kwa kuwa watumishi wake hawakuwa waajiriwa wa Serikali, Serikali kwa sasa haiwajibiki kulipa mafao ya watumishi hao.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nikiri tu kwa mara ya kwanza kwamba naisikitikia Serikali yangu kwa kunipa majibu mepesi katika suala zito linalowahusu wananchi wa Iringa kama hili. Kwa kuwa kabla sijaleta swali hili nilifanya utafiti wa kutosha na kukaa na hawa wafanyakazi; sasa naomba niulize maswali mawili tu ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali ndiyo ilianzisha shirika hili kama kampuni ya Umma chini ya Shirika la *STAMICO*, sasa kwanini Serikali inawakana wafanyakazi waliokuwa chini ya shirika hilo? Naomba Serikali itoe maelekezo sasa hawa wananchi waende wapi? (*Makofi*)

Swali la pili, hivi Mheshimiwa Waziri amefanya utafiti kiasi gani mpaka kutoa jibu kama hili kwa wafanyakazi wa Iringa, kwa kuwa kuna wafanyakazi ambao tayari wamepoteza maisha na wengine wameathirika kutokana na kutolipwa mafao yao? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba kwanini Serikali inawakana; Serikali haijawakana, hii ni ukweli. Sidhani kama Serikali inataka kweli wananchi wake wapate taabu, lakini kwa sababu kulikuwa kuna *process* ya kurekebisha mashirika na shirika hili lilikufa miaka! Maana yake tukisema ni hawa wafanyakazi tu wa *TAN-CUT*, kulikuwa kuna mashirika labda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

miaka 20 au 30 isingekuwa *fair* kwa Serikali wakati inaingiza mashirika haya kwa ajili ya *privatisation* kwamba iyachukue yale mashirika. Ni kweli wafanyakazi waliathirika, wametolewa kazini, *okay* kiwanda kilifungwa kwa sababu kulikuwa hakuna uzalishaji tena, lakini haimaanishi kwamba Serikali iwe inachukua *burden* ya kila mtanzania aliyekumbwa na kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, wakati tumeingia katika mchakato wa kurekebisha haya mashirika, fedha ambazo zilikuwa zinachukuliwa katika kuwalipa mafao wafanyakazi, zilikuwa ni fedha zinazotokana na wawekezaji. Kiwanda kilikufa zaidi ya miaka 10. Ni ukweli na unauma, lakini ndiyo hivyo. Serikali haiwezi ikabeba *burden* ya mashirika ambayo miaka 30, 40 au 50 nadhani pengine ingekuwa hivyo, basi leo tusingekuwa hapa kwa sababu *all the proceedings* za Serikali ingebidi tuwalipie wafanyakazi ambao miaka 30 au 40 huko nyuma walikuwa wakifanya kazi kwenye viwanda ambavyo vilikufa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, utaratibu ni huo. Kusema kufanya *research* kama uliyofanya wewe Mheshimiwa Mbunge, sikwenda Iringa, lakini nimefanya *desk review* na huo ndiyo ukweli ambao ulikuwepo. Nime-*consult* na watu wa *CHC* ambao walirithi kutoka *PRSC* na hao ndiyo waliokuwa na hiyo *concept* kwamba, *of course* kutokana na *terms of reference* yao mashirika ambayo yalikuwa hayakuwemo katika *process* hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Suala la *TAN-CUT*-Almasi lilianza kudaiwa na mtangulizi wangu Mheshimiwa Monica Mbega kuhusu madai ya wafanyakazi wa *TAN-CUT*. Niungane na Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba majibu ambayo Serikali inatoa ni kuwadhalilisha wafanyakazi wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MCH. P. S. MSIGWA]

TAN-CUT na kutowatendea haki kwa sababu kwa kweli walilitumikia Taifa hili na walifanya kazi kwa uaminifu.

Sasa swali, Serikali ina kumbukumbu za wafanyakazi wale na walilitumikia taifa, ni kwanini isifanye utafiti wa kuleta kumbukumbu na wafanyakazi wale wakalipwa haki zao kuliko kutoa majibu mepesi namna hii kwa wananchi wakazi wa Iringa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa. Vilevile, nachukua rai ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Iringa kwa niaba ya wafanyakazi wa Tanzania *TAN-CUT*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kazi kwa utaratibu, kwa kufuata sheria na kanuni zake. Mashirika yaliyoingia kwenye ubinafsishaji kupitia *PSRC* ni yale ambayo bado yalikuwa yanafanya kazi au yalikuwa yanafanya biashara au *operating companies*. Lakini yale ambayo hakuwepo hayakuingia *PSRC*, sasa huo ndiyo ukweli wenyewe. Lakini la kwamba wafanyakazi wa *TAN-CUT* wana matatizo, ni jambo lingine ambalo Serikali inaweza kulichukua, lakini haiwezi ikashurutisha kwamba iingie *PSRC* wakati haikuwa ni moja ya makampuni ambayo yalikuwa *PSRC*. Labda la umuhimu kwa niaba ya Serikali ni kwamba tuchukue rai hii tuangalie *fate* au hatima ya wale waliokuwa *TAN-CUT*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Azza Hillal Hamad.

Na. 87

Kupandishwa Hadhi Barabara ya Solwa – Didia

MHE. AZZA HILLAL HAMAD (K.n.y. MHE. AHMED ALLY SALUM) aliuliza:-

Barabara ya Solwa – Didia katika Wilaya ya Shinyanga ilishaombewa kupandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa (*TANROADS*):-

Je, ni lini barabara hiyo itapewa hadhi ya kuwa barabara ya Mkoa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi ilipokea maombi ya kuipandisha hadhi barabara ya Wilaya ya Solwa - Didia kuwa ya Mkoa kutoka Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2009/2010. Maombi hayo yalifanyiwa kazi na Kamati ya Kitaifa ya kupanga barabara katika hadhi stahiki na kubaini kuwa barabara hiyo kwa wakati ule haikukidhi vigezo vilivyoainishwa katika Sheria Na. 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, endapo Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Shinyanga itaridhika kuwa kwa sasa, maana baada ya Mkoa ule kuwa na Mkoa mwingine wa Simiyu kuwa itakidhi vigezo vya kuipandisha hadhi barabara hasa kutangazwa Mikoa na Wilaya mpya, napenda kuwashauri wawasilishe maombi hayo tena.

SPIKA: Mheshimiwa Azza, swali la nyongeza.

MHE. AZZA HILLAL HAMAD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, barabara hii ya Didia - Solwa inaunganisha Jimbo la Msalala na Jimbo la Nyang'hwale; na kwa kuwa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2012 ilishakaa na kuridhia kuwa barabara hii inakidhi vigezo hivyo: Je, ni lini Serikali itatoa majibu ya kuipandisha hadhi barabara ya Didia –Solwa na kuwa barabara ya Mkoa?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwaagize Mameneja wa Mikoa wanapoleta mapendekezo ya kupandisha hadhi barabara, wazingatie vigezo vilivyoainishwa kwenye Sheria hii. Zinaletwa barabara nyingi lakini unakuta hazikidhi, na sababu kubwa pengine wengi wanapenda wazilete kwa sababu Serikali ilianzisha Mfumo endelevu wa matengenezo ya barabara. Kwanza kuanzisha Mfuko wa Barabara na pia kwa kuanzisha Wakala wa Barabara *TANROADS*. Sasa kazi ya Mfuko ule imefanya vizuri na kazi ya Wakala ya Barabara inafanya vizuri. Sasa barabara zote zinapendekezwa zipandishwe hadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba nisome tu vigezo ambavyo ni muhimu katika kupandisha hadhi barabara kutoka Wilaya kuwa ya Mkoa. Kwanza, iunganishe Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Wilaya nyingine. Hicho ni kigezo cha kwanza. Kigezo cha pili, iunganishe Makao Makuu ya Wilaya na barabara kuu. Kigezo cha tatu, iunganishe Makao Makuu ya Mkoa na Makao Makuu ya Wilaya. Kigezo cha nne, iendeleze barabara ya Mkoa iliyopo na kuunganisha na barabara ya Mkoa nyingine au barabara kuu. Kigezo cha tano, iunganishe barabara kuu mbili ziendeze sehemu mbili tofauti. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge, vigezo vyote hivi hiyo barabara inakidhi, basi iletwe. Kuna Kamati Maalum ya Wizara itakwenda kukagua na kuhakiki kama kweli hiyo barabara inahitaji kupandishwa hadhi.

SPIKA: Mheshimiwa Silinde, swali la nyongeza.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na vigezo ambavyo Serikali imevitaja, Halmashauri nyingi nchini zimekuwa zikipeleka maombi hayo ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Momba ambayo kupitia kikao chake cha *RCC* cha mwezi Mei, 2012 kilipitisha barabara mbili kubwa kwa mfano kutoka Kakwezi kupitia Kapele llonga kilomita 50.6 Sumbawanga Vijijini pamoja na Mtungwa, Chilumo, Mkuwe mpaka Kasamba kupitia Chilimatundu kwenda Sumbawanga kilomita 51.1 ambazo zimekidhi vigezo hivyo, lakini mpaka sasa Serikali bado haijaleta majibu. Je, ni kwa nini Wizara ya Ujenzi inachelewesha kupitia barabara hizo ili zipandishwe hadhi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Ninasema simu zinafungwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba barabara ambayo inakidhi vigezo inapandishwa hadhi. Zipo barabara ambazo zimepandishwa hadhi, lakini zipo pia barabara ambazo hazikukidhi. Ndani ya Kanuni ya Sheria ile kuna Kamati Maalum ambayo lazima ipitie, ihakiki vigezo ambavyo nimevisoma hapa sasa. Sasa kama barabara ya Mheshimiwa Mbunge bado anafikiri inakidhi vigezo, basi tuwasiliane naye tuweze kuangalia, tulinganishe na hivi vigezo tuweze kuona kama kweli inakidhi au haikidhi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kafumu.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, barabara ya Igunga, Mbutu mpaka Igurubi nayo pia iliombewa kupandishwa hadhi, Serikali itaipandisha hadhi lini barabara hii?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Lazima Waziri awe kompyuta ili aweze kujibu maswali yote haya. Nafikiri ndiyo, basi naomba ujibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, barabara ya Igunga Mbutu; kwanza nadhani haja ya kupandisha hadhi barabara ni kutaka barabara ile ifanyiwe matengenezo. Sasa hivi Serikali imeshaanza kutengeneza daraja la Mbutu. Kwa hiyo, baada ya pale tunafikiria kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Sasa haya nayo ni mambo ambayo yanahitajika. Lakini kama bado anahitaji ipandishwe hadhi, namwomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kuangalia Wizarani yale mawasilisho yaliyoletwa tuweze kuona kama inakidhi kupandishwa hadhi ipande katika ngazi nyingine.

SPIKA: Naomba tuendeleo na swali linalofuata, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo.

Na. 88

**Kujenga Barabara ya Mtwara - Tandahimba
- Newala- Masasi kwa lami**

MHE. JUMA A. NJWAYO aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya lami kati ya Mtwara-Tandahimba - Newala hadi Masasi na kwamba ujenzi utanza kabla ya kumaliza kipindi chake cha Urais mwaka 2015:

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia hatua gani hadi sasa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama vile Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 ilivyoelekeza kwenye Ibara ya 64 (e) ambapo inatakiwa barabara ya Mtwara-Tandahimba -

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Newala – Masasi kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu na ahadi ya Rais ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, Wizara ya Ujenzi tayari imeanza kutekeleza.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga jumla ya Shilingi bilioni 3.1 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii pamoja na daraja la Mwiti.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kumpata Mhandisi Mshauri ambaye atafanya kazi hii zimeanza. Hatua ya kwanza ya kupata orodha (*short listing*) ya Makampuni ya Wahandisi washauri watakaoshiriki katika zabuni hii imekamilika. Makampuni yaliyoorodheshwa yamepatiwa makabrasha ya zabuni na zabuni hizi zinatarajiwa kuwasilishwa tarehe 7 Novemba, 2013. Tathmini itafanyika mara baada ya mawasilisho ya zabuni ili kumpata Mhandisi Mshauri ambaye atafanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

SPIKA: Mheshimiwa Njwayo, swali la nyongeza.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kiasi fulani naomba kuishukuru Serikali kwa sababu imeanza kidogo kutoa maelezo ya matumaini kwenye barabara hii. Lakini pamoja na hayo, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

La kwanza, mimi ninavyoamini Serikali ina Mpango Mkakati wa kila jambo lake. Sasa nadhani ni wakati umefika sasa basi, kueleza ni lini sasa ujenzi wa barabara hii kuwa ya lami utaanza?

La pili, sambamba na hili tumekuwa na matatizo ya barabara ya Ndundu - Somanga. Tuliahidiwa hapa kwamba mwezi Desemba, 2013 barabara hiyo itakamilika, lakini hali iliyoko kule haifanani na ahadi inayotolewa hapa. Mkandarasi aliyeko pale amebwaga vifaa vyake na hakuna kinachoendelea. Serikali itueleze, tatizo ni nini na nini? Kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. A. NJWAYO]

mpango gani wa haraka wa kutatua tatizo hili ili pale pasiendelee kutusumbua? Tena kilomita 14 tu zilizobaki, kwenye kilomita 60 ambazo zilikuwa tatizo! Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza tunazipokea pongezi kwa namna Serikali inavyoshughulikia mipango yake.

Suala la lini ujenzi utaanza, labda niseme tu kwamba suala la upembuzi yakinifu Waheshimiwa Wabunge ni hatua moja muhimu sana katika ujenzi wa barabara za lami. Katika upembuzi yakinifu tunaangalia ni vigezo vipi katika masuala ya uchumi, masuala ya kijamii, magari ya aina gani yatapita, kona ngapi, madaraja mangapi. Kwa hiyo, ni lazima kazi hii ya upembuzi ifanyike vizuri ili barabara ile iweze kudumu katika muda ule ambao unategemewa.

Kwa hiyo, naomba sana, ukishaona upembuzi yakinifu umeanza, ni hatua muhimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Juma Njwayo ni kwamba tutakapomaliza upembuzi yakinifu, tutakuja kufanya usanifu sasa kujua barabara iwe na unene wa kiasi gani, tuweze kujua gharama za barabara ile. Sasa tukishajua ni kiasi gani barabara ile itagharimu, basi ndiyo tutaanza kufanya *process* sasa ya kuanza kupitisha zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, nilijibu juzi kwamba suala la Ndundu – Somanga, Waheshimiwa Wabunge ni lazima itakamilika. Serikali imedhamiria kujenga barabara hii. Tumeshajenga zaidi ya kilomita 450 kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi, hatuwezi kushindwa kujenga kilomita 17 zilizobaki. Kwanza, sehemu kubwa ya kazi ya Mkataba huu, asilimia 90 ya kazi imeishakamilika. Kilichotokea wakati Mheshimiwa Njwayo amepita pale, mtambo wa lami siku ile ulikuwa umeharibika. Kama mtambo umeharibika siku ile, lazima Mkandarasi autengeneze ili aweze kuendelea. Lakini *otherwise* mpaka kilomita tano sasa hivi zimekwishafanyiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

priming na kazi ile inaendelea. Hivi sasa ninapoongea kazi ya kuweka lami inaendelea.

Kwa hiyo, nina hakika kwamba mwezi Desemba, 2013 ikifika kama Mkandarasi huyu atakuwa hajamaliza, tutaanza kumkata tozo ya kuchelewesha kazi hii kulingana na mkataba uliopo.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kilufi, swali la nyongeza.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Barabara ya Rujewa – Madibira – Kinyanambo imekuwepo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa muda mrefu na Mheshimiwa Rais alishaweka ahadi kwamba hiyo barabara itakamilika miaka zaidi ya 30 sasa iliyopita, na imekuwa ikitengewa fedha kidogo kidogo kwenye bajeti kwamba wataanza na madaraja, lakini imekuwa ni hadithi, hakuna utekelezaji. Nataka kujua ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa barabara hii muhimu ya kiuchumi kwa maana ya kutoa mazao kule na kuyapeleka maeneo mbalimbali katika nchi yetu kama ambavyo barabara nyingine zimefanyiwa? Kuna tatizo gani barabara hii haitaki kutengenezwa? Upembuzi yakinifu na taratibu zote zilishakamilika.

SPIKA: Inatosha, umeshajieleza vizuri. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya kutoka Madibira mpaka Kinyanambo na ndiyo maana imeshafanya usanifu. Lakini ilipofika mahali ikaonekana kwamba barabara ile inapita ndani ya Hifadhi, kwa hiyo, ikabidi tuanze kufanya mapitio ya usanifu ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa vile tayari Serikali imeishaji-*commit* kufanya usanifu, ninaamini kabisa hatuwezi kuwekeza fedha halafu tuiache barabara ile. Kwa hiyo, barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ngonyani, swali la nyongeza.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, tatizo la Tandahimba linalingana kabisa na tatizo la kule Korogwe Vijijini hasa Korogwe, *Old Korogwe* kwa Shemshi, Bumbuli na kutokea Soni; Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliahidi kuweka lami barabara hiyo: Je, lami hiyo itawekwa lini?

SPIKA: Haya. Swali la nyongeza kila mtu la kwake, tukimuuliza hapa atajibu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Ngonyaji kwamba Serikali iliahidi, nami nataka nimhakikishie kwamba ahadi za Serikali, ahadi za Rais zipo pale pale tunajipanga, tunatafuta fedha, tunaweka kwenye Mpango na juzi mmepitisha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015; sasa tutakapofika kwenye kuweka fedha zinazotakiwa kwa barabara hii, Mheshimiwa Mbunge basi ulete mapendekezo ili kusudi tuiwekee fedha za kujenga barabara hiyo katika kiwango ambacho kinastahiki.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Martha Mlata.

Na. 89

Watu wenye ulemavu kuhangaika kutafuta Misaada

MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. AL- SHYMAA J. KWEGYIR) aliuliza:-

Walemavu wamekuwa ni watu wa kuhangaika kwa kuomba misaada ya kiafya na kielimu:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. M. MLATA (K.n.y. MHE. A. J. KWEGYIR)]

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la kuhangaika kwa walemavu?

(b) Je, ni walemavu wangapi mpaka sasa wameshapewa matatibu ya bure au kusomeshwa na kupatiwa ajira kwa wale wenye vigezo vinavyotakiwa?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kupitia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004, Serikali inatekeleza mipango mbalimbali kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Mipango hiyo ni pamoja na utoaji wa haki na ulinzi kwa watu wenye ulemavu katika masuala ya elimu, ajira na mafunzo ya ufundi. Vilevile, watu wenye ulemavu wasiojiweza kabisa na wasio na ndugu wanatunzwa katika makazi ya watu wenye ulemavu na wasiojiweza.

(b) Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya kuhusu msamaha wa matibabu unawatambua watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na wazee. Pia utaratibu unatambua watu sio na uwezo ukiwajumuisha watu wote, walemavu wakiwemo. Kwa sasa Serikali haina mfumo wa kupata takwimu kitaifa kwa watu wenye ulemavu wanaopata msamaha wakati wa kupokea huduma za tiba peke yao bali hujumuisha makundi mengine yenye stahili za msamaha kwenye ngazi ya Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mazingira ya kumwezesha mtu mwenye ulemavu kupata elimu kupitia elimu jumuishi kwenye shule na vyuo bila ubaguzi. Aidha, zipo shule na Vyuo Maalum kwa watu wenye ulemavu, kwa wale ambao hawawezi kupata elimu jumuishi. Kwa sasa kuna juma la wanafunzi 94, wenye ulemavu walio katika Chuo cha Marekebisho ya Watu Wenye Ulemavu cha Yombo, miongoni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

mwao Wanawake ni 40 na wanaume ni 54 na katika Chuo cha Wasiiona Singida kuna walemavu wapatao 19. Kati yao, wanafunzi wanawake ni nane (8) na wanaume 11.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Watu wenye ulemavu Na. 9 ya 2010, kila mwajiri anatakiwa kuajiri asilimia tatu ya watu wenye ulemavu. Kwa sasa Serikali ina jumla ya watumishi 500,028. Miongoni mwao watu 2,025 ni watu wenye ulemavu, sawa na asilimia 0.4. Wizara yangu itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria hii ili kuona kwamba watu wenye ulemavu wanapata huduma za elimu, ajira na afya sawa na watu wengine.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Martha, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naomba tu anisaidie kwamba pamoja na juhudi kubwa sana ya Serikali kutaka kusaidia watu wenye ulemavu, watoto na wajawazito kama alivyosema, lakini bado imekuwa ni vigumu sana kutimiza azma yake kwa sababu hakuna Wizara maalum ambayo imekuwa ikishughulikia moja kwa moja masuala ya watu wenye ulemavu na kutawanywa Maendeleo ya Jamii ama Wizara ya Afya. Je, Serikali haioni kwamba sasa ikabidhiwe Wizara moja ili iweze kushughulikia moja kwa moja masuala ya watu wenye ulemavu?

La pili, kwa kuwa ni kweli wamekuwa wakienda kupata huduma kwenye Vituo vya Afya ama Hospitali kwa ajili ya afya, lakini bado wamekuwa wakipata huduma bure kumwona Daktari na vipimio. Inapofika kwenye masuala ya dawa, unakuta wanatakiwa wajitegemee kwa sababu dawa zinakuwa na upungufu. Je, kwa nini hakuna utarataibu wa kuweza kuwasaidia hawa watu wenye ulemavu pale wanapokosa dawa pale Hospitali? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, naomba majibu.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba masuala ya walemavu yapo chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii ambayo ni Idara chini Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Pia kuna Idara zinazotakiwa ziwepo katika ngazi ya Halmashauri za Ustawi wa Jamii ambazo kwa sasa bado hazijaundwa rasmi, lakini ndiyo maana huu mkanganyiko unaonekana kwamba masuala ya Ustawi wa Jamii baadhi ya Halmashauri zilikuwa zinashughulikiwa na Idara za Maendeleo ya Jamii. Tatizo hili tumeliona marekebisho yanafanyika ili ziundwe Idara Rasmi za Ustawi wa Jamii katika ngazi za Halmashauri zishughulikie masuala ya walemavu moja kwa moja bila mkanganyiko ambao unaonekana hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kwamba katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya kunakuwa na tatizo la upatikanaji wa dawa au upungufu wa dawa. Ninachoweza kusema ni kwamba tatizo hili siyo kwa walemavu peke yao, tatizo hili linawakumba watu wote wanaopata huduma za afya. Mikakati tunayoiweka sasa ni kuhakikisha kwamba kwanza kuna matumizi bora ya dawa yanapatikana kwa kuweka nembo maalum katika dawa kwasababu kulikuwa na upotevu mkubwa. Hilo la kwanza.

La pili, matumizi ya fedha zinazopatikana kutokana na uchangiaji; uwe uchangiaji wa papo kwa papo, uwe ni uchangiaji wa mifuko ya afya ya jamii au Bima ya Taifa, lazima fedha zile zitumike kununua dawa za ziada ili kuondoa uhaba kwa wagonjwa wakiwemo hao walemavu.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

MHE. KHALIFA SULEIMANI KHALIFA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, nina swali moja la nyongeza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. K. S. KHALIFA]

Mheshimiwa Spika, moja katika kundi la watu wanaopata matatizo makubwa ni walemavu ambao wamekosa miguu. Hospitali mbili; ya Muhimbili na ya *KCMC* mara nyingi ndiyo zinatengeneza miguu kwa walemavu hawa. Sisi wenye miguu yetu, Sh. 400,000/= au Sh. 500,000/= zinatutia mitihani: Je, hawa waliokosa miguu watapata wapi Sh. 500,000/= za kwenda kununua miguu? Serikali inasemaje katika kusaidia kundi hili pale wanapokwenda hospitali wakashindwa kuwa na pesa za kununulia hiyo miguu ya bandia? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo walemavu ambao wanahitaji viungo bandia ikiwemo hiyo miguu. Ni kweli pia kwamba Taasisi ya *MOI* pamoja na *KCMC* viungo hivyo hupatikana kwa gharama fulani.

Utaratibu uliowekwa ni kwamba, kwanza tuelewe kwamba siyo walemavu wote hawana uwezo. Wale ambao wana uwezo wanatakiwa kuchangia huduma hiyo, lakini wale ambao hawana uwezo, kuna kitengo maalumu cha Ustawi wa Jamii katika hospitali hizo zinatakiwa kuangalia kama kweli hawana uwezo huo waweze kuwasadia kwa fedha za Serikali. Yaani kwa maana nyingine, kuna misamaha. Lakini ni lazima nikiri hapa kwamba siyo mara zote wale ambao hawana uwezo wanapata huduma hii kwasababu mara nyingi vitengo hivyo vinaishiwa, vinakuwa havina fungu la kupata vifaa hivyo.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba Wizara yangu itaangalia uwezekano wa kuongeza bajeti katika eneo hili la kuwapa viungo bandia walemavu ili kuwaondolea hilo tatizo la kukosa kwa viungo hivi endapo hana uwezo wa kulipia.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mbassa, swali la nyongeza.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Suala la ulemavu kidogo lina tafsiri pana. Kuna watu wanapata ulemavu kwa kukosa huduma kidogo ambayo kama ingeweza kutolewa ingeweza kuwaondolea ulemavu. Kwa mfano, wanaopata upofu kwasababu ya kukosa tiba au upasuaji wa jicho: Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaruhusu wale wataalamu walio staafu kufungua vituo kwa ajili ya kutoa huduma hii?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchini kwetu kuna walemavu wengi wa macho ambao pengine kama wangepata tiba mapema wangeweza kutopata ulemavu huo. Vile vile yako Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo yanasaidiana na Serikali katika kutoa huduma hizi ili kuwaepushia ulemavu huo wanaoathirika.

Serikali haina pingamizi hata kidogo kwa madaktari ambao wanaweza kufungua Vituo vya kutoa huduma hizi, wawe wamestaafu au wawe katika Sekta Binafsi tu ili kuweza kutusaidia kama Serikali katika kutoa huduma hii.

Sioni tatizo, wanakaribishwa kufungua vituo hivyo na Serikali itawapa wepesi wa kufanya shughuli zao ili kuwaondolea wananchi matatizo hayo.

SPIKA: Ahsante. Naomba tuendelee na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Amina Abdallah Amour atauliza swali hilo, kwa niaba yake namwona Mheshimiwa Habib Mnyaa.

Na. 90

Sekta ya Uvuvi Kupewa Kipumbele

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA (K.n.y. MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR) aliuliza:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. J. MNYAA (K.n.y MHE. A. A. AMOUR)]

Je, kwa nini Serikali haitoi kipaumbele kwenye Sekta ya Uvuvi kwa kuwawezesha Wavuvi wadogo wadogo zana za kisasa kupitia MKUKUTA?

WAZIRI WA KILIMO NA MAENDELEO YA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA, Sekta ya Uvuvi imeendelea kupewa kipaumbele ambapo Serikali kupitia programu ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi imeainisha maeneo ya utekelezaji unaolenga kuwa na uvuvi wenye tija. Baadhi ya maeneo hayo ni kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi, kuimarisha masoko na usalama wa mazao ya uvuvi, kuboresha elimu ya uvuvi endelevu, kuongeza ukuzaji wa viumbe kwenye maji, kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika Sekta Binafsi, kuboresha utaalamu na matumizi ya teknolojia sahihi ili kufanya shughuli za uvuvi na ufugaji wa samaki ziwe zenye tija.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekuwa ikibuni na kutekeleza miradi mbalimbali ambayo ni pamoja na mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (*MACEMP*) uliotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2012. Jumla ya wavuvi 4,000 waliwezesha kwa kutekeleza miradi ya uvuvi 240 yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.8. Aidha, wavuvi 634 wanaoishi katika Hifadhi za Bahari Mafia, Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma, walipewa ruzuku ya kununua injini za boti 22, madema 20, maboya 26,000, boti 28 za uvuvi na nyavu 1,403 zilizogharimu Shilingi milioni 339.35.

Vilevile Serikali kupitia *DADPs* kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ilitoa Shilingi milioni 59.7 kwa vikundi nane kwa ajili ya kununulia injini, boti na zana za uvuvi na vilevile Serikali inajenga kiwanda cha kutengeneza boti kule *Mbamba Bay* Wilaya ya Mbinga ili kuwawezesha wavuvi wadogo kupata boti imara na zana bora za uvuvi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA KILIMO NA MAENDELEO YA UVUVI]

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali itaanzisha mfumo wa ruzuku kwa uvuvi wadogo wadogo itakayotolewa kwa utaratibu wa mfuko wa mzunguko (*Revolving Fund*). Ruzuku hiyo itatumika kununua boti za uvuvi na viambata vyake na zana bora za uvuvi. Aidha, ruzuku itatolewa kwa vikundi vya wavuvi vilivyosajiliwa na vinavyofanya shughuli za uvuvi. Chini ya utaratibu huu, maboti 50 na viambata vyake pamoja na nyavu za uvuvi 15,562 vinatolewa kwa wavuvi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. (*Makofi*)

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, katika jibu la Mheshimiwa Waziri miradi miradi aliyoitaja ya *MACEMP* na *DADPs* ni miradi ya Kitaifa ambayo imefanyika katika Jamhuri nzima ya Muungano na kwa kuwa mwuliza swali, Mheshimiwa Amina anatokea upande wa Zanzibar wa Jamhuri ya Muungano, na kwa kuwa mifano ya wavuvi waliofaidika 4,000, miradi 240, milioni 3.8 mifano iliyotolewa ya Ghuba ya Mnazi, Rufiji, Ruvuma ni upande mmoja wa Jamhuri:-

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatueleza kwa upande mwingine wa Jamhuri kwa mifano kama hii aliyoifanya ni wavuvi wangapi wamefaidika na ni maeneo gani?

Swali la pili, kwa kuwa Bunge hili tumejitahidi sana kuhangaikia kupata Benki ya Wakulima na mchakato umekuwa mzuri na karibuni itafunguliwa Benki ya Wakulima: Je, kama nchi hii kweli tuna nia ya kufaidisha na wavuvi: Je Serikali itatoa tamko sasa kuwa iko tayari kuanzisha Benki ya Wavuvi ili nao wafaidike? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Eng. Mnyaa kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA KILIMO NA MAENDELEO YA UVUVI]

La kwanza hili la *MACEMP*, *MACEMP* inatekelezwa katika pande zote mbili na *MACEMP* ipo Bara na Zanzibar. Napenda kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa imetekeleza *MACEMP* vizuri sana kuliko hata upande wa Bara. Wamefanya miradi mingi mizuri na wavuvi wengi wamefaidika pande zote kwa maana ya Pemba na Unguja. Kwa hiyo, suala hili naweza kukuletea *data*, lakini ungeweza kupata takwimu hizi vizuri kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Swali la pili la Benki ya Wakulima; kwanza niseme tu kuwa *Agriculture* kwa ujumla wake inahusisha mifugo, misitu, uvuvi; kwa hiyo, tukisema Benki ya Kilimo siyo kwa maana ile ya kwamba ni kilimo kile cha jembe tu, bali ni pamoja na mifugo, uvuvi na mambo kama hayo. Sasa hivi wafugaji na wavuvi wanachukua mikopo kwenye Benki ya Rasilimali wakati mchakato wa kukamilisha Benki ya Kilimo unaendelea.

SPIKA: Mheshimiwa Buyogera swali la mwisho la nyongeza.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha inawawekea mazingira mazuri wananchi ya kutafuta pato la kiuchumi, kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa wavuvi wadogo wadogo wa Wilaya Kibondo na Kasulu wanaovua samaki katika Mto Malagarasi, hasa kutokana na Wizara ya Maliasili na Utalii kutotambua leseni wanazopewa, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi Mbunge wao wa Jimbo la Kasulu Vijijini kusikiliza kilio cha wavuvi hawa wadogo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza maeneo ya uvuvi yaliyoko kwenye Hifadhi baada ya kupata leseni ya uvuvi ni lazima pia upate ruhusa kutoka kwenye Mamlaka husika ya Hifadhi ile ili uweze kuvua. Ni sawa na madini yanayopatikana maeneo ya Hifadhi, ni lazima upate kibali cha maliasili ndiyo unaweza kuvuna rasilimali yoyote iliyoko kwenye eneo la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA KILIMO NA MAENDELEO YA UVUVI]

maliasili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nakubaliana na wewe, wakati muafaka ukifika tutaambatana ili tuweze kusikiliza matatizo ya wananchi wako.

SPIKA: Naomba tuendeleo, kwasababu maswali yamebaki mengi na muda ni mfupi. Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi atauliza swali linalofuata.

Na. 91

Huduma Muhimu Kwa Wafugaji

MHE. SLYVESTER M. KASULUMBAYI alijibu:-

Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ya mwaka 2010, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya mifugo ni ng'ombe takriban milioni 19.2, mbuzi milioni 13.7, kondoo milioni 3.6 na kwa takwimu hizo ni dhahiri kuwa wafugaji wote wanajulikana walipo na wanatembelewa katika mazizi yao na kupata takwimu za idadi hiyo ya mifugo:-

Je, kwa nini Serikali inashindwa kuwapatia wafugaji hao huduma za msingi kama vile majosho, malambo, visima vya maji safi, shule, zahanati na barabara?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na sensa ya mwaka 2012 idadi ya mifugo nchini ni ng'ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.6, na kondoo milioni 7.0. Pia wapo kuku wa asili milioni 35.5, kuku wa kisasa milioni 24.5 na nguruwe milioni 2.01.

Mheshimiwa Spika, jamii huibua miradi kupitia mipango shirikishi inayobaini fursa na vikwazo vya maendeleo kulingana na vipaumbele vya jamii husika. Miradi iliyobuniwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA KILIMO NA MAENDELEO YA UVUVI]

au kuibuliwa na wadau hujumuishwa katika mipango ya kuendeleza kilimo ya Wilayani yaani (*DADPs*) ambayo imekuwa ikitengewa fedha kila mwaka kupitia programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini, yaani (*ASDP*). Kupitia mpango huu wa *DADEPs* Serikali imekuwa ikiwapatia wafugaji huduma za msingi ikiwa ni pamoja na huduma za majosho kwa lengo la kudhibiti kupe na magonjwa mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003/2004 hadi hivi sasa Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya imekarabati majosho 835 kwa gharama ya Shilingi bilioni 5.8 na kujenga majosho mapya 439 kwa gharama ya Shilingi bilioni tisa. Vilevile wadau wengine katika kipindi hicho walichangia ukarabati wa majosho 78 kwa gharama zao. Katika mwaka 2013/2014 yaani katika bajeti ya mwaka huu, 2013 Serikali itakarabati majosho 20 na kujenga majosho mapya 14 kwa gharama ya Shilingi milioni 514.4.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kupitia *DADPs* kila mwaka kwa madhumuni ya kutekeleza miradi inayolenga kuongeza upatikanaji wa maji kwa matumizi ya mifugo na wafugaji. Katika mwaka 2012/2013 kiasi cha Shilingi bilioni 1.5 kilitengwa kuwezesha ujenzi wa malambo mapya 35 na uchimbaji wa visima virefu saba. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.01 kupitia *DADPs* kwa ajili ya ujenzi wa malambo 12 na visima virefu 9. Aidha, Wizara imetenga jumla ya Shilingi bilioni 3.12 kwa ajili ya ujenzi wa malambo, majosho na visima virefu katika Wilaya za Chunya, Lindi, Rufiji, Kilindi, Same, Kiteto, Kishapu na Maswa.

SPIKA: Mheshimiwa Kasulumayi, swali la nyongeza.

MHE. SLYVESTER M. KASULUMBAYI: Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi za idadi ya mifugo, ni dhahiri kwamba wafugaji wanaingiza fedha nyingi sana katika kukuza uchumi wetu: Je, ni kwa nini Serikali haijaona umuhimu wa kuruhusu wafugaji kutumia mifugo yao kama dhamana ili waweze kupata mikopo kama wanavyopata watu wengine? (*Makofi*)

SPIKA: Naomba ujibu kwa kifupi, kwa sababu majibu yako yalikuwa marefu mno.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, suala la dhamana ni suala la kibiashara. Kama mnakubaliana na benki husika ya kibiashara, unaweza kuwa na kikundi chako cha wafugaji, wakakubaliana na benki, basi wakapata mikopo kwa kutumia dhamana ya ng'ombe.

SPIKA: Mheshimiwa Mshama, swali fupi la nyongeza, muda umekwisha.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nilikuwa nataka tu hapo hapo alipojibu Mheshimiwa Waziri kwamba wafugaji peke yao bila kutengenezewa Sera, hawawezi kufanikiwa kupata mkopo kwa kutumia wanyama wao. Je, Serikali iko tayari kuweka hiyo Sera ili kusudi mabenki yakubali kuwasaidia? *(Makoff)*

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, Sera ni suala ambalo linashirikisha Serikali na Wabunge katika kuiandaa. Kama ipo haja hiyo, tunaweza kulileta na kulizungumza, ni suala ambalo linaongeleka.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele atauliza swali hilo.

Na. 92

Kuanzisha wakala wa upimaji ardhi nchini

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. M. MASELE]

Nchi yetu inakabiliwa na tatizo sugu la ujenzi wa makazi holela mijini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha wakala wa upimaji ardhi nchini ili kurahisisha upimaji wa miji na ardhi?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo tatizo la ardhi isiyopimwa nchini ambapo hadi sasa ni takribani asilimia 10 tu ya ardhi yote ndiyo iliyopimwa. Vile vile Serikali inatambua kuwa nchi yetu inakabiliwa na tatizo sugu la ujenzi wa makazi holela mijini ambao unatokana na upungufu wa viwanja vilivyopimwa ikilinganishwa na mahitaji ya wananchi wengi wanaohamia mijini. Kutokana na uhaba wa nyumba, wahamiaji wapya mijini hulazimika kujijengea makazi bila kuzingatia masharti ya Sheria ya Mipango Miji. Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 imeweka masharti kuwa ujenzi wa nyumba mijini ni sharti upate kibali cha ujenzi, yaani (*building permit*) kutoka kwenye mamlaka husika kabla ya ujenzi kuanza.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ianzishe Wakala wa upimaji ardhi, limepokelewa kwa mchango muhimu kwani Wizara yangu ilikwishaanza kufanya utafiti wa awali (*survey*) juu ya faida za kuanzisha Wakala wa Upimaji Ardhi na Uthamini. Mambo ya msingi ya kuzingatiwa kabla ya kuanzisha Wakala wa Serikali ni pamoja na athari zake kisera, gharama za uendeshaji, na mengine yanayowiana nayo. Wizara inaendelea kukusanya taarifa kutoka nchi mbalimbali zinazothibitisha kuongezeka kwa ufanisi wa upimaji ardhi kupitia kwa Wakala ikilinganishwa na Idara chini ya Wizara. Ikiwa itathibitika kuwa kuanzishwa kwa Wakala kutaharakisha utekelezaji wa malengo ya kisera na kisheria katika upangaji,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI]

upimaji na umikilishaji ardhi, Serikali itachukua hatua zifaazo kuanzisha chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi holela unazidi kuharibu mazingira ya miji na nchi kwa ujumla, natoa wito kwa viongozi na Watendaji wa Mamlaka ya Upangaji Miji nchini kuwa watumie rasilimali chache zilizopo kupanga, kupima na kumilikisha wananchi viwanja ili kuboresha mazingira ya miji yetu.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Masele, swali la nyongeza.

MHE. AUGUSTINE M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba nchi yetu ina tatizo la upimaji wa ardhi na kwamba ni asilimia kumi tu ndiyo iliyopimwa; akakiri kwamba kuna maeneo mengine ambayo wameanzisha Wakala na wanafanya vizuri hata nje ya nchi; lakini hata hapa nchini kuna Wakala kama *TRA, TPAA*...

SPIKA: Nina wasiwasi utapoteza swali.

MHE. AUGUSTINE M. MASELE: Mheshimiwa Spika, hata hapa nchini kuna Wakala wanaofanya vizuri. Sasa nauliza, kwanini Wizara hii ya Ardhi inachelewa kuanza na Wakala huyu ili iweze kutusaidia katika kupima maeneo ya ardhi yetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ni mpya, tuna upungufu wa watumishi na vifaa: Wizara inatusaidiaje? Ahsante.

SPIKA: Maswali mengine mazuri. Mheshimiwa Waziri majibu yako kwa kifupi na wewe kwasababu majibu yako yalikuwa marefu leo.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Spika kuhusu kuharakishwa kuanzishwa kwa Wakala, katika jibu la swali la msingi nilielezea umuhimu wa kufanya utafiti kabla ya kukimbilia kuanzisha chombo ambacho ni kipya. Ziko hasara za kufanya kazi kwa haraka haraka bila kufanya utafiti wa kutosha. Nimeelezea kwamba unaweza kuanzisha chombo, kisera kikawa na athari zake. Kuna suala la gharama za uendeshaji wa vyombo hivi vipya tunavyoanzisha. Lazima tuangalie inaathari vipi gharama za uendeshaji, inaongoza ufanisi kiasi gani; na kwamba Taifa linanufaika kwa jumla? Tutakapokamilisha utafiti huo, ndipo tutakapopeleka mapendekezo Serikalini ya kuanzisha chombo hicho ikiwa tutaona kama kitakuwa na faida.

Swali la pili juu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe kama ni mpya inahitaji kusaidiwa kupangiwa Mji. Mheshimiwa Mbunge tuliwahi kukutana ofisini kwangu na nilimwahidi kwamba tutashirikiana na Halmashauri yake watakapokuwa wameleta ombi katika kuandaa *master plan* ya Mji ule. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba kwa kuwa sasa hivi tunaanza kuandaa bajeti ya mwaka 2014/2015, Halmashauri hiyo itenge fedha kwenye Bajeti hiyo, ili tushirikiane nao kufanya kazi hiyo ya kuandaa *master plan* ya Mji huo.

SPIKA: Nashukuru sana. Twende kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, ina maswali manne ya dakika kumi. Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli anauliza swali hilo kwa niaba yake, namwita Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

Na. 93

**Kujenga Jengo la Mahabusi na Ukarabati Nyumba za
Watumishi wa Magereza Rufiji**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MHE. KURUTHUMU
J. MCHUCHULI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo la mahabusu na kukarabati nyumba za Watumishi wa Magereza zilizopo katika Gereza la Mng'avu Wilayani Rufiji?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gereza analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge linaitwa Gereza la Kibiti na linafahamika pia kwa jina la Mng'alu. Serikali inaendelea na juhudi za kujenga, kukarabati na kukamilisha majengo ya Magereza nchini kwa awamu na kilingana na uwezo wa bajeti iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imejenga bweni moja lenye uwezo wa kuhifadhi wahalifu 80 na itaendelea kujenga mabweni mengine katika gereza hilo awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya uboreshaji wa makazi ya askari, mkakati wa kutumia vifaa vya ujenzi vinavyopatikana katika maeneo husika kwa nia ya kupunguza gharama za ujenzi unatekelezwa nchini kote ikiwemo Gereza la Kibiti ambapo tayari nyumba moja imeshajengwa na kukamilika. Pamoja na kukamilika kwa nyumba hiyo, pia maandalizi ya ujenzi wa nyumba nne yameanza kwa kufyatua na kuchoma matofali 3,000 na ufyatujaji wa matofali mengine 9,000 unaendelea.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Abdallah.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri na maswali mawili ya madogo ya nyongeza.

(1) Kwa kuwa kuna msongamano mkubwa sana wa mahabusu wa wafungwa katika Gereza la Mng'alu, na kati ya hao wanaishi katika bweni ambalo hivi sasa linavuja, jambo ambalo linaathiri afya za wafungwa na mahabusu hao: Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuweza kukomboa afya ya mahabusu na wafungwa hao?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. A. ABDALLAH]

(2) Kwakuwa pale wako Maafisa wa Magereza wamejitolea kuchimba bwawa la kufuga samaki na Serikali ikaahidi kupeleka fedha ili kusaidia mradi ule, lakini hadi leo wameshindwa kupeleka fedha ile: Je, ni lini fedha ile itapelekwa ili Maafisa hawa wa Magereza waweze kuendesha shughuli zao za maendeleo?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba tunatambua matatizo yaliyopo kwenye Gereza lile na hasa maeneo yanayovuja kwa kiasi fulani, lakini bado uwezo wa Gereza na idadi ya wafungwa na mahabusu tulionao sasa haijazidiwa kupita kiasi. Lakini yale matatizo madogo yakuvuja na nini, tumeshaanza kuyafanyia kazi, baada ya muda siyo mrefu yatakuwa yamekamilika.

Kuhusu eneo ambalo watumishi wenyewe wa Gereza na wakazi wa pale wameshachangia tumezingatia, tutachukua hatua kuona mchango wao haupotei bure.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Asha Mohamed Omari.

Na.94

Kuanzishwa kwa Kikosi cha *Anti Robbery*

MHE. ASHA MOHAMED OMARI aliuliza:-

Kutokana na kuongezeka kwa matukio ya ujambazi nchini, Jeshi la Polisi lilianzisha Kikosi cha Anti Robbery na kupewa pikipiki kama vitendea kazi:-

Je, ubunifu huo umepunguza uhalifu kwa kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kikosi Maalum cha Kupambana na Unyanga'nyi wa Kutumia Silaha (*Anti Robbery*) kilianzishwa mwaka 2006. Tangu kuanzishwa kwa kikosi hiki, matukio mengi yamedhibitiwa na kupunguza kwa kiasi kikubwa uporaji wa kutumia silaha katika Tasisi za Kifedha. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 matukio hayo yaliweza kupungua kwa asilimia 5.2 ukilinganisha na mwaka 2006/2007 ambapo ujambazi wa kutumia silaha uliongezeka na kufikia asilimia 9.2 ya makosa makubwa. Tukio la hivi karibuni la tarehe 19/08/2013 Jijini Dar es Salaam ambapo majambazi watatu wenye silaha waliweza kudhibitiwa eneo la *TAZARA* ni kielelezo tosha cha juhudi za Kikosi hiki katika kupunguza ujambazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na Jeshi la Polisi, kufichua majambazi wenye silaha na kuwataka majambazi kusalimisha silaha zao kwa hiari kwenye Vituo vya Polisi au Mamlaka nyingine za kisheria kabla Sheria hajachukua mkondo wake.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Asha, swali la nyongeza.

MHE. ASHA MOHAMED OMARI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanatoa elimu kwa Watanzania. Pamoja na shukurani hizo, nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hadi hivi sasa majambazi waliokamatwa na *Anti Robbery* ni wangapi ambao wamefikishwa Mahakamani na kufungwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, majambazi wote waliokamatwa na *Anti Robbery* walichukuliwa hatua za kisheria baada ya kuthibitika.

SPIKA: Tunaendelea na Nishati ya Madini Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, kwa niaba yake namwita Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 95

Kupeleka umeme kwenye kituo cha Afya cha Changuge.

MHE. LAMECK O. AIRO aliuliza:-

Mradi wa Umeme Vijijini kupitia REA unasaidia sana kuimarisha maendeleo vijijini:-

Je, ni lini mradi utapeleka umeme katika Kituo cha Afya cha Changuge kilichopo Kata ya Mirare.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme katika Kituo cha Afya cha Changuge Kata ya Mirare ni miongoni mwa kazi za upelekaji umeme katika Mkoa wa Mara zitakazotekelezwa na Serikali kupitia mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili chini ya Wakala wa Nishati Vijini. Mradi huo kwa Mkoa mzima utahusisha shughuli zifuatazo:-

- (1) Ujenzi wa njia za umeme msongo wa kilovolti 33 zenye urefu wa km 1,193;
- (2) Ujenzi wa njia za umeme msongo wa volti 400 zenye urefu jumla ya urefu wa km 493;
- (3) Ufugaji wa *transforma* 215; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

- (4) Kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 14,523.

Mheshimiwa Spika, mradi huo utatelekezwa na kampuni ya *DERM Electrics (T) Ltd.* iliyochaguliwa mwezi Septemba, 2013 kufanya kazi za ujenzi wa miundombinu katika Mkoa huo, ikiwamo utekelezaji wa mradi huu. Hivi sasa kampuni hiyo inakamilisha maandalizi ili utekelezaji wa mradi huo utakaogharimu Shilingi bilioni 48.91 uanze.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini ningependa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza natambua Mradi wa kupeleka umeme vijijini na faida zake, lakini ningependa kujua, katika shule za sekondari ambazo zipo karibu na vijiji, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuunganisha shule hizi za Sekondari kuziweka katika huu mradi ili wanafunzi waweze kufaidika na mradi huu katika vifaa ambavyo vinatakiwa kutumia umeme pamoja na nyumba za Walimu?

Pili, nilipenda pia kujua, tulikuwa tumepitisha Bajeti miaka miwili mfululizo na baadhi ya Vijiji mbalimbali katika Mkoa wa Mara kwenye Wilaya zote vilikuwa vimewekwa kwenye mpango. Sasa nilikuwa napenda tu kujiridhisha vile vijiji ambavyo vilishindwa kutekelezwa katika mwaka wa kwanza wa fedha 2011/2012: Je, katika Bajeti tuliyopitisha vyote vitapatiwa umeme?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, siyo tu sekondari, lakini nichukue nafasi hii kuwaomba sana wakandarasi, kuwaagiza kwamba pale ambapo shule au sehemu za huduma za kijamii zikiwemo Hospitali na shughuli mbalimbali za kijamii zinafanyika, ni maeneo lengwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

katika kuwekewa umeme. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaagiza kwamba labda itokee kwamba umbali huo ni mkubwa sana na unahitaji umbali wa peke yake. Lakini kwa umbali wa kawaida na Sekondari nyingi nchini zilivyowekwa, na jamiii walipokuwa wanapanga, sidhani kama ipo kwenye umbali mkubwa. Kwa hiyo, Shule zote za Sekondari, Zahanati na sehemu zote za kijamii lazima zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, la pili, vijiji vya Mara vilivyokuwepo kwenye Bajeti kama tulivyovitangaza, vimebakia vile vile na vipo kwenye utaratibu wa utekelezaji wa mradi huu.

SPIKA: Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la umeme kukosekana kwenye Kituo cha Afya kilichoulizwa na mwuliza swali, tatizo hilo linafanana na Kata ya Kifanya ambayo imejenga Kituo cha Afya: Je, Serikali itakuwa tayari kutoa umeme katika vijiji vyote vya Kata ya Kifanya na tukizingatia kwamba sasa kinajengwa Kituo cha Afya?

SPIKA: Mh! Umeshindwa kusema ndiko anakotoka Spika. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kijiji cha Kifanya ni miongoni mwa vijiji vilivyopo kwenye mpango huu, Kituo cha Afya kitapelekewa umeme. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata. Mheshimiwa Eng. Ramo Makani.

Na.96

Mji wa Tunduru Kupatiwa Umeme

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI aliuliza:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. R. M. MAKANI]

Mji wa Tunduru hauna umeme wa kuaminika na kutosha kukidhi haja na kasi ya maendeleo yaliyopo:-

Je, Serikali ina mipango gani ya muda mfupi, wa kati na mrefu wa kuipatia umeme Wilaya ya Tunduru iliyoundwa tangu mwaka 1905?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mpango wa muda mfupi na wa kati, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) chini ya Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili, inatekeleza mradi wa kusambaza umeme wa Wilaya ya Tunduru unaohusisha vijiji vipatavyo 20.

Kazi zitakazofanyika ni:-

- (i) Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa Kv 33 umbali wa km 247;
- (ii) Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa Kv 11 umbali wa km mbili (2);
- (iii) Ufugaji wa *transfoma* moja (1) kubwa ya Kv 33/11;
- (iv) Ufungaji wa *transfoma* ndogo 48; na
- (v) Kuwaunganisha wateja wa awali 3330.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2013 Kampuni ya Ukandarasi ya *Shandong Takai Power Engineering Co. Ltd.* imepewa kazi hiyo. Kwa sasa Kampuni hiyo inakamilisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

utaratibu ili kuanza utekelezaji wa kazi hii kwa gharama ya takribani Shilingi bilioni 1.4.

Mheshimiwa Spika, mipango ya muda mrefu ya Serikali ni:-

(i) Kuunganisha Wilaya ya Tunduru na gridi ya Taifa kutokea Songea, baada ya Mji wa Songea kuunganisha na gridi ya Taifa kupitia Mradi wa Makambako - Songea unaotarajiwa kuanza hivi karibuni; na

(ii) Kuunganisha Tunduru na umeme kutoka Mtwara utakaozalishwa kwa kutumia gesi.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa mipango ya uzalishaji umeme inakwenda sambamba na mipango ya usambazaji wa umeme, kazi za upanuzi wa njia ya umeme Wilayani Tunduru ni miongoni mwa kazi zilizojumuishwa katika utekelezaji wa Mpango kabambe wa Umeme Vijijini.

SPIKA: Mheshimiwa Eng. Ramo, maswali ya nyongeza.

MHE. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa hatua hiyo ambayo ni matumaini mapya kwa wananchi wa Tunduru. Lakini ni maswali mawili ya nyongeza madogo:-

(a) Kutokana na uzoefu ambao tayari tumeshauona, Serikali itakuwa imejipanga vipi safari hii au mara hii baada ya umeme huo kuwa sasa umefika kwenye maeneo ya karibu na wananchi ili kuwawezesha wananchi kusogeza umeme kwenye maeneo yao ya makazi na viwanda vyao vidogo vidogo kwa kuleta vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mita nyaya na nguzo mapema au kwa wakati?

[MHE. ENG. R.M. MAKANI]

(b) Kutokana na gharama zinazotokana na wananchi wanaohitaji kuunganishiwa umeme kuwa kubwa, na hasa zinazotokana na gharama za nguzo na nyaya, Serikali inafikiriaje au ina mpango gani wa kuweza kuwafanya wananchi watumie mpango wa *cost sharing* au kuchangia gharama pale ambapo wateja wawili, watatu au watano wanapokuwa wanapokuwa wainaishi maeneo jirani na wanapoweza kuunganisha umeme kwa kuchangishana gharama ili kuweza kuwapunguzia makali ya gharama?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, juu ya suala la vifaa, kwakuwa sasa miradi hii ndiyo inatekelezwa, masuala ya vifaa kwa wakati huu ni sehemu ya kandarasi. Lakini mtakumbuka kwamba tulipunguza bei ya uwekaji umeme kwa wateja hadi kufikia Sh. 177,000/= kwa sehemu isiyozidi mita 30.

Nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Mbunge awahakikishie wananchi kwamba bei hii ilipopunguzwa imetoa fursa kubwa na mpaka sasa hivi *TANESCO* wanamzigo mkubwa wa kuwasambazia umeme wananchi na hali inakuwa ngumu. Lakini kwa bei hii, kwa hakika nadhani inaridhisha na wananchi wa kawaida wanaimudu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni juu ya namna bora ya kupunguza mzigo kwa mara moja kwa wateja. Tunafikiria na tupo kwenye mchakato wa kuona namna gani tunaweza kupunguza, ama walipie kwa awamu au iwe sehemu ya uwekezaji wa *TANESCO*; bado mjadala unafanyika lakini tunadhani hivi karibuni tutatoa msimamo kwamba wananchi wanapunguziwa gharama ile wasilipe mara moja wakawa wanalipa kidogo kidogo kwa kadri tutakavyokubaliana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Jamani kama mnavyoona, muda wenyewe umekwenda na maswali yamekwisha.

Leo ninao wageni wachache, kuna wageni watatu wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge wakiongozwa na Ndugu Fatma Khalid, labda tumjue Ndugu Fatma Khalid, yupo wapi? Naona bado hajafika.

Kuna mgeni mwingine, hawa walioandika nao, wameandika vitu ambavyo havieleweki, wageni wote mliopo katika Bunge hili karibuni.

Waheshimiwa Wabunge, nawatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya Bunge maana yake ni Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge, leo Jumatano tarehe 6/11/2013, kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi saa saba kamili mchana kwenye Ukumbi wa Spika, kuna suala la muhimu la kujadili. Kwa maana hiyo matangazo yanayofuata mtajua wenyewe namna ya kufanya labda mtawaachia Makamu wenu kwa sababu yanaingiliana na kikao hiki.

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa saa saba kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi Na. 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa saba watakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake leo watakuwa na kikao saa saba na robo katika ukumbi Na. 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

kwamba leo saa tano kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Magreth Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba watakuwa na kikao katika ukumbi wa *basement*.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangwala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa saba na nusu mchana watakuwa na kikao ukumbi wa *basement*, nadhani kuna nafasi ya kutosha Kamati mbili.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hili, sijui kama linaeleweka kwa kiwango gani, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa Idd Azzan, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba wanaombwa kujisajili kushiriki Mbio za Uhuru ambazo zinatarajiwa kufanyika tarehe 8 Disemba, 2013, Dar es Salaam kwenye viwanja vya *Leaders Club*. Madhumuni ya mbio hizi, ni kuhamasisha jamii ya Kitanzania juu ya umuhimu wa kudumisha amani, umoja, upendo na mshikamano wetu tulioachiwa na Waasisi wetu. Mbio hizi zitakuwa katika aina nne yaani mbio za kilomita tatu za Viongozi, mbio za kilomita tano, kuna mbio kilomita 21 na mbio kilomita 42. Fomu za kujisajili zinapatikana mapokezi kwenye mlango mkubwa wa kuingia ukumbini. Wabunge wote wanaotaka kushiriki, wanatakiwa kujisajili katika aina hizo za mbio. Kwa hiyo, pale nje nadhani mtapata maelezo zaidi. Ni tarehe 8 Disemba na sisi tunategemea kutakuwa na Bunge hapa Dodoma kipindi hicho, mkaangalie na muweze kushirikiana na Ofisi muone ni namna gani hilo litawezekana kufanyika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, napenda kutoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Benardetha Mushashu ambaye anatuwakilisha katika Bunge la Afrika. Wakiwa katika kikao chao cha Bunge la Afrika amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Wabunge Wanawake wa Bunge la Afrika. Kwa hiyo, napenda kumpongeza na

ninadhani unapeperusha bendera ya Tanzania katika eneo hilo na vile utakavyofanya vizuri ndiyo sifa ya Tanzania itakavyokuwa nzuri. Hongera sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mnyika kila siku, hebu sema!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1), kwamba katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa Mwongozo, basi Spika atafanyakazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, Maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mapema juzi na jana ilitolewa Miongozo na Kiti chako juu ya suala la Serikali kutakiwa kutoa Kauli juu ya suala la viwango vya ufaulu. Mwongozo wa juzi uliutoa wewe na Mwongozo wa jana aliutoa Naibu Spika kwamba mapema iwezekanavyo Serikali ingetoa kauli. Nimejaribu kuangalia katika Kanuni zetu namna ambavyo Mbunge anaweza kutumia Kanuni kuwezesha hiyo mapema iwezekanavyo ikatafsiriwa kuwa ni lini kwa sababu jambo hili bado limeleta sintofahamu kubwa sana miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha nne wanaoendelea na mitihani yao bila kujua hatma yao. Naomba Mwongozo wako ili pengine Serikali iwekewe ukomo wa lini hasa itatoa Kauli.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na hilo, kwa kuwa Serikali ilishakabidhiwa ripoti ya Tume iliyoshughulikia masuala

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J.J. MNYIKA]

ya ufaulu basi kauli hiyo ya Serikali iambatane na ripoti ya Tume ambayo Waziri Mkuu alikabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuliwaambia katika Bunge hili, kwa hiyo naamini kati ya siku hizi mbili watatoa hasa lile la viwango vilivyotangazwa. Hili ombi lako lingine, nisingependa liunganishwe kwa sababu lile lilikuwa na sura yake tofauti na hili tunataka kuwaelimisha wananchi waelewe hata sisi tuelewe hicho kilichosemwa na Serikali ni kitu gani. Kwa hiyo, hii nyingine itafanyika kabla hatujaondoka. Ni katika hizi siku tatu, nne watapangiwa nafasi. Suala hilo lingine watashauriana na Serikali kuona watatoa lini. Ahsante kwa taarifa hiyo.

Kuhusu lile la kwako kuhusu mliotoa Maelezo Binafsi, kuna mengine itabidi Serikali ione namna ya kujibu, kwa sababu Maelezo Binafsi kufuatana na Kanuni zetu hayajadiliwi, lakini siyo kwamba inazuia Serikali kama jambo linaonekana ni kubwa mno kiasi kwamba wananchi wangependa kujua ikaacha kusema, kwa hiyo hiyo inafanyika pia.

Mheshimiwa Dkt. Ndugulile!

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, hoja yangu ilikuwa imejielekeza hilo hitimisho lako la pili na lilihusiana na Maelezo Binafsi hususani lile ambalo alikuwa amelisema Mheshimiwa John Mnyika jana kuhusiana na ukusanyaji wa kodi ya majengo katika Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tumekuwa tunalifuatilia hili jambo na mimi binafsi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Mkoa ambayo ilikuwa inafanya tathmini ya makusanyo ya kodi wakati Halmashauri ikifanya hivyo na baada ya *TRA* kukukusanya makusanyo. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tunataka...

SPIKA: Sasa unataka nini, unajadili au unafanyaje?

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, ndiyo namalizia.

SPIKA: Aaah, ni Mwongozo, Taarifa au ni kitu gani?

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 28(8) na 28(11).

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maombi yetu ni kwamba kodi hii ya majengo Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tunaomba irejeshwe katika Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam, hilo ndilo ombi letu. *(Makofi)*

SPIKA: Haya naomba ukae. Ukisikiliza maneno aliyosema Mheshimiwa Dkt. Ndugulile wala siyo Mwongozo ni mjadala. Mimi siwezi kuagiza kwamba kuanzia kesho wafanye hivyo. Kwa hiyo, wamesikia, watajibu kile alichosema Mheshimiwa Mnyika, ikibidi na Mheshimiwa Mnyika mwenyewe, ndiyo inaitwa *networking, networking* kwa Wabunge *is very important*. Kwa hiyo, amesema maneno yake yale yeye angetaka *results*, kwa hiyo, kazi yake nyingine ni ku-*network* asiache kwamba *it is assumed* wanaweza kujibu, a-*network* hiyo ndiyo kazi ya Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2013 *(The written Laws Mscellaneous Amendment (No. 3) Bill, 2013)*

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS
AMENDMENTS)(NO.3) ACT, 2013

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Sections

Title

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

PART II
AMENDMENT OF THE CIVIL AVIATION ACT,
(CAP. 80)

3. Construction.
4. Amendment of section 2.
5. Amendment of section 4.
- 6. Amendment of section 24.**
7. Amendment of section 26.
8. Amendment of section 27.
9. Addition of section 27A and 27B.
10. Amendment of section 32.
11. Amendment of section 34.
- 12. Addition of section 45A.**
13. Amendment of section 62.
14. Amendment of section 64.
15. Amendment of the Schedule.

PART III
AMENDMENT OF EDUCATION FUND ACT,
(CAP. 412)

16. Amendment of section 4.
17. Amendment of section 6.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

18. Amendment of section 13.
19. Amendment of the First Schedule.
20. Addition of Third Schedules.

PART IV AMENDMENT OF THE HIGHER EDUCATION STUDENT'S LOANS BOARD ACT, (CAP. 178)

21. Construction.
- 22. Amendment of section 3.**
23. Amendment of section 5.
24. Amendment of section 7.
25. Amendment of section 20.
26. Amendment of section 25.
- 27. Addition of section 32A.**

PART V AMENDMENT OF THE NATIONAL COUNCIL FOR TECHNICAL EDUCATION ACT, (CAP. 129)

28. Construction.
29. Amendment of section 2.
30. Amendment of section 6.
31. Amendment of section 16.
- 32. Amendment of Schedule.**

PART VI AMENDMENT OF THE OFFICIAL OATH ACT, (CAP.266)

33. Amendment of section 7.
34. Amendment of section 12.
35. Amendment of First Schedule.

PART VII
AMENDMENT OF THE OFFICE OF THE ATTORNEY
GENERAL (DISCHARGE OF DUTIES) ACT,
(CAP. 268)

- 36. Construction.
- 37. Amendment of section 23.

PART VIII
AMENDMENT OF THE PREVENTION OF
TERRORISM ACT, (CAP. 19)

- 38. Construction.
- 39. Amendment of section 3.
- 40. Amendment of section 6.
- 41. Amendment of section 12.
- 42. Addition of section 41A.

PART IX
AMENDMENT OF THE SOCIAL SECURITY
(REGULATORY AUTHORITY) ACT,
(CAP. 135)

- 43. Construction.
- 44. Amendment of section 7.

PART X
AMENDMENT OF THE UNIVERSITIES ACT,
(CAP. 346)

- 45. Construction.
- 46. Repeal of section 16.

PART XI
AMENDMENT OF WILDLIFE CONSERVATION ACT,
(CAP. 283)

- 47. Construction.
- 48. Amendment of section 15.
- 49. Amendment of section 17.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

50. Amendment of section 18.
51. Amendment of section 44.
52. Amendment of section 69.
53. Amendment of section 74.
54. Amendment of section 86.
55. Amendment of section 116.
56. Amendment of First Schedule.
57. Amendment of Fourth Schedule.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
....., 2013

OMBENI Y. SEFUE
Secretary to the Cabinet

A Bill

for

An Act to amend certain written laws.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

Short title 1. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.3) Act, 2013.

Amendment of certain written laws 2. The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner provided for in their respective Parts.

PART II

AMENDMENT OF THE CIVIL AVIATION ACT, (CAP. 80)

Construction Cap. 80 3. This Part shall be read as one with the Civil Aviation Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Amendment of section 2 4. The principal Act is amended in section 2 by deleting the definition of the term “air navigation services” and substituting for it the following:

“air navigation services” include air traffic management, communication, navigation, surveillance, search and rescue, metrological services for air navigation and aeronautical information services;”

Amendment of section 4 5. The principal Act is amended in section 4 -
(a) by deleting subsection (1) and substituting it the following:

“(1) The Minister may make regulations for the better carrying out of the provisions of this Act.”

(b) in subsection (2) by-

(i) deleting the word “may and substituting for it” the following phrase “,in consultation with the Authority;”;

(ii) adding immediately after the opening phrase of subsection (2) the following new paragraphs:

“(a) for regulating air navigation and air transport and regulation of economic air transport and regulation of economic air transport;

(b) giving effect to Chicago Convention, and its annex thereto, and any other civil aviation convention to which United Republic is a party;”

(iii) renaming paragraphs (a) to (u) as paragraphs (c) to (w) respectively;

(iv) deleting paragraph (v);

(v) renaming paragraphs (w) and (x) as paragraphs (x) and (y) respectively;

(vi) adding immediately after the renamed paragraph (y) the following:

"(z) regulating aviation training organization;

(aa) prohibiting or regulating the emission or causing of smoke, soot, ash, grit, dust and any other substance whatsoever which obscures or may obscure visibility in the vicinity of the aerodrome;

(bb) classifying and use of airspace, control search and reserve facilities;

(cc)for the aircraft design, construction, repair, over have maintenance, repair of facilities and related equipment;

(dd)overseeing the implementation of the safety management system; and

(ee)providing for development and implementation of the state safety program."

Amendment of section 24 **6. The principal Act is amended in section 24(2) by-**

(a) adding immediately after paragraph (c) the following:

"(d) borrowing and lending;"

(b) renaming paragraph (d) as paragraph (e).

Amendment of section 26 **7. The principal Act is amended in section 26(1) by-**

(a) adding immediately after paragraph (g) the following:

"(h) to plan, develop, regulate and promote operations of a safe, secure and efficient civil aviation system;

(i) to conduct safety, security and economic oversight of the aviation industry;

(j) to establish and implement the state safety programme;

- (k) to establish an acceptable level of safety;
- (l) to advise the Government on matters concerning civil aviation;
- (m) to coordinate search and rescue operations of aircraft;
- (n) to deal with acts of unlawful interference;
- (o) to establish, manage and operate training institutions for the industry;
- (p) to plan, develop and formulate the safe, secure and efficient management of Tanzanian airspace and;"

(b) renaming paragraph (h) as paragraph (q).

Amendment of section 27 **8.** The principal Act is amended in section 27 by deleting the words "and functions" appearing in the marginal note.

Addition of sections 27A and 27B **9.** The principal Act is amended by adding immediately after section 27 the following new sections:

"Functions and powers of the Board

27A.-(1) The Board shall generally be responsible for ensuring that the performance and management of the functions, and affairs of the Authority are carried out in an efficient, transparent and ethical manner.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), the Board shall -

- (a) set the Authority's strategic objectives, value and standards;
- (b) ensure that the necessary resources are in place for the Authority to meet in objective and review Management performance;

- (c) provide public education on the functions and obligation of the Authority;
- (d) determine and set priorities of the general performance and targets of the Authority;
- (e) ensure that measures for the development of civil aviation are in place and implementable;
- (f) consider and advise the Minister on the development and maintenance of civil aviation policy framework and such other matters affecting civil aviation as it considers desirable in the interest of civil aviation in the United Republic;
- (g) perform such other functions as the Minister may direct; and
- (h) approve the budget of the Authority.

(3) The Board may, in the discharge of its functions under subsection (1) and (2) shall have power-

(a) direct the Director General to furnish it with any information, reports or other documents which the Board may require;

(b) give lawful instructions and orders in writing to the Director General in connection with the Management and performance of the Authority.

(c) approve any organizational structures submitted by the Director; and

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunapendekeza kufuta na kukiandika upya kifungu cha 4(3) ili kuweka masharti kuhusu matumizi ya fedha zitakazowekwa kwenye Mfuko wa Elimu. Inapendekezwa kuwa fedha hizo zitumike kuboresha upatikanaji, usawa na ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, pili, kurekebisha aya ya (f) kwenye Muswada ya kifungu cha 6 ili kuiongezea Mamlaka ya Elimu jukumu la kuanzisha na kufanya mapitio ya mara kwa mara ya kanuni za utengaji na ugawaji wa rasilimali fedha za Mamlaka ya Elimu katika ngazi tofauti za elimu. Inapendekezwa kuwa angalau asilimia 50 ya rasilimali fedha itakayotolewa itumike kugharamia miradi ya maendeleo ya elimu ya juu.

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Mheshimiwa Spika, aidha, inapendekezwa kuwa aya mpya ya (i) iongezwe kwenye kifungu cha 6 ili Mamlaka ya Elimu iwe na uwezo wa kutumia fedha zinazowekwa kwenye Mfuko wa Elimu kwa ajili ya kugharamia majukumu ya kisheria ya Mamlaka ya Elimu, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Tume ya Vyuo Vikuu ya Tanzania, na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi baada ya kushauriana na taasisi hizo kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, tatu, tunapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) cha Sheria kinachompa Waziri mwenye dhamana ya elimu mamlaka ya kurekebisha muundo wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu ili kuondoa mamlaka ya Waziri kubadilisha Muundo wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, samahani nitarudia sehemu hii. Tatu, tunapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) cha Sheria kinachompa Waziri mwenye dhamana ya elimu mamlaka ya kurekebisha muundo wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu ili kuondoa mamlaka ya Waziri kubadilisha Muundo wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yanazingatia kuwa kifungu kidogo cha (4) kama kilivyo sasa, hakitoi mamlaka kwa Waziri kufanya marekebisho kuhusu Muundo wa Bodi ulioainishwa katika aya ya (2) ya Jedwali la Kwanza. Aidha, kutokana na mapendekezo yaliyo kwenye Ibara ya 23 ambayo yanakusudia kurekebisha Jedwali la Kwanza kwa kuainisha taasisi na maeneo ambayo Waziri atateua wajumbe wa Bodi, hakuna sababu ya Waziri kuwa na mamlaka ya kubadilisha muundo wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, nne, kufanya marekebisho katika kifungu cha 13 kinachohusiana na vyanzo vya mapato ya Mamlaka ya Elimu ili kuhahakisha kuwa Mfuko wa Elimu unakuwa na fedha za kutosha. Inapendekezwa kuwa moja ya vyanzo iwe fedha isiyopungua asilimia mbili (2%) ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya Serikali, ukiondoa malipo ya Deni la Taifa kama fedha ya nyongeza kwa ajili ya kuboresha elimu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

katika ngazi zote. Sheria ilivyo sasa inaweka masharti kuwa fedha hiyo isizidi asilimia mbili. Vyanzo vingine vinavyopendekezwa ni pamoja na Tozo ya Ujuzi wa Maendeleo (*Skills Development Levy*) chini ya Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na fedha zitazotolewa na Bunge na fedha zitakazotokana na mikopo au miradi. Mapendekezo haya yatawezesha mapato ya Mfuko wa Elimu kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, tano, tunapendekeza kurekebisha Jedwali la Kwanza kwa kuainisha Idara na Taasisi ambazo Waziri atazingatia wakati wa kuteua wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu na tunapendekeza kuwa Bodi iundwe na mjumbe kutoka katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuo, Divisheni ya Uratibu wa Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Hazina, Wizara ya Elimu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Taasisi za Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sekta Binafsi na Wizara ya Elimu. Sheria ilivyo sasa inataja tu kuwa Bodi ya Mamlaka ya Elimu itaundwa na wajumbe watano bila kutaja Taasisi au Idara ambazo Waziri atawatoa Wajumbe hao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, sehemu hii ya nne inapendekeza kuongeza Jedwali jipya la Tatu kwenye Sheria ya Mfuko wa Elimu ili kuainisha viwango vya asilimia ya mgawo wa fedha za Mfuko kwa taasisi zinazohusika. Taasisi hizo ni pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Tume ya Vyuo Vikuu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yanakwenda sambamba na mapendekezo yaliyoainishwa kwenye Ibara ya 20(d) ya Muswada. Sheria ilivyo sasa haiainishi kanuni na viwango vinavyopaswa kuzingatiwa katika kugawa fedha za Mfuko wa Elimu kwa taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura ya 230, Toleo la 2002. Ibara ya 26 ya Muswada inapendekeza kuwa kifungu cha 34 kirekebishwe ili kuongeza adhabu kwa mtu atakayetenda kosa chini ya Sheria hiyo

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

ikiwemo kutoa filamu au mchezo wa kuigiza wenye lugha ya uchochezi. Kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, adhabu inayopendekezwa kutokana na ushauri wa Kamati ambayo Serikali imeuafiki ni faini isiyozidi shilingi milioni tano badala ya shilingi elfu tano iliyoko kwenye Sheria ya sasa au kifungo kisichozidi miaka miwili badala ya miezi kumi na miwili iliyoko kwenye Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Ibara ya 29 ya Muswada inapendekeza kuwa kifungu cha 5 kinachohusiana na muundo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kifutwe na kuandikwa upya na mapendekezo haya yanakusudia kuongeza Uwakilishi wa Taasisi zifuatazo kwenye Bodi hiyo ambazo kwa sasa hazina uwakilishi:-

- (i) Tume ya Vyuho Vikuu Tanzania;
- (ii) Baraza la Taifa la Udahili wa Elimu ya Ufundi; na
- (iii) Mamlaka ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, Wajumbe wengine wa Bodi ni Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu na wawakilishi wa Taasisi au Idara zifuatazo:-

- (i) Hazina;
- (ii) Waziri mwenye dhamana ya fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;
- (iii) Wanafunzi wa elimu ya juu;
- (iv) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (v) Chama cha Waajiri Tanzania;
- (vi) Taasisi za fedha; na
- (vii) Vyuho Vikuu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanalenga kuongeza ufanisi na utendaji wa kazi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 30 ya Muswada kifungu cha 7 kinapendekeza kurekebishwa ili kuiongezea Bodi ya Mikopo mamlaka ya kutoa misaada na ufadhili kwa masharti maalum na kuishauri Wizara yenye dhamana ya Elimu ya Juu na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kuhusu utekelezaji wa masharti ya Sheria hiyo. Majukumu hayo kwa sasa hayapo kwenye Sheria. Hivyo, mapendekezo haya ya kurekebisha kifungu cha 7 yanalenga kuongeza ufanisi wa utendaji wa kazi ya Bodi na utekelezaji wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Ibara ya 31 ya Muswada yanahusu kifungu cha 21 cha (1)(b) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambapo tunapendekeza kuwa kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya ili kuweka masharti ya kumtaka Mwajiri wa mtu aliyenufaika na mkopo wa Elimu ya Juu kukata kiasi ambacho Bodi itaelekeza kutoka katika mshahara ghafi wa mtu huyo na mapendekezo hayo yanalenga kuhakikisha kwamba mikopo iliyotolewa inalipwa na inalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32 ya Muswada ina mapendekezo mengine ya kufuta na kuandika upya kifungu cha 25 kinachoainisha vyanzo vya mapato ya Bodi ya Mikopo kwa lengo la kupanua wigo wa vyanzo hivyo ili kuongeza mapato ya Bodi. Vyanzo vinavyopendekezwa ni: fedha za bajeti zitakazotolewa na Bunge, fedha zitakazopatikana kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mfuko wa Elimu, majeresho ya mikopo pamoja na riba, mikopo itakayoombwa na Bodi na fedha zozote zitakazopatikana kutoka katika vyanzo vingine, ikiwemo ulipwaji wa ada, misaada na zawadi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 33 ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sehemu hii ya kufuta na kuandika upya kifungu cha 32A kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho kwa madhumuni ya kuweka masharti yatakayoitaka kila Taasisi au Kampuni kutoa Taarifa za Wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya Juu ambapo Bodi ya Mikopo itakapowataka kufanya hivyo. Mapendekezo haya

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

yanalenga kuiwezesha Bodi kupata Taarifa sahihi za wanafunzi wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya Juu zitakazosaidia kuwafuatilia na hatimaye kurejesha mikopo husika ili marejesho hayo yatumike kuwakopesha wanafunzi wengine wa elimu ya juu wenye mahitaji hayo. Pengine nichukue nafasi hii pia kuwaomba watu wenyewe waliokopa warudishe fedha hizo wanapopata uwezo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Ibara ya 35 ya Muswada inapendekeza kuwa tafsiri ya sasa ya neno “Waziri” ifutwe na iandikwe upya kwa maana kwamba Waziri awe ni yule Waziri mwenye dhamana ya elimu ya ufundi badala ya Waziri mwenye dhamana ya sayansi na teknolojia. Mapendekezo haya yanazingatia muundo wa sasa wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yaliyomo kwenye Ibara ya 36 ya Muswada yanayopendekeza kufuta kifungu cha 6(3) yameondolewa kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho kufuatia ushauri wa Kamati ya Bunge. Hivyo, masharti ya sasa kwamba kila Amri inayotolewa na Waziri kwa lengo la kuifanya taasisi yoyote kuwa taasisi inayojitegemea, sharti kwanza iidhinishwe kwa Azimio la Bunge kabla ya kuanza kutumika na masharti hayo yataendelea. Muswada ulikuwa umependekeza kuwa Amri hiyo iwasilishwe Bungeni kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 38 cha Sheria ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinachoweka masharti kuwa Amri zote za aina hiyo ziwasilishwe Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanahusu kifungu cha 16 kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 37 ya Muswada. Tunapendekezwa kwamba kifungu hicho kirekebishwe kwa lengo la kuongeza vyanzo vipya vya mapato ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Vyanzo vinavyopendekezwa kuongezwa ni pamoja na fedha zitakazotolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mfuko wa Elimu, fedha itakayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na tozo mbalimbali zinazoweza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

kuainishwa na Baraza kwa ajili ya huduma zinazotolewa na Baraza hilo. Mapendekezo haya yanakusudia kuongeza mapato ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Magazeti. Marekebisho haya yanalenga kutekeleza Azimio la Bunge katika Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha 21. Bunge liliazimia, pamoja na mambo mengine, kwamba Serikali ipitie Sheria zilizopo ili kuona kama zinatoshesheza kuzuia lugha au kauli za uchochezi (*hate speeches*). Serikali imepitia Sheria ya Magazeti na kuona kuwa inazuia uchapishaji wa habari inayoweza kusababisha uchochezi au uvunjifu wa amani ama kama inavyoelezwa katika vifungu vya 36 na 37.

Mheshimiwa Spika, aidha, adhabu ya faini kwa makosa ya kuchapisha habari ya uchochezi au habari inayoweza kusababisha uvunjifu wa amani chini ya vifungu hivyo ni shilingi laki moja na nusu. Kwa kuzingatia kuwa adhabu hiyo ni ndogo kulinganisha na madhara ya kosa linalohusika katika jamii, Muswada unapendekeza katika Ibara ya 40 na 41 kuwa vifungu hivyo virekebishwe kwa lengo la kuongeza adhabu ya faini kwa makosa hayo ili adhabu hiyo isizidi shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Viapo. Kifungu cha 7 kinachohusu kiapo cha Majaji kinarekebishwa ili kuweka masharti kwamba Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Jaji wa Mahakama ya Rufaa au Jaji wa Mahakama Kuu, watatakiwa kula kiapo cha Kimahakama (*Judicial Oath*) mbele ya Rais kama inavyopendekezwa kwenye Ibara ya 43 ya Muswada. Kiapo hicho cha Kimahakama kitakuwa ni nyongeza ya kiapo cha utii. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kwamba kiapo cha Kimahakama kinamhusu Jaji wa Mahakama Kuu tu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine katika Sheria ya Viapo yanahusu kifungu cha 12. Inapendekezwa katika Ibara ya 44 kuwa kifungu hicho kirekebishwe ili kiapo cha kutunza siri ya Katibu wa Baraza la Mawaziri na Maafisa

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

wengine wa Baraza la Mawaziri kitolewe mbele ya Rais. Aidha, inapendekezwa kuwa iwapo Rais hayupo, kiapo hicho kitolewe mbele ya Makamu wa Rais na kama Makamu wa Rais hayupo basi kiapo hicho kitolewe mbele ya Waziri Mkuu. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa iwapo Rais hayupo, kiapo hicho kitolewe mbele ya Waziri anayeongoza kikao cha Baraza la Mawaziri. Madhumuni ya mapendekezo haya yanatokana na utaratibu wa kawaida wa uendeshaji wa vikao vya Baraza la Mawaziri ambapo vikao hivyo huongozwa na Rais na iwapo Rais hayupo, Makamu wa Rais huongoza vikao hivyo na pale ambapo wote wawili hawapo Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye anaongoza vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Jedwali la Kwanza la Sheria ya Viapo linapendekeza kurekebisha kwa kufuta maneno "*Judicial Oath*" na kuweka badala yake maneno "*Judge's/ Judicial Officer's Oath*" na vilevile, kufuta maneno "Kiapo cha Hakimu" na kuweka badala yake maneno "Kiapo cha Jaji/Afisa wa Mahakama". Lengo la mapendekezo haya ni kuweka masharti ya kiapo kwa maafisa wengine wa Mahakama ambao wametajwa katika Sheria ya Utumishi wa Mahakama wakiwemo Wasajili na Wasaidizi wa Majaji. Hii ni kwa sababu aina ya kazi wanazofanya zinahitaji usiri na hivyo, ulazima wa kiapo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16), T.L. 2002. Kama ilivyo kwa mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Magazeti, marekebisho katika sehemu hii ya kumi yanalenga kutekeleza Azimio la Bunge lililoitaka Serikali kupitia Sheria zilizopo ili kuona kama zinafaa kuzuia kauli au lugha za uchochezi. Kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho, mapendekezo ya kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 55 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu yameondolewa. Hii ni kwa kuzingatia kuwa masharti ya kifungu hicho yanashughulikiwa chini ya kifungu cha 31 na 32 cha Sheria ya Magazeti ambayo inaelezea kosa na adhabu ya kosa la uchochezi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada unapendekeza katika Ibara ya 48 kufanya marekebisho katika kifungu cha 63B ili adhabu ya kosa la kutoa matamshi katika mkusanyiko wa watu, yanayoweza kusababisha vurugu au kuchochea uadui baina ya makundi mbalimbali au jamii mbalimbali za watu iwe faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo kisichopungua mwaka mmoja. Adhabu ya faini ya kosa hilo kwa sasa ni shilingi elfu moja ambayo kwa kweli ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza pia kuongeza kifungu kipya cha 63C ambacho kinabainisha kosa la jinai la kutoa lugha au kauli ya uchochezi yaani, *“hate speech”*. Adhabu ya kosa hilo inapendekezwa kuwa faini ya shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine katika Sheria ya Kanuni za Adhabu yanahusu kifungu cha 89(1) kinachohusu kosa la kutumia lugha ya matusi, kupigana na vitisho vya kufanya vurugu. Inapendekezwa katika Ibara ya 50 ya Muswada kuwa adhabu ya kosa hilo iwe kifungu cha mwaka mmoja gerezani badala ya miezi sita inayotajwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza katika Ibara ya 51 kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 126 ili adhabu ya kosa la kusababisha udhia au usumbufu katika mikusanyiko ya ibada, iwe faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichozidi miaka miwili gerezani. Sheria ilivyo sasa haiainishi adhabu mahsusi kwa mtu anayetenda kosa hilo. Kutokuwepo kwa adhabu mahsusi ya kosa hilo kunazifanya Mahakama kutumia adhabu ya jumla chini ya kifungu cha 35 ambayo ni kifungu cha miaka miwili gerezani.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mwisho katika Sheria ya Kanuni ya Adhabu yanapendekezwa kufanywa kwenye kifungu cha 129, kinachohusu kosa la kutoa matamshi yenye lengo la kukashifu dini ya mtu mwingine. Kosa hilo linahusisha matamshi ya maneno ya kashfa, sauti za kashfa

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

au kutoa ishara kwa madhumuni ya kuudhi dini ya mtu mwingine. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha mwaka mmoja gerezani. Kwa mujibu wa Kanuni za Tafsiri za Sheria, Mahakama inaweza kutoa adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja. Hivyo, ili kuendelea kuzuia vitendo vya aina yoyote vinavyokusudia kuudhi na kukashifu dini ya mtu mwingine, Muswada unapendekeza katika Ibara ya 32 kuwa adhabu mbadala ya faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua mwaka mmoja gerezani kwa mtu anayetwa hatiani kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Ugaidi (Sura ya 19) T.L. 2002. Ibara ya 54 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria hiyo ili kuongeza tafsiri ya maneno “Kamishna wa Kitengo cha Udhubiti wa Fedha Haramu” na “Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu”. Maneno hayo yametumika kwenye Sheria hiyo lakini hayajatafsiriwa. Inapendekezwa sasa kuwa tafsiri ya maneno hayo iwe kama ilivyotolewa katika Sheria ya Udhubiti wa Fedha Haramu (Sura ya 423).

Mheshimiwa Spika, aidha, tunapendekeza kuwa kifungu kipya cha 41A kiongezwe kwenye Sheria hiyo ili kuweka masharti ya kuitaka Taasisi ya Fedha au mtu yeyote kukitaarifu Kitengo cha Udhubiti wa Fedha Haramu (FIU) kuhusu suala lolote ambalo taasisi au mtu huyo ataona kuwa linahusika kwa namna moja au nyingine na ufadhili wa ugaidi au linakusudia kufadhili shughuli yoyote ambayo inasimamiwa na au kwa niaba ya kundi la kigaidi. Aidha, kifungu hiki kinapendekeza pia adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano, au kifungo kisichopungua miaka miwili gerezani, au vyote, faini na kifungo, kwa mtu au taasisi ambayo inakiuka masharti ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura 257. Muswada unapendekeza katika Ibara ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

59 kuwa kifungu cha 3 kirekebishwe ili kuweka masharti kwamba Shirika la Umma lililosajiliwa chini ya Sheria hiyo litakuwa na wajibu wa kumtaarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu kesi inayotarajiwa kufunguliwa au itakayofunguliwa na shirika hilo au dhidi ya shirika husika na kwamba baada ya kupokea taarifa hiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa na haki ya kuingilia kati shauri hilo. Aidha, inapendekezwa kuwa iwapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatumia haki yake na kuingilia kati shauri husika, masharti ya Sheria ya Mashauri dhidi ya Serikali, Sura ya 5 (*The Government Proceedings Act*) yatatumika kana kwamba shauri husika limefunguliwa na, au dhidi ya Serikali. Mapendekezo hayo yanalenga kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutetea maslahi ya Serikali katika shirika husika la umma kuanzia hatua za awali za kesi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhubiti wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii, (Sura 135), T.L. 2002. Kifungu cha 7(1)(e) kinapendekezwa kurekebisha ili kukiwezesha chama cha waajiri chenye uwakilishi mkubwa kuwakilishwa na wajumbe wawili kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhubiti wa Mifuko ya Jamii. Lengo la mapendekezo hayo ni kuweka usawa wa uwakilishi kati ya waajiriwa na waajiri kwenye Bodi hiyo ambapo kwa sasa wafanyakazi wanawakilishwa na wajumbe wawili wakati waajiri wanawakilishwa na mjumbe mmoja.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne kama ilivyorekebisha kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Vyuo Vikuu, (Sura 346). Inapendekezwa kuwa kifungu cha 16 kifutwe na kiandikwe upya ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato vya Tume ya Vyuo Vikuu. Vyanzo vinavyopendekezwa ni; fedha zitakazotengwa na Bunge, misaada, mikopo, zawadi au ufadhili kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, fedha itakayotokana na uwekezaji, miradi au harambee zitakazoendeshwa na Tume, fedha itakayopokelewa kutoka kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, fedha itakayotolewa chini ya masharti ya

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Sheria ya Mfuko wa Elimu na tozo zitokanazo na huduma mbalimbali zitolewazo na Tume kwa wateja wake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi, (Sura ya 82), T.L. 2002; kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) kwenye kifungu cha 19 cha Sheria hiyo kama kilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na.4/2013 kinachompa Waziri mwenye dhamana ya mafunzo na ufundi stadi mamlaka ya kutoa msamaha wa ushuru kwa mwajiri au kundi la waajiri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda, kupitia kwako kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kuujadili Muswada huu na kuupitisha katika hatua zote mbili yaani kusomwa kwa Mara ya Pili na Kusomwa kwa Mara ya Tatu. Nina imani kwamba Bunge lako litaridhia marekebisho tunayopendekeza ili sheria zetu ziweze kukaa vizuri na kwamba litakubali marekebisho haya yawe sehemu ya Sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na Hoja hiyo au Mwakilishi wake. *(Makofi)*

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dokta Pindi Hazara Chana pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *[The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.3) Act of 2013.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *[The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.3) Act Of 2013.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam mnamo tarehe 29 Septemba, 2013 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika. Aidha, baada ya hapo, Kamati ilikutana nao katika vikao mbalimbali vilivyofanyika kwa nyakati tofauti katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge ulioanza tarehe 29 Oktoba, 2013 katika Ofisi ya Bunge, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yake, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *[The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.3) Act Of 2013,* unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria kumi na tano kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo; kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano katika Sheria hizo; kufuta baadhi ya vifungu ambavyo ama vinaleta mkanganyiko katika utekelezaji wa Sheria husika au vimepitwa na wakati na kuweka masharti mapya kwa ajili ya utekelezaji madhubuti wa Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebisha ni kama zifuatazo:-

(a) Sheria ya Usafiri wa Anga *(The Civil Aviation Act)*, Sura ya 80;

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

(b) Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Majimbo (*The Constituencies Development Catalyst Fund Act*), Sura ya 96;

(c) Sheria ya Mfuko wa Elimu (*The Education Fund Act*), Sura ya 412;

(d) Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (*The Films and Stage Plays Act*), Sura ya 230;

(e) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (*The Higher Education Students' Loan Act*), Sura ya 178;

(f) Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*The National Council for Technical Education Act*), Sura ya 129;

(g) Sheria ya Magazeti (*The Newspapers Act*), Sura ya 229;

(h) Sheria ya Viapo (*The Official Oaths Act*), Sura ya 266;

(i) Sheria ya Kanuni za Adhabu (*The Penal Code*), Sura ya 16;

(j) Sheria ya Kuzuia Ugaidi (*The Prevention of Terrorism Act*), Sura ya 19;

(k) Sheria ya Mashirika ya Umma (*The Public Corporation Act*), Sura ya 257;

(l) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi Jamii [*The Social Security (Regulatory Authority) Act*], Sura ya 135;

(m) Sheria ya Vyuo Vikuu (*The Universities Act*), Sura ya 346;

(n) Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi (*The Vocational Education and Training Act*), Sura ya 82; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

(o) Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori (*The Wildlife Conservation Act*), Sura ya 283.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilitoa mwaliko na pia kutangaza katika vyombo vya habari ili kuwaalika wadau mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 ili kupata maoni yao kuhusu mapendekezo ya Muswada katika vifungu mbalimbali vinavyofanyiwa marekebisho katika sheria nilizozitaja awali kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, baadhi ya watendaji wa Serikali hususan taasisi ambazo marekebisho ya sheria hizo yanawagusa moja kwa moja nao walihudhuria vikao vya Kamati ili kutoa ufafanuzi katika maeneo yanayowahusu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao kwa nyakati tofauti, waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati wakiwemo Chama cha Wanasheria Tanzania (*TLS*) na Chama cha Wanasheria Wanawake (*TAWLA*) waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao. Aidha, Kamati ilipokea na kufanyia kazi maoni yaliyowasilishwa kwa maandishi kutoka kwa Baraza la Habari la Tanzania (*MCT*), *National Organization for Legal Assistance* (*NOLA*), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*) na *Trade Union Congress of Tanzania*. Michango na maelezo ya ufafanuzi waliyoyatoa mbele ya Kamati vimesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya uchambuzi, Kamati ilipitia sehemu zote na kutoa maoni na ushauri katika kila sehemu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada kuhusu masuala ya utangulizi wa sheria inayopendekezwa. Kamati imepitia na kuchambua kwa kina Sehemu hii yenye jumla ya Ibara mbili na kuafiki mapendekezo hayo.

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada – Marekebisho katika Sheria ya Usafiri wa Anga (*The Civil Aviation Act*), Sura ya 80. Kamati imepitia na kuchambua kwa kina mapendekezo ya Serikali katika Sehemu ya Pili ya Muswada. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 2 cha Sheria mama ili kuweza kutoa tafsiri sahihi ya maneno “*air navigation services*” kwani hapo awali tafsiri iliyokuwepo haikuwa ikikidhi mahitaji halisi ya huduma za anga kwa mahitaji ya sasa kutokama na kuridhia Mkataba wa *Chicago Convention*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 4 cha Sheria mama ambacho kinahusiana na mamlaka ya Waziri mwenye dhamana kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Serikali inapendekeza kuwekwa kwa masharti kwamba Waziri mwenye dhamana atekeleze mamlaka hayo kwa kushauriana na Mamlaka ya Anga.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono na inakubaliana na pendekezo kwamba Waziri mwenye dhamana atunge Kanuni kwa kushauriana na Mamlaka ya Anga, kwani kwa kufanya hivyo kutawezesha kutungwa kwa Kanuni bora na zinazotekelezeka. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wataalam wa Mamlaka ya Anga watakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumshauri Waziri kuhusu mazingira halisi ya mamlaka na Kanuni zinazofaa kufanikisha utendaji bora wa mamlaka.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati inaunga mkono marekebisho ya kifungu hiki kwa kuwa yanalenga kukidhi viwango vya Kimataifa vilivyowekwa katika Mkataba wa kimataifa wa Chicago ambao Tanzania ni mwanachama. Hii itawezesha kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Anga inakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kusimamia na kudhibiti usalama wa anga katika nchi yetu na kuendana na nchi nyingine

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

duniani zinavyofanya katika kusimamia masuala ya usalama wa anga.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 ya Muswada katika mapendekezo yake ya awali ilikuwa inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 24 cha Sheria mama kwa kuiruhusu mamlaka ya anga kuweza kukopa na kukopesha. Baada ya mashauriano na Kamati, Kamati ilihoji iweje mamlaka ya anga kupewa uwezo wa kukopesha. Hatimaye Mwanasheria Mkuu amekubali ushauri wa Kamati kwa kuleta Jedwali la Marekebisho la kufuta pendekezo la awali la kutaka kuiwezesha mamlaka kukopesha. Marekebisho haya yamezingatia ukweli kwamba Mamlaka ya Anga ni chombo cha kutoa huduma hivyo si vyema kuiingiza katika mfumo wa kibiashara wa kuanza kukopesha.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Mamlaka ya Anga haina fedha za kutosha za kumudu gharama za uendeshaji, wazo la kuiruhusu Mamlaka ya Anga kukopa ni wazo zuri na Kamati inalunga mkono hivyo inakubaliana na marekebisho kama yalivyo katika Jedwali la Marekebisho linalohusu Ibara ya 6, ambalo linafuta neno kukopesha.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 27 cha Sheria mama kwa kuongeza kifungu kipya cha 27A ambacho kinafafanua mamlaka ya Bodi ya Mamlaka ya Anga. Serikali inapendekeza katika aya ndogo ya (h) kuwa bodi ifanye kazi nyingine yoyote ambayo Waziri ataitaka ifanye ("*h*) *perform such other function as the Minister may direct*"). Kamati inapendekeza kuwa aya hii ndogo ya (h) iboreshwe kwa kuweka masharti kwamba Bodi ifanye kazi nyingine yoyote inayohusiana na masuala ya anga na sio kuiacha kama ilivyo sasa. Hii itawezesha Waziri kutoa maelekezo kwa Bodi kufanya kazi zilizoko ndani ya misingi ya uanzishwaji wake na kuondoa uwezekano wa kifungu hiki kutumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 10 ya Mswada, Serikali ilipendekeza kufuta kifungu cha 32(2). Baada ya mashauriano ya kina na Kamati, Serikali imekubali kutofuta

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

kifungu hicho kutokana na ukweli kwamba uwepo wa kifungu hiki unasaidia kuondoa mgongano wa maslahi (*conflict of interest*) kwa Wajumbe wa Bodi au waliowahi kuwa Wajumbe wa Bodi kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu toka wameacha kuwa Wajumbe wa Bodi hiyo. Kufutwa kwa kifungu hiki kungemaanisha kuruhusu Mjumbe wa Bodi au aliyewahi kuwa Mjumbe wa Bodi kuingia kwenye mgongano wa kimaslahi na Bodi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mjumbe huyo angeweza kutumia taarifa alizowahi kuzipata wakati akiwa Mjumbe wa Bodi ili kujinufaisha yeye binafsi au kumpa taarifa hizo mtu mwingine au taasisi nyingine ili itumie taarifa hizo kujinufaisha.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12 ya Muswada hapo awali ilikuwa inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 45 cha Sheria mama kifungu kipya cha 45A. Kifungu hiki kililenga kuwapa kinga ya kutoshtakiwa Wajumbe wa Bodi na watumishi wengine wa Bodi ya Anga (*TCAA*) wao binafsi kwa jambo ambalo watalitenda kwa nia njema. Kamati ilimshauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuondoa pendekezo hilo kwani kuwapa kinga Wajumbe wa Bodi na watumishi wengine wa Mamlaka kunaweza kukapelekea kutumika vibaya kwa madaraka. Aidha, Kamati ilijiridhisha kuwa endapo mtumishi atakuwa ametenda jambo kwa nia njema, zipo taratibu za Sheria na Maamuzi ya Mahakama ambayo hutoa tafsiri hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada – Marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Majimbo (*The Constituencies Development Catalyst Fund Act*), Sura ya 96. Maoni na ushahi wa Kamati katika sehemu hii yamezingatia mambo ya msingi. Kwa ujumla Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 9 inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (*The Constituencies Development Catalyst Fund Act*) (*Cap 96*) kwa kufuta na kuweka kifungu kipya cha 9(1) na (2) ambavyo kwa ujumla wake vinatamka kuwa fedha zote za Mfuko ziwe zinakaguliwa na Mdhibiti na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria hii. Kifungu kidogo cha (2) kinaweka masharti kwamba fedha za Mfuko zinazopelekwa kwa lengo la kuchochea maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Zanzibar ziwe zinakaguliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kushirikiana na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na pendekezo hili kwani ni vyema pesa zinazotolewa kwa lengo la Kuchochea maendeleo ya Jimbo zikawa zinakaguliwa ili kuona kama zinafanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, kitendo cha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali Kushirikiana na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar katika ukaguzi wa fedha zinazotolewa kwa lengo la kuchochea maendeleo ya Jimbo upande wa Zanzibar kutarahisisha utekelezaji wa kazi hii ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada – Marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Elimu (*The Education Fund Act*), Sura ya 412. Ibara ya 20 ya Muswada inakusudia kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria ya Mfuko wa Elimu (*The Education Fund Act*) (CAP 412). Ibara ya 20 ya Muswada inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 6 cha Sheria mama kwa kufuta aya ya (a) na kukiandika upya ili kisomeke *“to provide funds to supliment the provision of education at all leves”* na pia kwa kufuta aya ya (f) na badala yake kuweka kama ifuatavyo:-

(f) “to develop and make periodic review of the formula for allocation and disbursement of the financial resources of the Authority to different educational levels except that, atleast fifty percent of the financial resources shall be provided to finance higher education for development projects”

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya marekebisho ya Serikali yaliyotajwa hapo juu, Kamati ina

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

maoni kwamba ingawa pendekezo la kifungu cha 6(a) cha Sheria mama kinatamka kuwa fedha za Mfuko zitatumika kutoa fedha za ziada ili kutoa elimu katika ngazi zote za elimu (*at all levels*) lakini Jedwali la Tatu la Sheria limeeleza kuwa fedha hizo zitagawanywa kwa asilimia 64 ya fedha za Mfuko kwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, asilimia 30 kwenda Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), asilimia 3 kwenda kusaidia Elimu ya Ufundi na asilimia 3 iliyobaki kwenda Tume ya Vyuo Vikuu. Aidha, Kamati inaona kwamba japokuwa maneno *“to suplliment education at all levels”* yametumika lakini elimu ya msingi na elimu ya sekondari zimeachwa bila kutengewa asilimia yoyote katika fedha za Mfuko wa Elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba elimu ya msingi na sekondari ndizo zenye mahitaji makubwa zaidi kuliko hata elimu ya juu, mapendekezo haya, kwa maoni ya Kamati hayafai kwani yanalenga kuendelea kutoa fedha katika ngazi za elimu ambazo zina unafuu ukilinganisha na elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ngazi zingine za elimu zimezingatiwa isipokuwa elimu ya msingi na sekondari, lakini bado Kamati inaona kuendelea kutenga asilimia si chini ya hamsini au zaidi kwa ajili ya elimu ya juu ni kuipendelea elimu ya juu huku tukiacha ngazi nyingine za elimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano haya, Mwanasheria Mkuu alikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuomba akawasiliane na mamlaka husika ili kuangalia namna bora ya kuweka Kanuni ya mgawanyo wa Fedha za Mfuko wa Elimu ili ziweze kunufaisha ngazi zote za elimu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (*The Films and Stage Plays Act*), Sura ya 230. Katika Ibara ya 26 inakusudia kurekebisha Kifungu cha 34(1) cha Sheria mama kwa kuongeza adhabu kutoka faini ya shilingi elfu tano hadi shilingi milioni tatu na kuongeza kifungo kutoka kifungu cha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

mwaka mmoja hadi kifungo cha miaka miwili kwa mtu anayepatikana na hatia kwa kutumia lugha za matusi na uchochezi katika filamu na michezo za kuigiza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono pendekezo hili kwani vitendo vya matumizi ya lugha za matusi na ya uchochezi vina athari kubwa katika jamii na adhabu iliyokuwepo awali imepitwa na wakati hivyo kuhitaji marekebisho ili kuendana na wakati pamoja na kupiga vita matumizi ya lugha za matusi na uchochezi katika filamu na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (*The Higher Education Students' Loan Act*), Sura ya 178. Katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika Ibara ya Muswada, Serikali inapendekeza kukifuta na kukiandika upya kifungu cha 5(1) kwa madhumuni ya kuiunda upya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika muundo mpya wa bodi wajumbe wafuatao wanapendekezwa kuwemo; Mwenyekiti wa Bodi, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Mjumbe mmoja kutoka Hazina, Mwakilishi mmoja kutoka Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mwanafunzi mmoja kutoka Jumuiya ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Waajiri, Mwakilishi mmoja kutoka Taasisi za Fedha, Mwakilishi mmoja kutoka Mamlaka ya Elimu na Mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Vyuo Vikuu. Pendekezo hili lilitolewa na Mwanasheria Mkuu akikusudia kufanya marekebisho katika Ibara ya 29 iliyopo kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa upande wake ina maoni kwamba ni vyema Katika Wajumbe wa Bodi wanaopendekezwa katika marekebisho haya akawepo mjumbe mmoja kutoka Vyuo Vikuu vya Umma, mjumbe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

mmoja kutoka Vyuo Vikuu Binafsi, Mwakilishi mmoja wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka Vyuo Vikuu vya Umma na Mwakilishi mmoja wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka Vyuo Vikuu Binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni haya ya Kamati yanatokana na ukweli kwamba japokuwa lengo kuu la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni kutoa Mikopo kwa walengwa wenye uhitaji lakini mahitaji ya Vyuo Vikuu Vya Umma na Binafsi ni tofauti sana hivyo ni vyema vyuo Vikuu vya Umma na Vyuo Vikuu Binafsi vikawa na uwakilishi ndani ya Bodi hiyo ili kulinda maslahi ya Vyuo vya Binafsi na Vyuo vya Umma. Kamati inashauri Bodi iwe na uwakilishi wa sekta binafsi ndani ya bodi hasa tukizingatia Sera ya PPP (*Public Private Partnership*).

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali katika Ibara ya 31 la kuiachia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu mamlaka ya kuweza kupanga kiwango cha asilimia ambacho mnufaika wa mkopo atakuwa akikatwa kutoka kwenye mshahara wake ili kurejesha deni kulingana na kiwango cha mshahara na mazingira halisi na uwezo wa mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu lililopo katika Ibara ya 31 ya Muswada. Uungwaji mkono huu unatokana na ukweli kwamba wanufaika wa mikopo wanadaiwa viwango tofauti vya mkopo kulingana na mchepuo aliouchukua aidha pia viwango vya mishahara ya watumishi vinatofautiana hivyo kuweka kiwango cha kukatwa kwenye Sheria kunaweza kuleta ugumu katika utekelezaji kulingana na sababu zilizelezwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*The National Council for Technical Education Act*), Sura ya 129. Katika Ibara ya 36 ya Muswada, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya Kufanya marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Aidha Ibara ya 37 ya Muswada inalenga kuliongezea Baraza la Taifa la Elimu ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Ufundi vyanzo vingine vya mapato ili likusanywe katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ajili ya kuhakikisha ubora wa elimu katika uthabiti na ithibati. Vyanzo hivyo vinajumuisha fedha zitakazopatikana kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, vyanzo vingine vya mapato kama vitakavyoainishwa na Baraza kutokana na huduma wanazotoa na pesa nyingine yoyote itakayopatikana kutokana na Sheia ya Mfuko wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali katika Pendekezo la Muswada katika Ibara ya 36 inapendekeza kufuta na kukiandika upya kifungu cha 6 cha Sheria mama. Lengo la Serikali ni kutaka kifungu hiki kisomeke "*6(3) Every order made under subsection (1) shall be laid before the National Assembly*".

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili linalenga kuondoa utaratibu uliokuwepo awali ambapo agizo la Waziri (*order of the Minister*) la kutaka kugeuza Taasisi ya Mafunzo ya Ufundi kuwa taasisi yenye mamlaka kamili (*self autonomous*) lilikuwa likiwasilishwa Bungeni na kujadiliwa ili kuona kama taasisi husika ina vigezo na sifa stahiki za kuwa mamlaka kamili. Kamati inashauri kwamba Mamlaka ya Bunge ya kujadili agizo la Waziri linapowasilishwa Bungeni la Kutaka kubadilisha Taasisi ya Ufundi kuwa mamlaka kamili liendeleo kujadiliwa na Bunge ili kulipa nafasi Bunge kuona kama agizo hili (*order of the Minister*) linakidhi vigezo na sifa stahiki.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Magazeti (*The Newspapers Act*), Sura ya 229. Sehemu hii inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Magazeti katika Ibara za 40 na 41 za Muswada kwa kuongeza adhabu ya faini kutoka shilingi elfu kumi na tano zilizokuwepo awali na kuweka shilingi milioni tano chini ya Sheria hii kuhusiana na makosa ya matumizi ya lugha za matusi na lugha za uchochezi zinazoweza kuleta machafuko katika jamii.

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba misingi ya uanzishwaji wa vyombo vya habari kama magazeti si kutumia lugha za matusi na kuandika habari za uchochezi zinazoweza kusababisha machafuko bali ni kuhabarisha jamii kuhusu taarifa na matukio mbalimbali yanayohusu jamii. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inaunga mkono pendekezo lililoko katika Ibara za 40 na 41 za Muswada zinazopendekeza nyongeza ya adhabu katika vifungu vya 36(1) na 37(1) (b) vya Sheria ya Magazeti la kuongeza adhabu kwa wale wanaokutwa na hatia ya kutumia lugha za matusi na uchochezi unaoweza kusababisha machafuko.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Viapo (*The Official Oaths Act*), Sura ya 266. Sehemu hii inapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Viapo, Sura Na. 266. Katika marekebisho haya kifungu namba 7 cha Sheria ya Viapo kinarekebishwa kwa lengo la kumjumuisha Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Majaji wa Mahakama ya Rufaa na Majaji wa Mahakama Kuu kula Kiapo cha Uaminifu pamoja na Kiapo cha Ujaji. Aidha, vifungu vya 7 na 12 vinafanyiwa marekebisho ili kuruhusu kiapo kutolewa mbele ya Makamu wa Rais iwapo Rais hatakuwepo na iwapo Rais na Makamu wa Rais hawapo basi kiapo hiki kitolewe mbele ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Kwanza la Sheria linarekebishwa ili kuwezesha Kiapo cha Mahakama kujumuisha Kiapo cha Majaji na Maafisa wa Mahakama. Kamati inaunga mkono marekebisho haya kwa kuzingatia kuwa kuna wakati Rais au Mamamu wa Rais wanaweza wasiwepo nchini hivyo marekebisho yanakusudia kuwezesha viapo kufanyika hata pale ambapo Rais hayupo viapo vifanyike mbele ya Makamu wa Rais na hata pale ambapo Makamu wa Rais hayupo basi Viapo viweze kufanyika mbele ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Kanuni za Adhabu (*The Penal Code*),

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Sura ya 16. Katika Ibara ya 47 ya Muswada, Serikali ilikusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 55(1) kwa kufuta maneno ya ufunguzi yote na badala yake kuweka maneno "Any person who-". Kamati ilifanya uchambuzi na kuona endapo maneno hayo ya ufunguzi (*opening phrase*) yangefutwa basi kifungu chote kingepoteza maana yote iliyopo hivi sasa. Aidha, kifungu kidogo cha (2) nacho kingeathirika kwa kupoteza maana kwa kuwa uwepo wake ulikuwa unategemea uwepo wa maneno ya ufunguzi yaliyopo kwenye sheria kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa baada ya ushauri wa Kamati, Mwanasheria Mkuu aliliona hilo na kukubaliana na ushauri wa Kamati kuwa kifungu hicho kisifanyiwe marekebisho bali kibaki kama kilivyo. Makubaliano hayo yatajionyesha kwenye Jedwali la Marekebisho litakaloletwa Bungeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 48 ya Muswada, Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika vifungu vya 62B (1) kuongeza adhabu zinazotokana na makosa ya matumizi ya lugha za matusi kutoka shilingi elfu moja iliyokuwepo awali na kuwa si chini ya shilingi laki tano kwa faini na kifungu kisichozi miezi kumi na mbili iliyokuwepo awali na kuwa mwaka mmoja. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza adhabu ili kuzuia vitendo vya matumizi ya lugha za matusi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Maana yake hiyo ni kengele ya pili.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba haya maelezo yote ya Kamati yetu yaingie ndani ya *Hansard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Ibara ya 49 ya Muswada inapendekeza kuongezwa kifungu kipya cha 62C mara

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

baada ya Kifungu cha 62B ambacho kinazuia matumizi ya lugha za matusi, lugha za vitisho, michezo ya kuigiza yenye lengo la kuleta uchochezi na uasi dhidi ya Serikali. Adhabu kwa mtu atakayepatikana na hatia kutokana na makosa ya namna hii ni faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja. Kamati inaunga mkono mapendekezo haya ya Serikali kwani vitendo vya utumiaji wa lugha za matusi, vitisho au lugha zenye kuamsha chuki dhidi ya Serikali si vya kuvumiliwa hata kidogo kwani vinaweza kuisambaratisha nchi na kuleta madhara makubwa sana katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi (*The Prevention of Terrorism Act*), Sura ya 19. Sehemu hii inafanya marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Ugaidi Katika Ibara ya 54 kwa kuongeza tafsiri za maneno “*Commissioner of Financial Intelligence Unit*” ili liwe na maana iliyotafsiriwa katika Sheria ya Uzuiaji wa Fedha Haramu (*Anti- Money Laundering*). Aidha, neno “*Financial Intelligence Unit*” (FIU) limepewa tafsiri kumaanisha Idara za Kiwizara (*extra ministerial department*) zinazoundwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Kupinga Fedha Haramu. Tafsiri za maneno hayo kuhakikisha kwamba Idara katika Wizara mbalimbali zenye lengo la kusaidiana katika vita dhidi ya ugaidi na fedha haramu zinasaidiana katika kutimiza majukumu yao. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kwa kiasi kikubwa usafirishaji wa fedha haramu na vitendo vya ugaidi vinaenda sambamba. Hivyo, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya ya kuzioanisha sheria mbili ili kuondoa mkanganyiko katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaunga mkono mapendekezo ya Ibara ya 57 inayopendekeza uanzishwaji wa kifungu kipya cha 41A kinachowataka watoa taarifa (*a Reporting person*) kuwajibika kutoa taarifa mapema katika kitengo cha “*Financial Intelligence Unit*” pale ambapo wana mashaka na miamala yoyote inayopitia katika taasisi zao ili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

kukiwezesha kitengo hiki kiweze kufanya uchunguzi wa haraka kuona kama fedha hizo hazina au zina uhusiano na vitendo vya ugaidi. Kamati ina maoni kwamba adhabu inayopendekezwa ya kulipa faini ya shilingi milioni mia moja au kifungo kisichopungua miaka miwili au vyote kwa pamoja ni sahihi kwani madhara yanayotokana na vitendo vya kigaidi ni makubwa mno kwa jamii hivyo hayastahili kuvumiliwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili – Marekebisho ya Sheria ya Mashirika ya Umma (*The Public Corporation Act*), Sura ya 257. Sehemu hii inahusu marekebisho katika Ibara ya 59 ya Muswada inayorekebisha kifungu cha Sheria ya Mashirika ya Umma (*The Public Corporation Act, (Cap 257)*) kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kifungu kipya kinachoweka masharti kwamba, Shirika lolote la Umma linapokuwa linashtakiwa au linashtaki basi limjulishe Mwanasheria Mkuu kuhusiana na suala hilo. Pia kifungu kidogo cha (3) kinampa haki Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati na kushiriki katika kulinda maslahi ya Shirika la Umma pale linaposhtaki au kushtakiwa.

Kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye Mshauri Mkuu wa mambo ya Sheria, Kamati inaona kwamba kifungu hiki kimeletwa wakati muafaka ili kuhakikisha kwamba maslahi ya Serikali katika Mashirika ya Umma yanalindwa kuepuka Mashirika ya Umma kupata hasara kwa kukosa uwakilishi mzuri wa kisheria kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Majukumu ya Mwanasheria Mkuu pamoja na kuwa yameainishwa katika Sheria nyingine, yamebainishwa katika Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

“59(3) Mwanasheria Mkuu atakuwa ndiye mshauri wa Serikali juu ya mambo ya sheria na na kwa ajili hiyo atawajibika kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo yote ya kisheria, na kutekeleza shughuli nyinginezo zozote zenye asili ya au kuhusiana na

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

sheria zitakazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Rais kuzitekeleza, na pia kutekeleza kazi au shughuli nyinginezo zilizokabidhiwa kwake na Katiba hii au na sheria yoyote"

Hivyo basi, kwa majukumu haya aliyopewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Katiba ni sahihi kwake kushirikishwa pale ambapo Shirika la Umma linashtaki au kushtakiwa ili aweze kulinda maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*The Social Security (Regulatory Authority) Act*), Sura ya 135. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali ya kurekebisha Ibara za 60, 61 na 62 za Muswada zinazokusudia kufanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mfuko ya Hifadhi ya Jamii (*The Social Security (Regulatory Authority) Act*) kwani marekebisho hayo yanakusudia kuongeza uwakilishi wa Mwajiri katika Bodi kwa nia ya kuweka uwakilishi ulio sawa kati ya wafanyakazi na waajiri kwenye Bodi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Vyuo Vikuu (*The universities Act*), Sura ya 346. Katika Ibara ya 64 ya Muswada inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 16 na kukiandika upya ili kuiwezesha Tume ya Vyuo Vikuu kuwa na vyazo vya mapato kutoka katika fedha zinazotengwa na Bunge, misaada na mikopo kutoka chanzo chochote ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano, fedha kutoka katika uwekezaji, miradi, fedha kutoka Mfuko wa Elimu, fedha kutoka Bodi ya Mikopo au fedha kutokana na ada zitokanazo na utoaji wa huduma. Kamati inaunga makono marekebisho haya kwani kwa kufanya hivyo Tume ya Vyuo Vikuu itaweza kupata fedha za kutosha ili iweze kutimiza majukumu yake kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi (*The Vocational Education and Training Act*), Sura ya 82. Katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Ibara ya 66, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 19 cha Sheria mama. Inapendekezwa kwamba kifungu kidogo kipya (2) kiongezwe ili kumwezesha Waziri kutoa msamaha wa ushuru kwa mwajiri au kundi fulani la waajiri ambao mzunguko wao wa fedha haufikii kiasi cha shilingi milioni arobaini kwa mwaka. Kamati inaunga mkono pendekezo hili kwani waajiri ambao vipato vyao havifikii kipato cha shilingi milioni arobaini kwa mwaka itawawia vigumu kutoa (kulipa) ushuru huo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada – Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori (*The Wildlife Conservation Act*), Sura ya 283. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Wanyamapori kwa kufanya marekebisho mbalimbali ambayo kwa namna moja au nyingine yanagusa masuala ya vita dhidi ya ujangili. Kamati inaona kuwa kwa kuwa kumekuwepo na tuhuma nyingi kusuhu matumizi mabaya ya madaraka na unyanyasaji kwa wananchi wakati wa oparesheni hii na kwakuwa Mheshimiwa Spika anakusudia kuunda Kamati Teule ili kuona kama Oparesheni Ondoa Ujangili ilifuata Sheria, Kanuni na Taratibu hivyo ni vyema Marekebisho ya Sheria hii yakasubiri Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema (Mb)-Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam kutoka Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo zinahusika na Sheria mbalimbali zinazorekebisha kwa kutoa ufafanuzi kwa Kamati katika maeneo mbalimbali ya Muswada na kufanya kazi hiyo kwa weledi na kujituma kwani walifanya kazi katika masaa ya ziada na siku za mapumziko, lengo likiwa ni kuhakikisha Muswada huu unachambuliwa vizuri kabla ya kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii vilevile, kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuchambua kikamilifu maoni yaliyowasilishwa na wadau kuhusu Muswada huu na kuchambua Muswada wenyewe Ibara kwa Ibara pamoja na maudhui yake bila kuchoka. Nawashukuru kwa ushirikiano wao na kwa maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yamefanikisha kuboresha Muswada huu pamoja na marekebisho yote yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana – Mwenyekiti, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja – Makamu, Mwenyekiti, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughway Lissu, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Halima James Mdee na Mheshimiwa Zahra Ali Hamad.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashiillah, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati hadi kuandaliwa kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Namwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu, Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, naomba nitoe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act of 2013*. Naomba nifanye hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu za Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013, ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 23 Agosti, 2013 na kusomwa kwa mara ya kwanza tarehe 6 Septemba, 2013. Mwanzoni Muswada huu ulipendekeza marekebisho ya Sheria Mbalimbali kumi na tano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya mapendekezo ya marekebisho ya wanyamapori kuondolewa, sheria ambazo zimebaki na zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ziko 14. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mfuko wa Elimu, Sura ya 412 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346 ya Sheria za Tanzania.

Sheria nyingine ni pamoja na Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Mfuko wa Kichocheo cha Maendeleo ya Jimbo, Sura ya 96 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Filamu na Michezo ya Maigizo, Sura ya 230 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni Sheria za Magazeti, Sura 229 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266 ya Sheria za Tanzania; Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA

UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Mafunzo ya Ufundi, Sura ya 82 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya umuhimu wake kwa haki ya wananchi na kwa maisha ya Taifa letu tunapendekeza kuanza uchambuzi na Sheria ya Magazeti.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya vifungu vya 36(1) na 37(1)(b) vya Sheria ya Magazeti. Lengo la mapendekezo haya ni kuongeza adhabu ya faini kwa makosa ya kuchapisha habari, uvumi au taarifa za uongo zinazoweza kusababisha taharuki au hofu kwa wananchi au zinazoweza kusababisha uvunjifu wa amani (kifungu cha 36(1); au kuchapisha, kusambaza au kutoa taarifa ya uchochezi (kifungu cha 37(1)(b)).

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, adhabu ya makosa hayo ni faini isiyozidi shilingi elfu kumi na tano au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja. Adhabu mpya zinazopendekezwa na Muswada ni faini ya Shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Frederick M. Werema, kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge lako Tukufu, mapendekezo haya "yanalenga kutekeleza azimio lililopitishwa na Bunge letu katika Mkutano wa 11, Kikao cha 21, kulaani tukio la kulipuliwa kwa bomu katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi Parokia ya Olasiti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge liliazimia kwamba, Serikali ipitie Sheria zilizopo ili kuona kama zinatoshesheza kuzuia lugha au kauli za uchochezi (*hate speeches*) na kwa kuwa Sheria hiyo inazuia uchapishaji wa habari zinazoweza kusababisha uvunjifu wa amani na kwa kuwa adhabu ya faini kwa makosa ya kuchapisha habari za uchochezi au zinazoweza kusababisha uvunjifu wa amani ni ndogo kulinganisha na madhara ya kosa husika kwa jamii,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

Muswada unapendekeza adhabu ya makosa hayo kuwa shilingi milioni tano." [Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akiwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2013, kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Dodoma, Novemba, 2013, ukurasa wa 10] Mwisho wa kunukuu maneno ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kujadili mapendekezo ya marekebisho haya kwa kuangalia historia ya Sheria ya Magazeti katika nchi yetu na kupima haja na uhalali wa kuendelea kuwa na Sheria hii katika karne hii ya ishirini na moja.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wa kihistoria wa sheria utaliwezesha Bunge lako Tukufu sio tu kuelewa hali halisi ya uhuru wa habari na uhuru wa mawazo katika Tanzania ya leo, bali pia utaliwezesha Bunge lako Tukufu kupima ukweli na uhalali wa sababu za Muswada huu zilizotolewa na Serikali hii ya CCM. Aidha, *historical analysis* italiwezesha Bunge lako Tukufu kuelewa maana halisi ya mapendekezo haya ili liweze kufanya maamuzi ya busara na yenye ufahamu juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Magazeti ilitungwa kwa mara ya kwanza na dola ya kikoloni mwaka 1928. Hata hivyo, Sheria hiyo haikuwa na vifungu vya jinai za kashfa na uchochezi. Vifungu hivyo viliingizwa katika Sheria za nchi yetu kwa mara ya kwanza mwaka 1953 wakati vifungu vya 51-58, 63 na 63(a) vya Kanuni ya Adhabu vilipotungwa.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la vifungu hivi lilikuwa kuwadhibiti wakosoaji na wapinzani wa sera na dola ya kikoloni waliokuwa wameanza kujitokeza katika miaka hiyo. Ndiyo maana mhanga wa kwanza wa vifungu hivi alikuwa mtu aitwaye Julius Kambarage Nyerere, wakati huo akiwa Rais wa Chama cha Siasa cha Upinzani kiitwacho *Tanganyika African National Union (TANU)* na wenzake wawili. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

Mheshimiwa Spika, kwa wasiofahamu au wasiokumbuka historia ya tulikotoka, mwaka 1957, Mwalimu Nyerere, akiwa mhariri wa gazeti la *Sauti ya TANU* pamoja na Robert Makange, mhariri msaidizi wa gazeti hilo na Rashid Baghdelleh, mhariri wa gazeti la Mwafrika, walishtakiwa kwa kuchapisha kauli ya Mwalimu Nyerere kwamba Wakuu wa Wilaya wa kikoloni waliokuwa wanazuia mikutano ya hadhara ya *TANU* walikuwa wapumbavu! Wakoloni walidai kwamba kauli hiyo ya Baba wa Taifa ilikuwa ya kichochezi na ya kashfa kwao. (*Makofi*)

Hivyo basi, wakoloni walimfungulia mashtaka ya jinai kwa kutumia kifungu hiki hiki ambacho leo, miaka hamsini na sita baadaye, Bunge lako Tukufu linaombwa kukirekebisha kwa kukiongezea adhabu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Martin Sturmer katika kitabu chake cha *The Media History of Tanzania*, Mwalimu Nyerere alipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela au faini ya pauni elfu tatu. Mwalimu alilipa faini hiyo badala ya kwenda jela. Washtakiwa wenzake Makange na Baghdelleh walishindwa kulipa faini na hivyo walifungwa jela na ndio walikuwa *Prison Graduates* wa kwanza kabisa katika historia ya mapambano yetu ya uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, licha ya matukio haya muhimu kisheria na kisiasa katika historia ya nchi yetu yaliyotokea katika miaka ya mwisho ya utawala wa kikoloni, mwaka 1976 ni mwaka muhimu zaidi katika historia ya vyombo vya habari na uhuru wa mawazo. Hii ni kwa sababu ni katika mwaka huo utaratibu wa kisheria na wa kitaasisi wa kudhibiti na kuminya uhuru wa habari na haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari ulikamilika.

Mheshimiwa Spika, mwaka huo Sheria ya Magazeti na Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, zinazopendekezwa kurekebisha na Muswada huu, zilitungwa na Bunge hili Tukufu. Sheria hizi mbili zilitungwa *fasta fasta*: Miswada yake ilisomwa kwa mara ya kwanza na ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]*

pili, kujadiliwa na kupitishwa siku hiyo hiyo, yaani tarehe 16 Machi, 1976. Zote zilipata ridhaa ya Rais Nyerere tarehe 3 Aprili, 1976.

Mwaka huo huo wa 1976, Sheria ya Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA) iliyokuwa na lengo la kudhibiti ukusanyaji, upokeaji na utoaji habari ndani na nje ya nchi yetu, nayo ilitungwa. Sheria hiyo ilipiga marufuku ukusanyaji, upokeaji na utoaji habari ambao haukufanywa na SHIHATA au chini yake au kwa mamlaka yake kwa kuyafanya kuwa makosa ya jinai yenye adhabu ya faini na/au kifungo. Sheria hiyo ilifutwa mwaka 2000 kwa sheria iliyotungwa na Bunge hili Tukufu na kazi ya SHIHATA sasa inafanywa na Idara ya Habari (MAELEZO) ambayo iko chini ya Wizara ya Habari, Michezo, Utamaduni na Vijana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Magazeti, vifungu vya jinai ya kashfa na uchochezi vya 51-58, 63 na 63A vilivyolingizwa kwenye Kanuni ya Adhabu mwaka 1953, vilifutwa na kutungwa upya katika Sheria ya Magazeti. Kwa maana hiyo, kwa kufanya kashfa na kile kiitwacho uchochezi kuwa makosa ya jinai yenye adhabu ya faini au kifungo, Sheria hii iliendeleza matumizi ya sheria za jinai za kashfa na uchochezi zilizokuwa mhimili wa udhibiti wa vyombo vya habari na uhuru wa mawazo wakati wa utawala wa kikoloni wa Kiingereza.

Kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni, lengo kuu la kuweka vifungu hivi katika Sheria ya Magazeti lilikuwa kudhibiti wakosoaji na wapinzani wa sera za Serikali na kuwalinda watawala.

Kwa maneno ya Ndugu Edgar Maokola Majogo, wakati huo Mbunge wa Nachingwea, katika mjadala Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria hiyo katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Pili wa Bunge hili Tukufu uliofanyika tarehe 16 Machi, 1976, kulikuwa bado na "... harufu ya kuwa na kasumba kasumba za kikoloni katika sheria zetu ambazo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA

UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

tumezirithi....” [Kwa mujibu wa majadiliano ya Bunge (*Hansard*) Taarifa Rasmi, Mkutano wa Pili, Tarehe 16 Machi – 18 Machi, 1976, ukurasa wa 42].

Mheshimiwa Spika, kama inavyosema taarifa ya mwezi Julai mwaka huu ya Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari, “tangu uhuru, mamlaka (za Serikali) na (wenye) maslahi ya kibiashara katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki ... zimetumia sheria za jinai zinazohusu uchochezi, kashfa na (lugha) ya matusi, ambazo mara nyingi ni mabaki ya tawala za kikoloni zilizopita kunyamazisha wale wanaowakosoa katika vyombo vya habari.” [Kwa mujibu wa Tom Rhodes , “*A Bid to Rid Africa of Criminal Defamation, Sedition Laws’, Committee to Protect Journalists, July 12, 2013*].

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake, Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Afrika kuhusu Uhuru wa Mawazo na Uhuru wa Habari Bibi Pansy Tlakula amesema kwamba na naomba kunukuu: “Sheria za jinai za kashfa zinatumiwa karibu mara zote kuadhibu ukosoaji halali wa wenye madaraka badala ya kulinda haki za watu kuwa na haiba/sifa wanazostahili.” “*A Bid to Rid Africa of Criminal Defamation, Sedition Laws’, Committee to Protect Journalists, July 12, 2013*]. (Makofi)

Kwa sababu hizi, Katiba Mpya ya nchi ya Kenya imepiga marufuku matumizi ya sheria za jinai za kashfa kuhusiana na mawazo au maoni au matangazo na uchapishaji au usambazaji wa habari kwa kutumia njia yoyote [Kwa mujibu wa Ibara 34(1)(b) ya Katiba Mpya ya Kenya, 2010]. Hata Zimbabwe, licha ya majanga ya kisiasa yaliyosababisha nchi hiyo kuwekewa vikwazo vya kiuchumi, nayo imepiga marufuku matumizi ya sheria hizi kwa mujibu wa Katiba Mpya ya nchi hiyo ya mwaka huu [Kwa mujibu wa Ibara ya 61 ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Zimbabwe, 2013].

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza zaidi ni kwamba, licha ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuonesha mwelekeo wa kupanua uhuru wa maoni, fikra na uhuru wa habari na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

vyombo vya habari katika nchi yetu [Kwa mujibu wa Aya za 29(1) na 30 za Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2013 zinapendekeza kupanua haki ya uhuru wa maoni na uhuru wa habari na vyombo vya habari kwa namna inayofanana kiasi fulani na Katiba Mpya za Kenya na Zimbabwe], inaelekea Tanzania, chini ya Serikali hii ya CCM imebakia nchi pekee katika ukanda huu wa Afrika inayoendeleza 'kasumba kasumba za kikoloni katika sheria zetu ambazo tumezirithi'! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa turudi kwenye sababu za Muswada huu kama zilizovyoeelezwa na Mwanasheria Mkuu Jaji Werema. Kudai kwamba mapendekezo ya Muswada huu yana uhusiano wowote na shambulio la kigaidi katika Kanisa Katoliki Olasiti sio sahihi. Hii ni kwa sababu, hadi leo hii zaidi ya miezi nane tangu shambulio la Bomu la Olasiti, Serikali hii ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi, iwe ndani ya Bunge hili Tukufu au nje ya Bunge, kuhusu sababu za shambulio hilo la kikatili ndani ya nyumba ya ibada, au wahusika wake.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, miezi mitano baadaye, Serikali hii ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi ndani ya Bunge hili Tukufu au nje ya Bunge, kuhusu sababu za shambulio la Bomu la Soweto, Arusha, kwenye mkutano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wa kampeni ya uchaguzi mdogo wa Madiwani lililosababisha vifo vya watu wanne.

Mheshimiwa Spika, ukimya huu mkubwa wa Serikali hii ya CCM, unaashiria kwamba hadi sasa, hata Serikali yenyewe haifahamu sababu za mashambulio hayo ya kigaidi. Kwa maana hiyo, hakuna na hata Serikali hii haijadai upo ushahidi wowote wa kuthibitisha uhusiano kati ya mashambulio hayo na utoaji, uchapishaji na usambazaji wa lugha au kauli za kichochezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dhana ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba mapendekezo haya yanalenga kuzuia *hate*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA

UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

speeches, inapotosha, kwa makusudi, ukweli halisi juu ya lengo na maudhui ya Sheria ya Magazeti na marekebisho yanayopendekezwa kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anafahamu, au anatakiwa afahamu, kwamba '*uchochezi*' katika context ya Sheria ya Magazeti, ni tofauti kabisa na *hate speech*. Uchochezi ni *sedition* au *incitement to violence* kwa lugha ya kimombo. Kwa lugha ya kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Magazeti kinachopendekezwa kurekebisha, '*uchochezi*' ni uchapishaji wa kauli yoyote ya uongo, uvumi au taarifa ambayo inaweza kusababisha hofu na taharuki kwa umma au kuvunja amani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, kama Mwanasheria Mkuu anavyofahamu au anavyotakiwa kufahamu, *hate speeches* ni matamshi au kauli za chuki. Kwa lugha ya aya ya 49 ya Muswada huu, *hate speeches* ni maneno au vitendo au machapisho au picha au mchezo wa maigizo wenye nia ya kujenga chuki dhidi ya kikundi cha watu kutokana na rangi, jinsia, ulemavu, imani, utaifa au asili yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchanganya '*uchochezi*' (*sedition/incitement to violence*) na '*matamshi/kauli za chuki*' (*hate speeches*), Mwanasheria Mkuu wa Serikali inapotosha kwa makusudi maana na lengo halisi la mapendekezo ya Muswada huu kuhusu Sheria ya Magazeti.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu nchi yetu haijawahi kuwa na sheria inayokatiza *hate speeches* kwa maana ya kisheria ya maneno hayo. Ndio sababu Muswada huu unapendekeza kurekebisha kifungu cha 63 cha Kanuni ya Adhabu ili kuingiza matamshi/kauli hizo katika sheria zetu. Kama sheria ingekuwapo, kama anavyodai Mwanasheria Mkuu wa Serikali, basi kusingekuwa na haja wala sababu ya kuleta mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni ya Adhabu yaliyoko katika aya ya 49 ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAMI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

Sheria ya Magazeti hayana msingi kwa sababu nyingine: hakuna ushahidi wowote kwamba adhabu zilizoko katika vifungu vya 36(1) na 37(1)(b) zinazopendekezwa kuongezwa zimeshindwa kudhibiti makosa ya uchochezi. Hii ni kwa sababu, kwa kadri ya ufahamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tangu Sheria hiyo ilipotungwa miaka zaidi ya thelathini na saba iliyopita, hakuna mwandishi habari au mchapishaji wa gazeti lolote ambaye amewahi kufikishwa mahakamani na kupatikana na hatia ya makosa hayo.

Mheshimiwa Spika, badala ya kuwapeleka wakosaji wa aina hiyo Mahakamani wakaadhibiwe kwa mujibu wa Sheria hiyo, Serikali hii ya CCM imejenga utamaduni wa kufungia magazeti na kutisha waandishi habari. Hii peke yake inathibitisha hoja kwamba, Sheria ilitungwa kwa malengo ya kisiasa ya kudhibiti wakosoaji na wapinzani wa Serikali na watawala na sio kuzuia makosa ya jinai *as such*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kwa Bunge lako Tukufu, taarifa ya kesi zote kama zipo zilizofunguliwa Mahakamani kuhusu ukiukwaji wa masharti ya vifungu vya 36(1) na 37(1)(b) vya Sheria ya Magazeti tangu Sheria hiyo ilipotungwa mwaka 1976. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itoe mbele ya Bunge hili tukufu taarifa ya adhabu zozote za faini, kama zipo, zilizotozwa kwa mujibu wa vifungu hivyo ili Bunge hili Tukufu liweze kupima ukweli wa kauli ya Serikali kwamba, adhabu hizo ni ndogo kulingana na ukubwa wa makosa yenyewe. Taarifa hizi zitaliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili na kufanya maamuzi ya busara kuhusu mapendekezo ya Muswada huu, badala ya kufanya maamuzi kwa hisia na taarifa au kauli potofu kama za Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, miaka ishirini na mbili iliyopita, yaani mwaka 1991, Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Nchini Tanzania, maarufu kama , ilisema yafuatayo kuhusu Sheria ya Magazeti na Sheria ya Magazeti ya Zanzibar, 1988:

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA, KATIBA NA UTAWALA]

"Sheria hizi ... zinakwenda kinyume na ibara ya 18(1) ya Katiba zote mbili, ile ya Muungano na ile ya Zanzibar. Aidha, sheria hizi zinawapa Mawaziri mamlaka mengi na makubwa mno. Kwa mfano, Mawaziri wana uwezo wa kuagiza gazeti lisichapishwe tena. Sheria hizi hazitii maanani umuhimu wa magazeti katika jamii kwamba, ni moja ya vyombo muhimu vinavyotoa msukumo wa shughuli za umma.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuwepo sheria ambazo zitayapa magazeti uhuru kamili bila ya kubanwa na chombo chochote cha dola. Tunapendekeza kuwa sheria inayohusu uhuru wa magazeti (*The Freedom of the Press Act*) itengenezwe haraka iwezekanavyo, ikitia maanani vile vile hali iliyopo sasa ya teknolojia ya magazeti [Kwa mujibu wa Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Tanzania, 191, Kitabu cha Kwanza: Taarifa na Mapendekezo ya Tume Kuhusu Mfumo wa Siasa Nchini Tanzania, *para.* 607]." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi chote hicho, Serikali hii ya CCM imekataa kutekeleza mapendekezo haya ya Tume ya Nyalali. Badala yake, kama tulivyosema katika maoni yetu kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo na Vijana wakati wa kikao cha mwaka huu cha Bunge la Bajeti, "... Tanzania imegeuka kuwa Taifa lisilotaka watu kuhabarishwa vizuri juu ya matendo ya watawala. Tanzania imegeuka kuwa Taifa linalofungia magazeti yanayofichua ufasidi, uchafu na matumizi mabaya ya madaraka miongoni mwa viongozi, watendaji na watumishi wa Serikali hii ya CCM. Tanzania imegeuka, chini ya usimamizi wa Wizara na Serikali hii ya CCM, kuwa Taifa linaloteka nyara wanahabari, kuwatesa kwa kuwang'oa kucha na meno, kuwatoboa macho, kuwamwagia tindikali na hata kuwaua [Kwa mujibu wa Maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Habari, Michezo, Utamaduni na Vijana, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Michezo, Utamaduni na Vijana kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Dodoma, Juni, 2013]." (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA, KATIBA NA UTAWALA]

Mheshimiwa Spika, miezi mitatu haikupita tangu tuseme maneno haya kabla ya Serikali hii ya CCM kuthibitisha ukweli wake kwa kutumia Sheria ya Magazeti kuyafungia magazeti ya Mtanzania na Mwananchi [Kwa mujibu wa *Committee to protect Journalists, Tanzania suspends two leading newspapers, Nairobi, September 30, 2013*]. Sasa, kwa Muswada huu, badala ya kupendekeza sheria hii ifutwe kama ilivyokuwa kwa Sheria ya SHIHATA na kama ilivyopendekezwa na Tume ya Nyalali, Serikali hii ya CCM inaliomba Bunge lako Tukufu kuiongezea makali zaidi!

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kuuondoa Muswada huu kwa mujibu wa kanuni ya 90 ya Kanuni za Kudumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sio hivyo tu, kwa kuzingatia historia ya Sheria hii na mapendekezo ya muda mrefu kama tulivyoonysha kwenye Maoni haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kufanya kile ilichokifanya kuhusiana na Sheria ya SHIHATA: kuleta Muswada katika Bunge lako Tukufu wa kuifuta kabisa Sheria ya Magazeti na kutunga sheria mpya itakayohifadhi uhuru wa habari na uhuru wa mawazo.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi na Serikali inayojidai kumuenzi Baba wa Taifa, ni aibu kwa Serikali hii ya CCM kuendeleza sheria ya jinai ya kashfa na uchochezi iliyotumika kumtia hatiani Mwalimu Nyerere na waandishi habari wenzake wawili zaidi ya nusu karne iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Sheria ya Filamu na Michezo ya Maigizo, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 34 cha Sheria ya Filamu na Michezo ya Maigizo. Kwa mujibu wa mapendekezo ya marekebisho, adhabu ya kukiuka masharti mbalimbali ya Sheria hiyo itaongezeka kutoka faini isiyozidi shilingi elfu tano au kifungo kisichozi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja, hadi faini isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo kisichozi miaka miwili jela au vyote kwa pamoja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

Mheshimiwa Spika, ni wazi, kama ilivyo kwa mapendekezo yanayohusu Sheria ya Magazeti, kwamba lengo kuu la mapendekezo haya ni kuongeza makali ya sheria hii badala ya kupanua uhuru wa mawazo na fikra.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yake kwa Kamati, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alidai kwamba, lengo la mapendekezo haya ni kuongeza adhabu kwa mtu atakayetenda kosa chini ya sheria hii ikiwemo kutoa filamu au mchezo wa kuigiza wenye lugha ya uchochezi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa maoni ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, mapendekezo haya yanalenga kutekeleza Azimio la Bunge lililopitishwa katika kikao cha 21 cha Mkutano wa 11 kulaani tukio la kulipuliwa kwa bomu katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi, Parokia ya Olasiti.

Mheshimiwa Spika, moja ya maazimio ya Bunge ilikuwa ni kwamba, Serikali ipitie Sheria zilizopo ili kuona kama zinatoshesheza kuzuia lugha au kauli za uchochezi yaani *hate speeches*. Hivyo, kwa maneno ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali adhabu inayopendekezwa inalenga kuzuia lugha au kauli za uchochezi zinazoweza kutolewa kwa kupitia filamu au michezo ya kuigiza [Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akiwasilisha Muswada wa Marekebicho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2013, kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Dodoma, Novemba, 2013, ukurasa wa 7].

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikubaliani na mapendekezo haya na sababu zilizotolewa na Serikali hii ya CCM. Aidha, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, lengo halisi la mapendekezo haya ni kuendelea kuminya na kudhibiti uhuru wa mawazo, maoni na fikra ambao umehifadhiwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Kutumia tukio la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]*

Bomu la Olasiti kama sababu ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii ni kutumia janga hilo ili kuficha malengo halisi ya Serikali hii ya CCM.

Kwanza, hadi sasa zaidi ya miezi nane tangu shambulio la Bomu la Olasiti, Serikali hii ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi, iwe ndani ya Bunge hili Tukufu au nje ya Bunge, kuhusu sababu za shambulio hilo la kikatili ndani ya nyumba ya ibada, au wahusika wake. Vivyo hivyo, miezi mitano baadaye, Serikali hii ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi ndani ya Bunge hili Tukufu au nje ya Bunge, kuhusu sababu za shambulio la Bomu la Soweto, Arusha, kwenye mkutano wa CHADEMA wa kampeni ya uchaguzi mdogo wa Madiwani lililosababisha vifo vya watu wanne.

Pili, kama ilivyo hivi sasa, Sheria ya Filamu na Michezo ya Maigizo haina makatazo yoyote juu ya matumizi ya lugha au kauli za uchochezi kwa kupitia filamu na michezo ya kuigiza. Ukweli ni kwamba, Sheria hii haikutungwa kwa lengo la kuzuia uchochezi au ugaidi kwa kutumia filamu au michezo ya kuigiza, badala yake, Sheria hii ilitungwa kama sehemu ya silaha za uhibitaji wa mawazo, maoni na fikra.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa kauli hii uko katika hotuba ya Waziri wa Utamaduni wa Taifa na Vijana wakati huo, Meja Jenerali Mirisho H. Sarakikya, wakati wa kujadili Muswada wa Sheria hiyo katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Pili wa Bunge hili Tukufu tarehe 16 Machi, 1976: alisema yafuatayo:

“Ndugu Spika, Muswada huu unakusudia kuweka sheria mpya badala ya Sheria ya Ukaguzi wa Filamu za Sinema inayotumika sasa ... ambayo itafutwa. Sheria hiyo mpya itakuwa na masharti bora zaidi ya kusimamia utengenezaji wa Filamu za Sinema, maonyesho ya Picha za Sinema na utoaji wa Leseni kwa ajili ya majumba ya kuonyesha Sinema.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo kutungwa kwa sheria mpya kumetoa fursa ya kuweka masharti ya Sheria

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]]

itakayosimamia maonyesho ya Michezo ya Kuigizwa au ya Kitamaduni kwenye majukwaa au kwenye kumbi za maonyesho. Masharti hayo yatafanya maonyesho ya michezo hiyo yapatane na utamaduni wa Kitanzania [Kwa mujibu wa Majadiliano ya Bunge (*Hansard*): Taarifa Rasmi, Mkutano wa Pili 16 Machi – 18 Machi, 1976, ukurasa wa 47].

Mheshimiwa Spika, Meja Jenerali Sarakikya alielezea nguzo kuu ya Sheria hii kwa maneno yafuatayo, naomba kunukuu tena:

“Sharti lililopo kubwa kupita yote katika Muswada inasema utengenezaji wa filamu ya sinema ambayo inakusudiwa kuonyeshwa au kuuzwa humu nchini au nje ya nchi hii, ni lazima ifanywe kwa leseni na kwa kufuata masharti ya leseni hiyo ambayo itatolewa na Waziri mwenye dhamana juu ya ukaguzi wa filamu ya sinema. Kwa hiyo, ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuongoza, kusaidia au kushiriki katika utengenezaji wa filamu ya sinema ambayo haikukatiwa leseni [Kwa mujibu wa Majadiliano ya Bunge (*Hansard*): Taarifa Rasmi, Mkutano wa Pili 16 Machi – 18 Machi, 1976, ukurasa wa 47].

Mheshimiwa Spika, dhana hii ya Sheria kama silaha ya udhibiti wa kiitikadi yaani *ideological control* imekuwepo tangu zama za ukoloni na ni sehemu ya harufu ya kasumba kasumba za kikoloni katika sheria zetu ambazo tumezirithi, kama alivyosema Mheshimiwa Maokola Majogo. Ndiyo maana katika hotuba yake Bungeni, Meja Jenerali Sarakikya alisema kwamba masharti ya Sheria hii ... yanafanana na masharti ya sheria inayotumika sasa ila ina tofauti mbili nazo ni kwamba, Muswada huu unahimiza matumizi zaidi ya lugha ya Kiswahili katika utengenezaji wa filamu za sinema na kwamba vitendo vyovyote vilivyo kinyume cha sheria vitaadhibiwa vikali zaidi kwa mujibu huo au kwa mujibu wa sheria hii [Kwa mujibu wa Majadiliano ya Bunge (*Hansard*): Taarifa Rasmi, Mkutano wa Pili 16 Machi – 18 Machi, 1976, ukurasa wa 47].

Mheshimiwa Spika, katika utafiti wake wa hivi karibuni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

Juu ya Uchumi Siasa wa Sinema Filamu za Video nchini Tanzania, Dkt. Mona Mwakalinga wa Idara ya Sanaa za Maonyesho ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, amesema kwamba, tangu miaka ya mwanzo ya uhuru, Serikali ya Tanzania, iligundua kwamba filamu ni chombo muhimu. Serikali iligundua kwamba endapo filamu itaangukia katika mikono mibovu ingeweza kutumiwa dhidi yake. Viongozi wa Kiafrika wana hofu kuunga mkono sekta ya filamu kwa sababu wanaogopa kwamba sinema inaweza kutumiwa na watengenezaji filamu kupotosha mazingira ya kisiasa [Kwa mujibu wa Mwakalinga, M., 'The Political Economy of Cinema (Video Film) in Tanzania', *African Review*, Vol. 40, No.1, 2013:203-217, 2016].

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kauli ya Serikali hii ya CCM kwamba, mapendekezo haya yanalenga kudhibiti lugha au kauli za uchochezi kupitia filamu na michezo ya kuigiza ili kuzuia vitendo vya kigaidi kama mashambulio ya mabomu ya Olasiti na Soweto ya Arusha, hayana msingi wala ushahidi wowote. Lengo ni lile lile alilolisema Meja Jenerali Sarakikya miaka thelathini na saba iliyopita; kuendeleza udhibiti wa kiitikadi wa watawala dhidi ya wananchi kwa kuhakikisha kwamba vitendo vyovyote vilivyo kinyume cha sheria hii vitaadhibiwa vikali zaidi kwa mujibu kwa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya Adhabu; Aya ya 47 ya Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Kanuni ya Adhabu kwa kuweka adhabu mpya dhidi ya malengo ya kichochezi *seditionous intention* yaliyotajwa katika kifungu cha 55(1). Adhabu inayopendekezwa ni faini ya shilingi milioni tano au kifungu jela kwa muda usiopungua miaka mitano. Kwa sasa kifungu cha 55 hakitengenezi kosa lolote la jinai bali kinafafanua maana ya makosa ya uchochezi yaliyohamishiwa katika Sheria ya Magazeti.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, mapendekezo haya yameletwa Bungeni bila ya Serikali hii ya CCM kufanya tafakuri au utafiti wowote. Kwanza, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali angefanya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

utafiti kidogo tu angegundua kwamba kifungu cha 55 hakina na hakijawahi kuwa na sababu yoyote ya kuendelea kuwepo katika Kanuni ya Adhabu. Hii ni kwa sababu kifungu hicho hicho kilitungwa upya, kwa maneno yale yale, kama kifungu cha 31 cha Sheria ya Magazeti.

Pili, makosa ambayo kifungu hicho kinachoyafafanua hayako tena kwenye Kanuni ya Adhabu, bali yako katika Sheria ya Magazeti. Inaelekea katika fasta fasta ya kupitisha Muswada wa Sheria ya Magazeti, kifungu cha 55 kilisahuliwa katika Kanuni ya Adhabu wakati vifungu vyote vinavyohusu makosa ya uchochezi na kashfa ya kijinai vilipohamishiwa katika Sheria ya Magazeti.

Tatu, kwa kuwa kifungu cha 55 cha Kanuni ya Adhabu ni cha ufafanuzi tu, hakuna sababu wala mantiki yoyote kisheria kukibadilisha na kukifanya kuwa *substantive section*, yaani kifungu kinachotengeneza makosa ya jinai. Sababu ya hoja hii ni rahisi sana; tayari kuna kifungu cha 32 cha Sheria ya Magazeti kinachotengeneza makosa ya uchochezi kwa matendo ambayo tayari yameshafafanuliwa katika kifungu cha 31 cha Sheria hiyo! Kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba mapendekezo ya aya ya 47 ya Muswada huu yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Elimu na Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Aya ya 22 inapendekeza kwamba fedha za Mfuko wa Elimu ziwe ni pamoja na tozo ya uendelezaji wa stadi kama zilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mapendekezo ya aya ya 20, fedha hizo sasa zitatumika kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya Mamlaka ya Elimu, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Tume ya Vyuo Vikuu na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, kwa *formula* iliyowekwa katika Jedwali lililoko kwenye mapendekezo haya.

Maana ya mapendekezo haya ni kwamba fedha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

ambazo, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha iliyotungwa na Bunge hili hili mwaka jana, sasa zinakwenda moja kwa moja kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, zitatakiwa zipelekwe kwanza kwenye Mfuko wa Elimu, halafu ndiyo zipelekwe katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, kabla...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Tundu Lissu, samahani. Ninayo hotuba yako, lakini hayo unayosema sasa siyaoni kwenye hotuba yako.

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA KATIBA NA SHERIA: Yapi?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Unazungumzia ya elimu, mambo ambayo yako kwenye hotuba yako ni mambo matatu. Kwanza, Sheria ya Magazeti, kuanzia ukurasa wa tatu mpaka ukurasa kumi na moja. Halafu unaanza Sheria ya Filamu na Michezo ya Maigizo ukurasa wa kumi na moja mpaka ukurasa wa kumi na nne; halafu unaanza Kanuni ya Adhabu unaishia ukurasa wa kumi na sita, mwisho. Halafu unaanza ukurasa wa kwanza na wa pili na hayo hayamo.

SPIKA: Naomba Mheshimiwa Tundu Lissu ukae chini kidogo. Hapo hapo kaa tu kiti cha kwanza tu!

Inaelekea kwa sababu ya kuchapa haya mambo haraka, kuna karatasi nyingine hazijachapwa vizuri kwa sababu hii niliyonayo inaendelea ina *page* nyingine. Kwa hiyo, nafikiri katika uchapaji wa haraka, kuna karatasi nyingine zime-*miss*, lakini mimi ninazo zote. Kwa hiyo, naona tutaliangalia hili. Kwa hiyo, naomba uendelee ni dakika mbili. Zimebaki dakika ngapi?

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Tatu.

SPIKA: Mbili na nusu, haya malizia dakika zako.

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Maana ya mapendekezo haya ni kwamba, fedha ambazo, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha iliyotungwa na Bunge hili hili mwaka jana ambazo sasa zinakwenda moja kwa moja kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, zitatakiwa zipelekwe kwanza kwenye Mfuko wa Elimu, halafu ndiyo zipelekwe katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, kabla ya Bodi hiyo kuzipeleka katika vyuo husika kwa ajili ya kugawiwa kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, urasimu unaopendekezwa na Muswada huu utasababisha ucheleweshaji mkubwa wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ambao tayari ni tatizo sugu. Aidha, mapendekezo haya yatasababisha mateso na usumbufu kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi ni moja ya sababu kubwa za vita isiyokwisha kati ya wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na Serikali hii ya CCM. Badala ya kutatua tatizo hili na kurejesha amani katika vyuo vyetu vikuu, mapendekezo haya yatalikuzia tatizo hili na kusababisha vurugu kubwa zaidi katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapinga vikali mapendekezo haya na inashauri yaondolewe kabisa kwenye Muswada huu. Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza fedha zinazotokana na tozo ya uendelezaji wa stadi ziende moja kwa moja kwenye Bodi ya Mikopo kama utaratibu wa sasa ulivyo, badala ya kuzitengenezea mlolongo wa kirasimu usiokuwa tija yoyote kwa wanafunzi wa taasisi ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, wakati Muswada huu unapendekeza kuhamisha fedha za tozo ya uendelezaji wa stadi kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwenda kwenye Mfuko wa Elimu, mapendekezo ya aya ya 23 yamewanyima wanafunzi uwakilishi katika Bodi ya Mamlaka ya Elimu ambayo ndiyo itakayofanya maamuzi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

kuhusu fedha hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kueleza sababu za kutokuwepo kwa uwakilishi wowote wa wanafunzi katika muundo mpya wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Serikali itolee jambo hili maelezo kwa sababu katika muundo wa sasa wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuna wawakilishi wawili wa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu za umma na zile za binafsi. Kwa nini busara hiyo hiyo isitumike katika kuunda Bodi ya Mamlaka ya Elimu itakayosimamia fedha za Mfuko wa Elimu kama inavyopendekezwa na Muswada huu.

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, muundo unaopendekezwa ni sharti uweke uwakilishi wa wanafunzi wawili watakaowakilisha taasisi za elimu ya juu za umma na zile za binafsi kama ilivyo kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba yale ambayo sijayasema yaingie kwenye *Hansard*, nashukuru sana.

SPIKA: Ahsante.

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kuzuia Ugaidi; kwa mujibu wa maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sheria ya Kuzuia Ugaidi inapendekezwa kurekebishwa ili kuzilazimu taasisi za fedha au watu wengine, kutoa taarifa kuhusiana na suala lolote ambalo taasisi au mtu huyo ataona kuwa linahusika kwa namna moja au nyingine na ufadhili wa ugaidi au linakusudia kufadhili shughuli yoyote ambayo inasimamiwa na au kwa niaba ya kundi la kigaidi kwenye Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]

haina pingamizi na mapendekezo haya. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuzungumzia masuala yanayohusu utekelezaji wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha karibu mwaka mmoja sasa, kumejitokeza matukio ya matumizi mabaya ya utaratibu wa Kimahakama kuhusiana na utekelezaji wa Sheria ya Kuzuia Ugaidi. Kwa ushahidi ambao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inao, kumejitokeza tabia ya baadhi ya viongozi wa ngazi za juu wa CCM kula njama za kuwatengenezea wanachama na Viongozi wa Vyama vya Upinzani, hasa CHADEMA, kesi za uongo za ugaidi.

Mheshimiwa Spika, katika tukio mojawapo lililotokea mwishoni mwa mwaka jana, mwandishi mwandamizi wa mojawapo ya magazeti yanayochapishwa kila siku hapa nchini, kwa kushirikiana na Naibu Katibu Mkuu wa CCM walimlipa fedha mwanachama mmoja wa CHADEMA ili akarekodi mazungumzo kati yake na Mkurugenzi wa Ulinzi na Usalama wa CHADEMA ambayo baadaye yalitumika kuwafungulia wote wawili mashtaka ya kigaidi kwa mujibu wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, katika tukio lingine, wanachama watano wa CHADEMA walifunguliwa mashtaka ya ugaidi katika Mahakama ya Hakimku Mkazi, Tabora. Kesi hiyo baadaye ilipelekwa mbele ya Mahakama Kuu ya Tanzania katika kesi ya Henry Kilewo & Wenzake wanne dhidi ya Jamhuri, *Miscellaneous Criminal Application No. 53 ya 2013*. Katika kesi hiyo, Mahakama Kuu ya Tanzania, Jaji Lukelelwa, ilikemea vikali vitendo vya matumizi mabaya ya Sheria ya Ugaidi ambayo imesababisha watu wasiokuwa na hatia ya makosa hayo wanatuhumiwa nayo ili tu wanyimwe dhamana na wataabike magerezani.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanaofanya vitendo kama hivi viovu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kuwakumbusha msimamo wa chama chao kabla hakijageuka kuwa kama kilivyo leo. Katika uchambuzi wake wa Azimio la Arusha, Baada ya Miaka Kumi, uliotolewa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA]*

mwaka 1977, CCM ilikiri kwamba, kuna mifano ya wananchi wetu kuteswa na viongozi wa Serikali na Chama ambao walitarajiwa kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, wakati vitendo hivyo vya ukatili vinapoanza kujulikana, juhudi kubwa sana zinafanywa kuwanyamazisha ama wale walioteswa ama wale waliojipiga vifua kutoa habari badala yao. Haya ni mambo ya aibu. Lazima katika jambo hili Chama chetu kiwe macho sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria nyingine ambayo hatujayazungumzia katika maoni haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono msimamo wa Kamati ya Kudumu ya Bunge lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote haya, tunaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mnajua, naomba tuelewane na hii napenda watu wote waelewe. Utaratibu wa Bunge ambalo linafanya kazi kwa kutumia Kamati zake, kazi kubwa kabisa ya Miswada yetu, inafanyika kwenye Kamati. Ndiyo maana tunaalika na watu wengine wa nje kushiriki kwenye uundaji wa Miswada yetu. Huko ni sehemu muhimu sana ya kufanya kazi zetu katika Bunge.

Kwa hiyo, nashawishika kusema kwamba, kumetokea tabia ya kuamini kwamba Kamati hazina umuhimu, zina umuhimu wa pekee. Muswada wowote hautakiwi kuja Bungeni, unatakiwa ujadiliwe na Kamati kwanza. Hakuna namna Spika, anaweza kuingiza Muswada hapa kama Kamati haijamwambia kwamba, tumefanya kazi vizuri, tumemaliza sasa uingie Bungeni. Huo ndiyo utaratibu na napenda wananchi wajue hivyo na wanapoalikwa na Kamati, maana yake ni hiyo.

Kwa hiyo, sasa nina wachache ambao ningependa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

wachangie, muda wetu ni mfupi, kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla na wengine watachangia jioni.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, aliyesoma taarifa ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti, lakini pia niwapongeze kwa mara nyingine, wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, waliochambua kwa umakini wa hali ya juu. Naunga mkono taarifa hiyo ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna marekebisho ya sheria kumi na tano.

SPIKA: Naomba kidogo tukubaliane. Tulipokuwa tunafanya dakika kumi ilikuwa ni Kamati ya Mpango, tulichukua kanuni zile za fedha, lakini sasa tunaingia dakika zile za kawaida, kwa hiyo ni dakika kumi na tano kama kawaida; hivyo, wengine niliowataja hapa hawatafikiwa kwa sababu muda hautoshi. Mheshimiwa Pindi endelea!

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kuna marekebisho ya sheria zipatazo kumi na tano. Kwa hiyo, naomba nianze kama ifuatavyo kwamba, naunga mkono marekebisho ya Sheria ya *Civil Aviation Act*, lakini niseme kwamba, *Civil Aviation Act* imepewa fursa ya kukopa. Sasa kulikuwa na neno pia iruhusiwe kukopesha, kwa hiyo nadhani *Civil Aviation Act* na masuala ya kukopesha hayaendani, kwa hiyo, ningeomba hapo neno kukopesha katika kifungu cha sita liondolewe.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo naunga mkono pia, ni kuhusiana na Sheria ya *Education Fund*. Amesema kuwa kutakuwa na *additional fund* ambazo hizo *additional fund* zitapita *educational fund* na kwenda katika *level* mbalimbali. *Higher learning*, vyuo vya VETA. Kwa hiyo,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. P. H. CHANA]

tunaomba kwenye zile pesa za *Education Fund*, kifungu cha 29 ziende *at all levels* hivyo, shule za msingi na sekondari pia zikumbukwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo naliunga mkono kwa asilimia mia moja, ni kifungu cha 36 kwamba, *every order made under section (1) shall be laid before the National Assembly*. Kwa hiyo, nasema hizo taarifa zinazotoka kwa Waziri wa Elimu zisiwe *laid before the National Assembly* lakini ziwe *laid and discussed*. Kwa hiyo, kifungu hicho kibaki kama kilivyokuwa mwanzo, siyo ku-*table* tu mezani, lakini Bunge pia lipate kujadili maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu Sheria za Wanyamapori. Kulikuwa na Sheria za Wanyamapori ambazo zimeletwa kufanyiwa marekebisho. Kwa hiyo, niungane na maoni ya Kamati kwamba, zile Sheria za Wanyamapori, tukizingatia maamuzi yako Spika, umeunda Kamati Teule kuangalia Masuala ya Wanyamapori, ningeomba Sheria zile za *Wildlife Conservation Act*, zisubiri.

SPIKA: Mheshimiwa zimeondolewa kwa sasa, kwa hiyo, hakuna haja ya kupoteza muda.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Ndiyo, sawa, kwa hiyo naunga mkono mawazo hayo. Marekebisho mengine ni *Prevention of Terrorist Act*, ambayo kutakuwa na *intelligence Unit*. Hiyo *intelligence Unit* itakuwa ina haki ya kuomba taarifa kutoka kwenye Benki mbalimbali. Marekebisho haya yaliyokuja nayaunga mkono, kwamba, Benki zitapaswa kutoa taarifa pale inapopaswa kupeleka kwa *financial intelligence Unit* ili kupunguza masuala ya kufadhili shughuli za Ugaidi. Niombe sana Taasisi zetu za fedha ziwe zinatoa ushirikiano wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja sasa niende kwenye Sheria ya Magazeti. Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaruhusu uhuru wa maoni na pia kuna uhuru wa vyombo vya habari. Kuna marekebisho yamekuja hapa. Naomba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. P. H. CHANA]

kuhoji leo vyombo vya habari, *press and media*. Vyombo vya habari katika nchi yetu wakati mwingine vimekuwa vikitumika ndivyo sivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malengo ya Serikali ilipoleta marekebisho haya, wametuambia kwamba, malengo ya marekebisho ya Sheria ya Magazeti ni kulenga kuongeza adhabu ili kulinda matumizi ya lugha ya matusi, makosa haya yanajumuisha matumizi ya lugha za uchochezi ambazo zinaweza kusababisha machafuko katika jamii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina amani, hii ndiyo hazina. Unapofanya *SWOT analysis* unaangalia una *resources* gani. Kwa hiyo, ya kwanza kabisa Tanzania unaanza na amani hiyo ni *capital*, lakini ni ukweli ambao kila Mtanzania anafahamu, magazeti yetu kuna wakati yanatumika na kikundi fulani, kuwabeba kikundi fulani au mtu fulani na kuangamiza kikundi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina majibu ya moja kwa moja, lakini naomba leo nipate majibu. Nauliza kwa Bunge lako Tukufu. Pale ambapo gazeti linamdhalilisha mtu, halina ushahidi, gazeti linaandika kitu fulani bila ushahidi wa Mahakamani kwamba huyo mtu kweli ana makosa. Kwa mfano, inaandikwa fulani ni jangili. Watu wamewekwa picha zao pale, eti ni majangili. Wanasheria wanasema jambo hili linakwenda Mahakamani, Mahakama ikithibitisha ndiyo unasema huyu jangili, lakini hata haijathibitishwa, kuna watu majangili imewekwa pale. Hasa huyu mtu hata kesho akiomba msamaha, tayari heshima yake kwenye jamii imeondoka, tayari yamkini alikuwa na mikataba fulani fulani, hawatafunga mkataba naye watasema wewe ni jangili.

Mheshimiwa Spika, sasa haya mambo tufanyeje na mimi majibu sina, nawauliza *editors* na naomba wale mnaoweka kipima joto kwenye *TV*, tuweke kipima joto. Pale ambapo magazeti yanatumika kuchochea ndivyo sivyo, je, huu ni uhuru wa habari? Watanzania wote tujaze kile kipima joto. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. P. H. CHANA]

Tunafanyaje Watanzania pale ambapo magazeti, *The Newspaper Act* tunayo, lakini yanatumika kuvunja amani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna nchi tumeshuhudia, Misri leo hii kuirudisha ile amani ni changamoto, kuna nchi tunaona wanapigana, tunafanyaje Watanzania? Tusaidiane. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, natambua mchango mkubwa wa magazeti, *communication*, taarifa, nchi ambayo haina magazeti, ni hatari kubwa. Lazima tuwe na magazeti, watu wapate taarifa mbalimbali kwenye magazeti, lakini pale ambapo yanatumika ndivyo sivyo inakuwaje? Kunakuwa na waandishi wa habari, wanalipwa fedha, wanammaliza mtu. Hususan kwa wanasiasa, yanatumika sana, tunafanyaje Watanzania? *The Newspaper Act* ifanyeje? Tunakwenda kwenye Katiba mpya, tusaidiane. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi sina matatizo na waandishi wa habari, nina wanangu wengi nawapenda, *editors*, na wamekuwa wanarifagilia sana kwenye magazeti, hata nikikumbuka Bunge lililopita nawapenda sana, lakini pale ambapo haitakiwi iwe samaki mmoja akioza, samaki wote wameoza, Yule samaki mmoja tumtoe *faster*, yule anayedhalilisha *professional* ya Waandishi wa Habari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, unakuta kuna chombo kama *BBC*, *Voice of America*, *they have no politics*, wanatoa *data*, *statistics* na ukienda kusema mbona mmesema hivi, wanakueleza, lakini magazeti yetu, leo watasema Mr. Pindi Chana, kumbe ni Bibi! Kesho wanasema, samahani tunaomba radhi, alaa! Kumbe mlikuwa mnaandika hamjui kama huyu mtu ni mwanamke au ni mwanamme! Unatoaje habari bila kufanya *due diligence* na huo ni mfano tu nimejitolea mwenyewe. (Makofi)

Yaani magazeti yetu kutwa kuomba radhi, jana tulisema hivi, hatukumaanisha hicho. Sasa watu wanabaki na ile *information* ya mwanzo. *I am talking of The Newspaper Act*, tufanyeje pale ambapo magazeti yanachochea na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. P. H. CHANA]

yanavunja amani. Amani hii tumeipigania sana, tumetumia nguvu kubwa, leo hii *East Africa, Sub Sahara Africa* hazina yetu Tanzania ni amani, hakuna ukabila, hakuna udini. Sasa haya magazeti tushirikiane, tusaaidiane tupeleke nchi yetu mbele, wawekezaji waje watupe mfano, *Tanzania no tribalism, no whatever*. Wale ambao wanatumika ndivyo sivyo, kwa kweli naomba leo Bunge hili Tukufu litupe majibu na tupo Wabunge 357.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo kabisa na maoni mbalimbali ya AG, lakini pale ambapo unakuta Spika anafanya kazi vizuri, Rais wa Jamhuri ya Muungano, anafanya kazi vizuri, lakini hizo *headlines, they are too judgmental*. Vichwa vya habari vinahukumu kabla ya jambo lenyewe halijakwenda Mahakamani. Naomba niwahoji Watanzania wenzangu, tusaaidiane, pale ambapo magazeti yanatumika kuharibu amani, kuchochea vurugu, kumdhalilisha mtu, au kikundi cha watu, Chama au Vyama, kuhatarisha amani, tuna mashirika ya dini, ni nini kifanyike? Ndiyo swali langu na sina majibu lakini na mimi nahoji nini kifanyike? Najua kuna wataalam wa sekta hiyo, wa *press* na *media*, na kipima joto muweke hilo swali, nini kifanyike? Je, ndiyo uhuru wa habari, tuseme ruksa tu, ruksa tu. (*Makofi*)

Watu waropoke, waseme, wadhalilishane, tuna watoto, tuna ndugu, tuna familia, tuna *donor community*! Kuna *partnership* za Kimataifa, tuko sehemu ya *United Nations*! Lazima tuwe na *ethics*, maadili. Maadili yetu yako wapi Watanzania! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii nimechelewa nilitaka nikachukue magazeti nije nisome *headlines* hapa nioneshe, angalia gazeti hili. Kwa hiyo, kwa vile sinayo, naomba iwe *homework* ya kila mmoja tukitoka hapa, mkasome mahali pengi wanauza magazeti, *library*, tusome *headlines* za leo. Zile *headlines* kwelikweli ambazo zimewekwa zina afya? Hiki kizazi chetu, watoto wetu tunawafundisha nini? Magazeti ni mahali pa kuwapa elimu watoto wetu, pa kuwafundisha na sina majibu, Watanzania tufanyeje? (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. P. H. CHANA]

Mhesimiwa Spika, maeneo mengine, naunga mkono taarifa ya Kamati, naunga mkono mapendekezo mengi ambayo yametolewa, lakini naunga mkono na nakuachia swali, pale ambapo magazeti, *The Newspapers* yanatumika ndivyo, sivyo, siyo kwa kujenga, tufanyeje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lisu atajibu. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii, lakini nianze kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nichukue nafasi hii niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mbunge Mahiri kabisa, msomi wa eneo hili la Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Kamati imefanya kazi ya kutosha na imefanya uchambuzi makini na kutuletea Muswada huu hapa mbele. Niseme kwamba, kabla sijaendelea katika maeneo mengine, lakini taarifa ya Kamati tumesikia hapa imejikita katika maeneo yote ya msingi kama yalivyoorodheshwa.

Mheshimiwa Spika, pia tumesikia taarifa ya Kambi ya Upinzani, imetumia takribani robo tatu ya taarifa nzima kuzungumza suala la magazeti. Nafikiri katika Muswada huu taarifa muhimu zaidi ninavyoiona kwangu hapa na nitaanza nayo hiyo, halafu hizo nyingine nitazizungumzia, ni suala zima la Bodi ya Mikopo iliyozungumzwa katika taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niunge mkono mabadiliko haya yanayofanywa katika Muswada huu ili kurekebisha vifungu vya uchangiaji na mapato ya fedha katika Mfuko wa Elimu, lakini yale mabadiliko pia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

yanayokwenda kupeleka fedha katika Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, wanafunzi wetu na watoto wetu wa Kitanzania wanaweza kupata elimu katika vyuo vikuu vilivyojengwa na Serikali makini ya Chama cha Mapinduzi, ambavyo vinatoa elimu kwa watoto wote katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na eneo lifuatalo:-

Mheshimiwa Spika, nimepokea jedwali la marekebisho kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ukurasa wa nne wa jedwali hili, kifungu namba 32(a), kinaamuru kwamba sasa Bodi ya Mikopo, itazitaka taasisi zote za kiserikali na zisizo za Kiserikali, kuhakikisha zinatoa taarifa kuhusiana na wanufaikaji wa mikopo, yaani wanafunzi, ili kujua ni kwa kiwango gani wanafunzi wetu na watoto wetu wa Kitanzania wamenufaika na mikopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwanza hoja hii, lakini hapo sasa ndipo ninapokuja na nasema eneo hilo ndilo eneo la msingi ambalo sasa hivi tunatakiwa kulitazama vizuri. Asilimia 20 ya Vyuo Vikuu katika nchi yetu, ni vyuo vikuu vinavyomilikiwa na Serikali, asilimia 80 ya Vyuo Vikuu vilivyobaki ni vyuo vikuu binafsi, lakini vyuo vikuu hivi vyote vinapokea fedha kutoka katika Serikali yetu ili kwenda kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa, kumekuwa na tatizo kubwa sana la watoto wa Kitanzania, wakiwemo watoto wa Jimbo la Peramiho, wakiwemo watoto wa Jimbo la kule Ludewa kwa Mheshimiwa Deo Filikunjombe, wakiwemo watoto wa maeneo na Majimbo mengine mengi. Shida ya upatikanaji wa mikopo, Serikali inajitahidi kutoa fedha kwa kiasi cha kutosha kadri ilivyojipanga.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kabla hujavunja ile Kamati kwa mujibu wa Kanuni, hujafanya mabadiliko ya Kamati ile iliyokuwa inakagua mahesabu ya Mashirika ya Umma, Chuo Kikuu cha Mkwawa kilipokaguliwa na kwenda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

mbele ya ile Kamati, ilionekana kabisa kwamba, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo, inatimiza wajibu wa kupeleka fedha kwenye Chuo Kikuu kile kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi, lakini fedha zile zinatumiwa ndivyo sivyote! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, iligundulika kabisa kwamba, kuna wanafunzi hewa wamepeleka ile mikopo na wanafunzi wengine ambao wanatakiwa kupata mikopo wamenyimwa, lakini fedha zile zimefujwa kwa makusudi mazima kwa ujanja ujanja tu pale kwenye kile Chuo Kikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa shida iliyopo hapa na ninayoiona, ni kweli leo Sheria hii inaleta mabadiliko na kuitaka Bodi ya Mikopo kupata taarifa kutoka katika vyuo vikuu ni namna gani wanufaika wamenufaika, lakini kifungu hiki hakielezi na mpaka sasa kifungu hiki hakimpi nguvu Mkaguzi Mkuu na Mdhambi wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kukagua fedha hii na hasa inapopeleka kwenye hivi vyuo binafsi.

Mheshimiwa Spika, kama asilimia 80 ya Vyuo Vikuu Tanzania vinamilikiwa na Taasisi binafsi na asilimia 20 vinamilikiwa na Serikali na kama tumeshapata mfano mmoja wa Chuo Kikuu ambacho kinakaguliwa na kinamilikiwa na Serikali, lakini kuna ufujaji. Fedha za mikopo ya wanafunzi zinawekwa kwenye *deposit account* kuwanufaisha watu wachache watoto wanakosa mikopo; fedha za mikopo ya wanafunzi zinapewa majina ya wanafunzi hewa, je, huku kwenye asilimia 80 hali ikoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ikoje huko kwenye asilimia 80 na kama watoto wa Tanzania ni asilimia 20 tu ndiyo wako huku kwenye Vyuo Vikuu vya asilimia 20, ina maana wanafunzi wetu wengi wako huku kwenye asilimia 80 na wengi ndiyo wanahangaika hiyo mikopo hawajapata, hali ikoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba AG, hapa jioni wakati wa Sheria hii, tufanye mabadiliko hapa, CAG apewe nguvu,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

pamoja na kupokea taarifa ya wanufaika, akakague haya mahesabu huko kama kweli wanafunzi wetu, watoto wetu hawa wa wakulima wanaohangaika na mikopo, kama kweli wanapata fedha hizi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, watoto hawa wanakwenda kwenye Vyuo Vikuu, hawana fedha ya chakula, hawana fedha ya kulipia maradhi, lakini wako kwenye mikopo, fedha hawapati. Matokeo yake wanaandamana, wakiandamana kuna watu wanakwenda kuwaunga mkono. Wanapoteza muda wa kusoma, lakini ukienda kukagua hapa siri hii inaweza ikafanikiwa. Naomba sana AG, atakapokuja hapa leo mchana, naomba kifungu hiki, kimpe nguvu Mkaguzi wetu CAG akague, akague fedha hizo zinazokwenda kwenye hiyo asilimia 20, lakini pia zinazokwenda kwenye asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, lengo hapa la Muswada huu leo, ni kuhakikisha tunaboresha muundo na utaratibu mzuri wa kuhakikisha watoto wa Kitanzania hata kwa kile kidogo kinachopelekwa na Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, kinawafikia na lazima hapa tuishukuru sana Serikali yetu kwa wingi wa wanafunzi, lakini bado imeendelea kuhangaika kutafuta mikopo kuwasaidia wanafunzi hawa. Kwa hiyo, kwa kweli suala hili ni suala la msingi, kuona ni namna gani matumizi bora kwa muundo huu tunaotengeneza leo, unawafikia walengwa kwa wakati maalum, lakini fedha zinazopangwa zinatumiwa kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niungane na hii Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri, naungana nao mkono katika eneo lifuatalo, ni kweli kabisa, fedha za Mfuko wa Elimu kuziacha zikaboreshe elimu ya juu tu, tukaacha kuboresha elimu ya msingi, ya sekondari, hapo tutakuwa hatujitendei haki.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sasa hivi, mimi natembelea sana Sekondari zangu kwenye Jimbo la Peramiho. Kuna siku nimefika Sekondari moja watoto wa Shule ile, wananiambia, Mheshimiwa Mbunge, tunatamani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

Sekondari hii ingefanana na Shule yetu ya Msingi fulani. Ina maana wanaona mazingira ya Sekondari yao bado hayako vizuri. Sasa hapa tunasema fedha asilimia 50 zitakwenda kuboresha Miundombinu ya Vyuu Vikuu.

Mheshimiwa Spika, tuangalie na miundombinu ya shule za msingi, za sekondari, hapo tutakuwa tumefanya vizuri. Tukiwaandaa watoto wa Kitanzania vizuri kwenye msingi na kwenye sekondari, wakifika chuo kikuu watafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Magazeti na hii ya Filamu, nataka kusema kitu kimoja, Serikali yangu tulateeni hapa Muswada, Kamati ya Maendeleo ya Jamii imelia na Serikali kila siku, haya yote mnayoyasikia humu hayatakuwepo. Tunakawia nini kuleta Muswada wa kuhakikisha tunatengeneza Sheria ya kusimamia vyombo vya habari? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunachelewa nini, wadau wa vyombo vya habari, wenyewe wale wenye maadili mema, wamelia kila siku wanataka Sheria hii iwepo na wanajua Sheria hii ikishatungwa, itasaidia. Siku hizi kumekuwa na lugha inaita baadhi ya waandishi wa habari makanjanja, tena nadhani sasa hivi afadhali inaanza kufa. Tunadhalilisha hii tasnia, kuna watu wanadhalilisha tasnia ya habari bila sababu ya msingi, tunachelewa nini Serikali kuleta Muswada huu. (*Makofi*)

Tulateeni Muswada, tukae na wadau, tukubaliane mambo ya msingi, tuwe na Sheria itakayolinda tasnia ya habari katika nchi yetu ya Tanzania. Sioni kwa kweli kila siku tunarekebisha rekebisha tu hapa, Sheria nzima iko hatutaki kuifanyia utaratibu mzuri, tunakawia nini. Wadau wote wako tayari, Kamati ya Maendeleo ya Jamii imesema kila siku iko tayari. Tunakawia nini, AG tulateeni huo Muswada.

Mheshimiwa Spika, tukishapata huo Muswada, tutaelewa ni namna gani tasnia hii muhimu ya habari katika nchi yetu ifanye kazi kwa kuzingatia weledi unaotakiwa. Huo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

ndio ukombozi pekee, lakini ukombozi wa kila siku tunabishana, tunatumia masaa hapa, tunazungumza, watu wanaendelea kuumia, wanaendelea kuteseka. Akina Pindi Chana humu wanauliza maswali, anajibu nani? Majibu yako katika Sheria ambayo itatungwa na Bunge hili na iletwe Sheria hiyo itungwe ili kusimamia weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na haya mambo mengine yanayosemwa, wote ni mashahidi, ziko filamu nyingine katika nchi yetu zinakiuka maadili ya Kitanzania kwa kiasi kikubwa tu, maadili yanapotoshwa, weledi wa Watanzania na utamaduni wetu unapotoshwa, hakuna mtu hata anayeshtuka kama hilo nalo ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema kwamba, kwenye mabadiliko ya Sheria naunga mkono, kwenye mabadiliko ya Sheria hii ya tasnia ya habari, naiomba Serikali ilete Muswada, uletwe Bungeni, tujadiliane hapa, tushauriane na wadau, tutengeneze Sheria itakayolinda amani ya nchi yetu, itakayoboresha weledi wa tasnia ya habari na itakayowasaidia Watanzania kupata habari katika viwango vya Kimataifa vinavyotakiwa kwa sasa, vinginevyo hatutakuwa na uelekeo unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja hii na naipongeza Serikali na Kamati kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea mchana, napenda kuwataja, lakini kwa nini msije wote niwataje mkiwepo? Mnataka waje tu waliotajwa, mje nitawataja. Tutaendelea na Muswada mchana, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 6.55 mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi cha asubuhi, kabla hatujaahirisha. Nilikuwa nimemtaja Profesa Msolwa, lakini ikawa muda hautoshi. Sasa nitamwita Mheshimiwa Profesa Msolla atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali (Na 3) wa mwaka 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue vile vile nafasi kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge iliyochambua Muswada huu kwa undani na kutoa mapendekezo ambayo ni muafaka kabisa, kwa kufanya kazi hii nzuri. Binafsi ningelipenda kujikita sana katika eneo la Mikopo ya Wanafunzi kwa sababu kumekuwa na matatizo mengi sana, naona hii ni fursa ya kuweza kutoa maoni yangu, juu ya eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali, kwanza kwa kuongeza fedha za mikopo kwa ajili ya wanafunzi na kwamba idadi ya wanafunzi wanaopata mikopo sasa imeongezeka, japokuwa bado kuna kilio kikubwa. Naipongeza kwa sababu kuwekeza katika elimu, ni kwamba tunawawekea urithi mkubwa na wa uhakika vijana wetu. Wazungu wanasema *invest in human brain*, ni bora zaidi kuliko kitu kingine chochote, ambako tunaweza kuwa tunawekeza.

Mheshimiwa Spika, leo sisi ni mashahidi, tunaona kwa kila kazi ya kitaalam, ama ya kitaaluma, tunapata watu hata Wakandarasi tu wa ujenzi wa barabara, madaraja, tunawapata watu kutoka nje ikionesha kwamba sisi wenyewe, hatujafikia viwango hivyo vya kuwapata wataalam wa kutosha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P. M. MSOLLA]

Mheshimiwa Spika, nimesema tatizo la mikopo ni kubwa kwa sababu siyo wanafunzi wote wanaokidhi vigezo wanapata mikopo hiyo. Wengi wao wanaokidhi vigezo vya kupata mikopo hawapati mikopo. Mathalani kwa mwaka huu wa masomo wa 2013/2014, wanafunzi waliokuwa wameomba mikopo walikuwa ni 42,487.

Mheshimiwa Spika, waliokidhi vigezo walikuwa ni wanafunzi 38,376. Waliokata mikopo katika ngazi mbalimbali walikuwa ni 34,538, waliokosa walikuwa ni 4,838. Sasa wastani wa mikopo kwa mwanafunzi bila kujali kama anachukua masomo ya Sayansi, ama masomo mengine ya sanaa, ni sh. 4,000,000/= Kwa idadi hii ya wanafunzi 4,838 mahitaji ambayo yanahitajika kwa sasa ni shilingi bilioni 19.3.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinaweza kuonekana ni nyingi, lakini kama tunaweza kwenye elimu, nina hakika ingekuwa na manufaa makubwa zaidi, kuliko kuwaacha vijana wengi namna hii na kila mwaka wanaongezeka wanakosa mikopo na wanabakia nje. Ningeishauri Serikali iweke mikakati ya kuona namna gani fedha za namba hiyo zinaweza zikapatikana ili vijana wetu walio wengi waweze kunufaika na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, siyo siri katika eneo hili la *Africa South of Sahara*. Kwa muda mrefu, Tanzania ilikuwa ndiyo ya mwisho kwa maana ya wale wanafunzi waliokuwa na umri wa kwenda Vyuho Vikuu, Tanzania tulikuwa wa mwisho. Hivi majuzi tu kutoka chini tumekuwa wa tatu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwekeza zaidi katika elimu ili kusudi tuweze kuwa na vijana wengi na hii ndiyo njia peke yake vile vile ya kujiondoa katika hilo lindi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na mgawanyo uliopendekeza juu ya fedha kwenda katika ngazi mbalimbali za elimu, lakini ambacho naona kwamba hakijakaa vizuri ni namna zile fedha zitakavyomfikia mwanafunzi, kwamba fedha zinaanzwa kukusanywa huko na *TRA*, zinakwenda Hazina. Kutoka Hazina ziende Wizara ya Elimu, kutoka Wizara ya Elimu ziende kwenye Mfuko wa Elimu, kutoka Mfuko wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P. M. MSOLLA]

Elimu ziende kwenye Bodi ya Mikopo, kutoka Bodi ya Mikopo ziende kwenye Chuo na kutoka Chuoni ndiyo iende kwa Mwanafunzi, ni mlolongo mrefu sana. Hii inawachelewesha wanafunzi mara nyingi hata wanapokwenda shuleni kwa muhula wa kwanza, wanashauriwa kabisa waende na fedha za kwao, kwa kujikimu kwa sababu fedha hizo zitakuwa hazijafika.

Sasa kwa kupitia njia hii, ni kwamba tunahalalisha urasimu huo na wanafunzi wengi wataendelea kupata fedha zao na badala ya kuendelea na masomo wataendelea kuhangaika kwa namna ya kujikimu. Hivyo hivyo, fedha zile ambazo zinatoka kwenye *Skills Development Levy*, ambazo nazo zamani zilikuwa zinakwenda moja kwa moja kwenye Bodi ya Mikopo. Halafu Bodi ya Mikopo ndiyo inatoa fedha hizo kwa wanafunzi, nazo vile vile zinaambiwa zipitie kwenye Mfuko wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, ningepomba sana, Serikali iangalie uwezekano wa kufupisha hii njia. Kwa sababu ni njia nyingi mno na lazima kutakuwa na ucheleweshaji. Mara nyingine unaweza kukuta mtu anayehusika hayuko pale. Nashauri kwa njia zote mbili, iwe fedha za mikopo, iwe zinazotoka *Skills Development Levy* ziweze kupelekwa kwenye Bodi ya Mikopo moja kwa moja, wameshakuwa na uzoefu mkubwa ili kusudi wapeleke fedha hizo kwa wanafunzi kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna uwakilishi wa wanafunzi kwenye Bodi ya Mikopo. Kipengele cha kuwapeleka wanafunzi wawili kiliwekwa kwa makusudi, kwa sababu kuna Vyuo Vikuu vya Umma na Vyuo Vikuu vya Binafsi. Mahitaji ya sehemu hizi mbili ni tofauti. Sasa leo hii kuweka mwanafunzi mmoja halafu pale akaingia mtu anayetoka kwenye Mfuko wa Elimu, kidogo haipendezi.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri ili kusiwe na malamiko, mwanafunzi mmoja atoke kwenye Vyuo Vikuu Binafsi na mwingine atoke kwenye Vyuo Vikuu vya Umma, kwa utaratibu uliokuwepo. Kama kuna ulazima wa huyu Mwakilishi kutoka kwenye Mfuko wa Elimu, basi idadi hiyo iongezwe ama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P. M. MSOLLA]

awe kama *Observer whatever be the case*, lakini kuwakatalia kabisa hawa, kidogo haitapendeza hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya ambayo nimeyatoa, naipongeza Serikali kwamba, sehemu ya fedha hizi zitakwenda katika kuboresha miundombinu ya elimu. Nami nasema katika miundombinu ya elimu, tuweke mkazo mkubwa katika miundombinu ya masomo ya hisabati na sayansi kwa sababu, kwa sasa hivi vijana wanaochukua masomo ya sayansi ni wachache sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile kumekuwa na upungufu hata wa Walimu wa Sayansi. Ili kusudi tuweze kwenda mbele, ni vema tukawa na miundombinu mizuri angalau hatua kwa hatua ili hatimaye tuweze kuwa na vijana ambao wanapenda masomo ya sayansi, kwa sababu wengine wamekosa kuwa na upendo wa masomo hayo kwa sababu wanakosa Walimu. Tuanze na Walimu tujenge miundombinu na hatimaye tutapata vijana wengi ili baadaye tupate *a critical mass of scientists* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada wa Sheria Mbalimbali katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, ningependa nianze kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo langu, katika Kata ya Kamsamba, Kijiji cha Senga, Kitongoji cha Mchangani, ambao walikumbwa na dhahama ya kuchomewa nyumba zao. Nyumba 392, zilichomwa moto na mimi mwenye ni shuhuda, nilikwenda kushuhudia siku ya Jumapili, maduka, Makanisa mawili; Kanisa la Katoliki, pamoja na Kanisa la *Free Pentekoste*; vyakula vyote, malazi, pikipiki na kila kitu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Spika, kwa kweli inasikitisha sana ile *operation*, ukienda kuwaona wale watu. Nawapa pole kwa kuendelea kuishi porini, kwa sababu mpaka sasa hivi hakuna msaada wote ambao wameupata. Nimewasiliana na Waziri Mkuu, pamoja na Mheshimiwa Lukuvi, wajaribu kupeleka msaada wa haraka. Kwa sababu tukisema tuendeleo kusubiri majibu ya Tume ambayo bado haijaundwa, maana yake wale watu wataendelea kuteseka na msimu wa mvua umeanza.

Mheshimiwa Spika, hayo siyo tu yaliyotokea katika Jimbo langu, bali hata katika Majimbo mengine. Kwa hiyo, tungependa wapeleke msaada wa haraka wa chakula, pamoja na malazi. Kama hiyo haitoshi, ni vizuri Serikali ikatambua kwamba, wanapofanya *operation* kama hizi, wasiwe wanavamia wananchi. Hii ni nchi yetu, hatuvamii Watanzania ama wananchi wenzetu kama watu wengine. Kwa hiyo, naamini hatua za haraka kabla Tume yako haijaanza kufanya kazi, itachukua hatua mara moja kupeleka hiyo misaada ya kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, kwenye Muswada huu, nataka kuchangia katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178. Ukipitia mapendekezo; jumla ya mapendekezo yote kwa lugha moja ama nyingine siyo mabaya, lakini kigumu ambacho siku zote tumekuwa tukitofautiana, ni namna ya utekelezaji wa haya ambayo yameainishwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (7) kwenye Sura ya 178, kinataka kuongeza idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Mikopo. Ukiangalia tu katika hali ya kawaida ni kwamba, hakuna shida, lakini shida yetu sisi kama Taifa, siyo kuongeza idadi ya Wajumbe, shida yetu ni kuwa na mfumo bora ambao utasaidia Bodi ya Mikopo na elimu ya juu kwa ujumla wake. Sasa tunafikiri siku zote kwamba, idadi ndiyo kigezo pekee, ambacho kinaweza kusaidia kutatua haya matatizo yaliyokuwa yameelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyoh ningeimba Serikali, siyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. E. SILINDE]

tu waje na idadi, watueleze na namna ambavyo tumekuwa tukipendekeza kui-*structure* upya Bodi ya Mikopo na hicho ndiyo kimekuwa kilio, lakini kama haitoshi, kulikuwa na Tume iliyounda, Tume ya Profesa Maboko, ambayo ilikuwa inafuatilia migogoro inayotokana na Mikopo ya Vyuu Vikuu, mpaka leo hii hatujapata taarifa yake, tujue ni nini kilikuwa ni chanzo, ili sisi tuweze kuishauri Serikali vizuri, iweze kuondokana na haya majanga ambayo kila siku yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kifungu kingine ambacho kinatakiwa kifanyiwe marekebisho kwenye Sheria yetu, ni kifungu cha 20. Kwenye kifungu cha Ishirini, kinataka ama kinaiongezea nguvu Bodi kumkamata mtu yeyote aliyepewa mkopo ambaye ameshindwa, kulipa asilimia (8%) ya mshahara wake.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine tuwe wakweli. Watu wote wanaojiriwa nchi hii, miongoni mwa malalamiko makubwa ambayo yamekuwa yakitoka, ni kwamba, mishahara ni midogo hususan wale wanaojiriwa katika sekta ya Serikali, kwa maana Serikalini. Sasa hili limekuwa ni tatizo. Sasa leo tunataka Sheria sasa iwakamate na walipe asilimia nane ya mshahara. Sidhani kama tutakuwa tunawatendea haki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama ingekuwa ni mapendekezo, basi angalau hata hii asilimia nane tui punguze, kwamba angalau walipishwe hata asilimia mbili. Nasema hivyo kwa sababu moja, Sheria yetu kwa wanafunzi wote wanaomaliza *Higher Learning Institution*, zote hizi kuajiriwa siku hizi imekuwa ni kazi. Kumpata mtu aliyeajiriwa kutoka moja kwa moja shuleni, ni kazi.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tunao wenzetu tuliomaliza nao Vyuu mwaka 2010, lakini hawana ajira, wamekuwa wakilalamika. Sasa huyu mtu baadaye mtamkamata kwa sababu anashindwa kulipa na wengine sidhani kama watakuja kuajiriwa katika sekta rasmi ama isiyo rasmi, katika kipindi chote cha maisha yao, maana yake

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. E. SILINDE]

wengine itabidi wajajiri na ni vigumu kuwapata kwa sababu ajira zenyewe hazieleweki.

Mheshimiwa Spika, nafikiri, Serikali ilikuwa ina haja ya kutafakari upya. Mnaweza kukamata baadhi ya watu, lakini mjue kabisa, miongoni mwa mateso ambayo wanafunzi waliyapata ni namna ya kupata huu mkopo. Sasa hata kulipa na yenyewe wanalipa kwa shida. Kwa hiyo, itakuwa ni jamii wa Watanzania inayoteseka na ni jamii ambayo tunasema Serikali yake haiwajali wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, cha mwisho, lazima mjue kabisa, mishahara inayolipwa Serekalini tunaita kwamba ni *daily living salaries*, yaani ni mishahara ambao unaishi kuanzia tarehe moja ya mwanzo wa mwezi mpaka tarehe 30, baada hapo huna chochote cha ku-save. Kwa hiyo, Mtanzania anageuka kuwa mtumwa maisha yake yote mpaka siku anazeeka, ndiyo maana wengi wakishazeeka ama wakishastaafu kazini, wanakuwa hawana chochote kilichobakia zaidi tu ya kujilaumu katika maisha yao yote.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu kingine, Sheria inapendekeza kuwepo na vyanzo vingine vya mapato, naliunga mkono. Sheria inataka angalau tuwe na asilima mbili ya *Recurrent Budget* ambayo tunaipitisha. Ningependekeza isiwe asilimia mbili tu, iwe angalau asilimia tano kwa sababu nchi zote duniani, elimu ndiyo kipaumbele nambari moja. Ukienda Kenya, ukienda Marekani, hata huko Malaysia ambako sisi sasa hivi ndiyo tume-*adopt* hii Sera ya *Big Result Now*, kipaumbele chao kabla hawajaendelea kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1981, wao elimu ndiyo ilikuwa kipaumbele na walifanya nini kuhusu masuala ya elimu. Wao cha kwanza siyo tu waliamua kusomesha wananchi ndani ya nchi yao, walichukua wanafunzi wale wanaomaliza Kidaato cha Sita, wanakwenda kusoma nchi za nje, yaani kwa maana ya kwamba, wengine walikuwa wanakwenda Marekani, wengine Ujerumani na wengine China.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, walikuwa kila mwaka wanapeleka wanafunzi siyo chini ya 10,000. Kwa miaka 20, wana-*graduates* kutoka nje ya nchi 200,000. Kwa hiyo, wale watu wote waliporudi nchini, leo hii ndiyo maana unaona Malaysia iko pale, kwa sababu watalaam wanatoka kutoka China, wanarudi nchini kwao.

Mheshimiwa Spika, *BRN* ndani ya nchi hii itakuwa ni ndoto, kwa sababu Walimu waliofundisha watoto waliofeli ndiyo mlolongo ule ule unakwenda mpaka *University*, ni vigumu. Kwa hiyo, ningependa hapa Serikali sasa iwekeze zaidi kupeleka wanafunzi nje ya nchi, siyo kuendelea kung'ang'ania vyo vya ndani. Maana yake dunia ili iweze kuendelea, lazima mwananchi apate *exposure*, bila *exposure* huwezi kufanya kitu chochote katika dunia hii, kwa sababu mtazamo wako utabaki pale pale. Unafikiri maendeleo ni kuwa na fedha kama Rostam Aziz, hiyo ndiyo *thinking* yako, hapana, utoke nje ya hapo. Sasa ni vizuri dhana hii tukaiondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, iwe wazi kwamba *BRN* yetu, kwenye masuala ya elimu lazima iwe ni *long term*. Isiwe katika *short term* kama tunavyofikiria, kwamba ndani ya miezi nne, ndiyo yanakuja haya matokeo kwamba katika kipindi cha miezi minne twende na *Division Five (5)* na vitu vingine. Twende katika *long term planning* ambayo kwenye sekta ya elimu inawezekana, ila kwenye mambo ya maji mambo ya *BRN* yanawezekana ndani ya dakika moja.

Mheshimiwa Spika, ukiwa na hela ukisema uchimbe kisima kesho kitatoa maji. Ukiwa na hela ukisema ujenge barabara, barabara itaonekana. Ukiwa na hela ukisema unataka kujenga hospitali, itaonekana. Hiyo *BRN* kwenye mambo yanayoonekana inawezekana, lakini kwenye mchakato wa elimu, ni vigumu. Kwa sababu elimu *is a process*; kumtoa mwanafunzi kutoka zero, haelewi, mpaka kumfikisha kuwa Profesa, *it takes years*, siyo kama ambavyo sasa hivi tunakwenda. Kwa hiyo, hili naomba lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, mfumo ambao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. E. SILINDE]

unakwenda kutumika, mfumo wa fedha. Malalamiko ya wanafunzi ni mikopo kushindwa kufika kwa wakati. Leo hii tumeongeza, kwamba sasa itakwenda katika Mfuko wa Elimu, ambao ndiyo utakaosimamia fedha zote.

Mheshimiwa Spika, sasa tuulizane. Mfuko wa Elimu kwa maana ya *Education Fund* ulikuwepo, tuambiwe ulifanya kazi kwa kiwango gani, *assurance*, katika kipindi cha nyuma ambao ulikuwa ni *Education Fund*, uhakika wake, uwezo wake au ubora wake ulikuwa kwa kiwango gani mpaka sasa tuwape jukumu la kusimamia hizi fedha ambazo zimeshindikana katika kipindi hiki chote ambacho kimekuwa kikipelekea wananchi kugombana kila siku.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa, ningependa Serikali tujaribu kupitia upya Sheria ya Magazeti, lakini kwenye kupitia upya sheria tusiongeze kubana. Tunatakiwa tuelimishe watu namna ya kutoa taarifa nzuri ama habari nzuri, tofauti na sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kueleza ni kwamba jamani, leo unaweza wewe kama mtawala ukaona hii sheria inabana watu wengine, lakini kesho wewe utakuwa upande wa upinzani, ama utakuwa mfuasi. Maana yake moja ya sifa ya kiongozi ni lazima ukubali, leo mimi ni kiongozi, kesho nitakubali kuwa raia kuongozwa na Mbunge mwingine. Maana yake tusije kuwa kama wale Wabunge wengine, ukishindwa unakwenda Mahakamani. Lazima ujue siku nyingine nitakuwa mfuasi. Sasa leo wewe ni mtawala, kesho utakuwa mfuasi.

Mheshimiwa Spika, Sheria zote zilizotungwa na watawala tangu wapate uhuru, ndizo zilizotumika kuwanyonga wao wenyewe. Kwa hiyo, msiwe na hiyo tunasema *myopia thinking*, kwamba mtazamo wako ni miaka hii miwili ya leo, lakini miaka mitano ijayo huoni. Hii ndiyo itakayokuja kuwagharimu, kwa hiyo tujaribu kuangalia hayo. Turuhusu uhuru wa magazeti, magazeti yatoe taarifa, lakini tusiwa *-limit* katika kila jambo. Kiukweli jamani, ukweli siku zote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. E. SILINDE]

ni uchochezi. Maana yake mtu yeyote anayesema ukweli, ni uchochozei na ukweli ni mgogoro.

Mheshimiwa Spika, moja ya vitu vibaya sana ambavyo Serikali wamekuwa wanafikiri ni kuwa, taarifa zinazotajwa kwenye magazeti ni uchochezi, siyo uchochezi, tunahitaji watu kufahamu. Ndiyo maana nimetolea mfano wananchi Jimboni kwangu, makazi 392 yamechomwa moto. Hakuna taarifa kwenye vyombo vya habari vilivyo-*cover* hizi taarifa kwa sababu wametishiwa wasioneshe, kwa sababu ni ukweli utakaochochea uasi kwa Serikali. Lakini muda mwingine inabidi iwe hivyo ili Serikali iweze kujifunza, msipofanya hivyo mtakwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwisho kabisa, Serikali nyinyi wote mmesoma kitabu cha *Rich Daddy, Poor Daddy*. Tuwe *a rich Daddy, to-think big*, maana yake Serikali siku zote imekuwa iki-*think* katika *Poor Daddy*. Kila kitu hakiwezekani, hatuwezi kwenda kwa mfumo huo na ndiyo maana hii Serikali inalegalega.

Mheshimiwa Spika, ukiwaaambia lipa mikopo kwa asilimia mia moja, watu wanasema hiyo haiwezekani, *that is a thinking of poor daddy, rich daddy* anasema itawezekana, tutaangalia namna kama tutachukua fedha kutoka katika Makampuni ya Madini au tutachukua fedha katika *resources* nyingine kwa maana ya Maliasili. Maana yake nguvu tunayowekeza kwenye madini, tukiwekeza hiyo hiyo katika maliasili, naamini nchi hii, itabadilika na tutafika kule tukakokwenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu siku ya leo. Kwanza kabisa, naomba ni-*declare interest* kwamba ni Mwandishi wa Habari. Niliweza kufanya kazi katika Magazeti ya Chama ya Uhuru na Mzalendo kabla sijawa Mbunge. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. E. A. BULAYA]

Mheshimiwa Spika, natambua mchango wa Waandishi wa Habari katika Taifa hili kwa sababu bila wao hata hizi habari ambazo sisi tuko humu leo hii, zisingeweza kurushwa na wananchi wakaelewa. Vile vile natambua kwamba, kuna baadhi ya Waandishi wa habari wanakiuka *ethics* za uandishi wa habari, nalitambua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Jenista Mhagama, nilimsikiliza kwa makini. Tukitaka tutatue yote haya tuulete ule Muswada wa Habari kwa sababu tunaweza tukaleta sheria hapa zikatengeneza mazingira ambayo yanaonekana ni ya uonevu. Ie sheria ya Habari itaweka misingi ya jinsi gani Mwandishi wa Habari anapaswa kufuata *ethics* zake.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa upande mwingine italinda uhuru wa Mwandishi wa Habari kupata habari. Hapo tutakuwa tume-*balance*. Sasa hivi vifungu vilivyopo hapa vinaonesha kabisa vinataka kuegemea upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali tufanye hima tulete Muswada wa Habari ili tuweze kutatua tatizo hili. Hapa ndipo tutakapowabana vizuri na hapa ndipo tutakapopembua pumba na mchele, kuliko hivi ilivyo sasa. Napenda ku-*quote* sana msemo wa Baba yangu Mwanasheria Mkuu, namheshimu sana kwamba tusitunge sheria zenye hasira. Sasa hapa ilikuwa inaonesha faini kama sikosei shilingi 15,000/= kutoka kiwango hicho mpaka shilingi 5,000,000/= na kama sikosei hapa inawagusa waandishi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli siyo Waandishi wote wameajiriwa, wengi ni *correspondent* ambako na mimi nilianzia huko. Wangapi ambao wana uwezo wa kulipa faini hii. Ninavyosema hivi siyo kwamba, nakubali habari za uchochezi, hapana, lakini kiwango hiki ni kikubwa mno. Kwa hiyo, kuna haja kabisa ya Serikali kukaa tuulete ule Muswada

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. E. A. BULAYA]

ili tuweze kulinda pande zote mbili, kwa sababu hata kuna *source* wengine wagumu kutoa habari. Mwandishi wa Habari anashidwa ku-*balance*, lakini habari ikitoka analalamika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili ku-*balance* pande zote mbili, lazima ule Muswada uje, tuweke ni jinsi gani ambavyo tutaweka utaratibu wa kuwabana Waandishi, lakini na wao kuwaweezesha kupata habari kwa uhuru.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kumuunga mkono Baba yangu Mzee Msolla pale, alipokuwa akizungumzia katika Sheria ya Bodi ya Mikopo. Mwanzo ikuwa imekaa vizuri, lakini sasa huu utaratibu ambao umeletwa ndiyo unaotuletea matatizo. Mlolongo unakuwa mrefu, fedha zitoke Hazina, ziende sijui Mfuko wa Elimu na wengine wanatoa hapo wanapeleka *Bank* ili wapate *interest* huku wanafunzi wanaendelea kuhangaika mtaani. Inaondoa dhana ya nia njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kuwapatia wanafunzi mikopo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme, huu utaratibu hautufikishi popote. Utaendelea kuwatesa vijana wenzangu wa elimu ya juu, na malalamiko na matatizo ya wanafunzi wa vyuo vikuu hayatakwisha. Kwa hiyo, naiomba Serikali suala hili, ilianganalie kwa kina.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hapo hapo, kuhusiana na uteuzi wa Wajumbe katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hili jina tu lenyewe, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, leo hii tunaleta marekebisho ya kupunguza wigo wa ushiriki wa wanafunzi. Sasa hivi tunataka Mwanafunzi mmoja, mwanzo ilikuwa inatoa mwanya kwa wanafunzi wawili. Kama tunavyojua, vyuo vya elimu ya juu, binafsi ni asilimia 80, leo hii tunatoa uwakilishi wao kwenye Bodi, kwa kweli hatutawatendea haki.

Mheshimiwa Spika, hata huo uwakilishi wa watu wawili ni mdogo sana, kwa sababu hii *Board* inawahusu wanafunzi wa elimu ya juu, wanatakiwa wawe na uwakilishi wa kutosha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. E. A. BULAYA]

Pia nataka kuuliza tuko katika Serikali ya Muungano, sijui katika upande wa Zanzibar umezingatiwaje? Hilo lenyewe ni jambo la msingi, naamini Mwanasheria Mkuu atanipa majibu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, pia nizingumzie kipengele cha filamu, ni kweli kuna filamu nyingine ambazo zipo kinyume na taratibu zetu, lakini je, Serikali mmejipanga vipi kuhakikisha mnatuletea Muswada wa kulinda kazi za wasanii, wa kulinda kazi za filamu za wasanii wetu. Wakati huu tukiwa tunahakikisha hawakiuki maadili, pia tutengeneze utaratibu wa kuhakikisha wanafaidika na kazi wanazozifanya. Hilo ni jambo la msingi sana!

Mheshimiwa Spika, kuna wengine wanatoa filamu nzuri tu zinaelimisha, wakati tunaleta sheria hizi pia tuangalie na upande wa pili. Sasa hivi filamu ni ajira na pia sana ni ajira, tunaweka utaratibu gani? Tunaleta sheria gani za kuhakikisha hawaibiwi kazi zao na wananufaika na kazi wanazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kipengele kingine ambacho napenda kukizungumzia ni kifungu cha 45, lakini sina uhakika kama kimefutwa, ni kuhusiana na kinga kwa Wakurugenzi na Wajumbe wa Bodi pindi wanapofanya maamuzi kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu asiyejua kuna *lobbying* za ajabu kama maeneo haya ya Bodi. Siamini kwamba kama mtu ambaye yuko *committed* ataacha kufanya *research* ya kutosha na kutoa maamuzi sahihi kwa maslahi ya Taifa lake. Tukiacha sheria hii ya kuwalinda watu kwa kweli hatutalitendea haki Taifa letu, ndiyo tutaendelea kupokea ndege ambazo zinakuja hazijaruka mbovu. Hiki kifungu pia na chenyewe nadhani kiangaliwe kwa umakini wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja, lakini mapendekezo haya yote yafanyiwe kazi kwani ni ya msingi kwa mustakabali wa Taifa letu. Ahsante. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Margaret Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Mustapha Akunaay.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Pia niipongeze Serikali na hasa kwa kuja na marekebisho yanayohusu Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika changamoto tunazoziona katika suala zima la elimu nchini, mojawapo ni ukosekanaji wa fedha au malipo ya wanafunzi wanapotaka kujiunga na elimu ya juu. Sisi Kamati ya Huduma za Jamii tumekuwa tukipata makundi makubwa ya vijana wakija kutuona ili tuwasaidie Serikali iwape mikopo ili waendeleo na mafunzo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, kwa kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu; juzi Kamati ya Huduma za Jamii iliwashauri Serikali na wakaweza kutafuta utaratibu ambao utawawezesha wanafunzi 1,000 zaidi ili waendeleo na mafunzo ya elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati huo huo naomba tumpongeze Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ambaye yeye hoja yake binafsi imesaidia sana Serikali kuleta marekebisho ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mapendekezo yangu katika kufanya marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kwanza kabisa kama mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge, asili ya kuwepo kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni kuwasaidia vijana wanaotoka katika familia duni. Kwa hiyo, napendekeza sababu iliyokuwa ya msingi isiachwe, ioneshwe wazi katika sheria hii kwamba walengwa wakubwa ni vijana wanaotoka katika familia duni ili tuisahau asili ya kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo, sheria itamke wazi kwamba walengwa ni vijana wanaotoka katika familia duni.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. S. SITTA]

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuipongeza Serikali kwa pendekezo lake la kutenga 64% ya fedha kupelekwa Bodi ya Mikopo, lakini shida inakuja, katika sheria haikuonesha wazi kwamba hiyo 64% itakayopelekwa kwenye Bodi ya Mikopo itatumikaje, sasa tuna wasiwasi kwamba inaweza ikabadilishwa madhumuni yake. Kwa hiyo, napendekeza kwamba ile 64% inayopendekezwa katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ioneshe wazi mgawanyo wa matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo napendekeza kwamba katika hiyo 64% itakayopelekwa katika Bodi ya Mikopo, basi 60% ya 64% inayopelekwa kwenye Bodi ya Mikopo iwalenge vijana wanaotoka katika familia duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiangalia katika marekebisho yaliyoletwa katika Sheria ya Bodi ya Mikopo hajatoa fasili ya mwanafunzi mhitaji anayetoka katika familia duni. Kwa hiyo, napendekeza kwamba, kuwe na fasili inayoonesha huyu mwanafunzi mhitaji anayetoka katika familia duni ni nani ili alengwe vizuri au aweze kusaidiwa kutokana na fasili itakayotoka katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napendekeza katika kifungu 32(b) kitamke wazi kwamba, mwajiri atapaswa kutoa taarifa ya waajiriwa wake ambao wamekopa ili waweze kurudisha mikopo ile iweze kuwasaidia wengine kwa sababu kukiwa na kipengele kinachombana mwajiri kutoa taarifa ya waajiriwa wake wenye madeni ya mikopo, itakuwa vigumu sana kuwatambua, lakini kukiwa na kipengele kinachombana mwajiri, basi atashiriki vizuri katika kutoa taarifa ya waajiriwa wake ambao wanadaiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa Sheria ya Mfuko wa Elimu, katika kifungu cha 22(b) yawekwe maneno yatakayosaidia kuelekeza vyanzo vya mapato ili viwe wazi kama ilivyo katika Sheria ya VETA, Sheria ya VETA vyanzo vya mapato viko wazi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. S. SITTA]

kabisa. Kukiwa na vyanzo vya mapato vinavyoeleweka basi hata Mfuko wa Elimu nao utaweza kupata fedha kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika Sheria ya Mfuko wa Elimu katika kipengele cha 23 hakijaeleza wazi jinsi gani elimu katika ngazi ya msingi na sekondari itanufaika. Kwa hiyo, napendekeza kwamba maneno *at all levels* yaongezwe katika kifungu cha 23 ili itoe uwezekano wa kusaidia pia elimu ya msingi na sekondari ama sivyo eneo hili ambalo ni la muhimu sana litasahaulika, tutakazania au tutaweka mkazo zaidi katika elimu ya juu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sheria ya Baraza la Taifa la Elimu yaani *NACTE*, vyanzo vya fedha viwekwe wazi kwa sababu tumeona hili nalo ni eneo ambalo litapata 3%, lakini kama vyanzo vya mapato havikuwekwa wazi, *NACTE* haitaweza kupata fedha kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla muda wangu haujakwisha, nataka kutoa wito kwa Watanzania kwamba Serikali ikija na mpango mzuri wa kupata vyanzo vya uhakika vya kuchangia suala la elimu tukubali kwa sababu tunapoguswa tena kuchangia tunakuja juu, lakini ni kawaida yetu sisi Watanzania kuchangia maendeleo ya elimu. Kwa hiyo, nawaomba, kama Serikali itakuja na mpango mzuri wa namna gani wananchi tuchangie elimu kadri ya uwezo wetu, tukubali! Lakini tukiguswa kidogo tu eeeh! Watu wanashangaa, lakini kwenye harusi tunachangia na kadhalika lakini inapokuja suala la elimu, inakuwa ni vigumu.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Watanzania kwamba tuchangie ili mradi Serikali ije na mpango mzuri unaoeleweka na unaozingatia uwezo wa watu, nawaomba sana. La sivyo tukiwa kila wakati tunategemea Serikali tu, bila sisi wenyewe kukubaliana na Serikali pale inapohitajika kuchangia, kwa kweli itakuwa ni vigumu sana kusaidia elimu nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, pia nafikiri kwamba tuipongeze

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. S. SITTA]

Serikali kwa kuja na mpango huu na nawaomba sisi wote tuunge mkono marekebisho ya Sheria yaliyokuja yanayohusu Bodi ya Mfuko wa Elimu, Mfuko wa Elimu na Baraza la Taifa la Elimu, zipite vizuri ili zikaanze kufanya kazi kwa sababu vijana wetu kwa kweli wanateseka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Akunaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah!

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Jambo la kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu za kusimama hapa mbele yako.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na kifungu cha kurekebisha Sheria ya Magazeti na nachukua nafasi fupi kwa kueleza historia yetu ya Sheria ya Magazeti kama ilivyoelezwa na Kambi ya Upinzani kwamba, mwaka 1991 Tume ya Nyalali ilielezea vizuri kwamba, Sheria nzima ya Magazeti inataka iandikwe upya kwani kuna vifungu vingi vinavyokandamiza magazeti na vinavyokandamiza waandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, sasa leo kama kinaletwa kifungu kimoja tu cha kuadhibu mwandishi ambaye ataandika habari za uchochezi, kuongeza adhabu kutoka faini ya sh. 15,000 mpaka miaka mitatu au kutoka sh. 15,000 mpaka miaka milioni tano itakuwa sheria hii haina maana, kwa sababu kwanza uandishi ni fani ambayo ina utaalum na utaalum wowote kawaida unakuwa na Kamati Maalum ya kuangalia utaalum huo yaani nataka kuzungumzia kwamba kila utaalum una *code of conduct*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama habari imeandikwa na ikachapishwa kwenye gazeti inatakiwa ipitiwe kwanza na Council fulani kama hapa Tanzania ni *Media Council* ili kuangalia kwamba habari hiyo inachochea au inaharibu jina la mtu, ndiyo iamuliwe kwamba hiyo ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. B. AKUNAAAY]

kashfa au ni shauri la jinai. Kuufanya uandishi mara moja ni jambo la jinai, hiyo ni kwamba tumekiuka Sheria ya Kimataifa ya Haki ya Mwandishi.

Mheshimiwa Spika, kama Jaji Nyalali alivyosema, sheria hiyo imepitwa na wakati katika miaka kama 23 iliyopita, sasa leo imeletwa hapa kwa ajili ya kutaka kunyamazisha waandishi ni jambo la hatari sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, sheria hii inazungumzia juu ya kuchapisha, sasa kuchapisha inachapishwa kwanza inapitiwa na *Editor* na gazeti haliwezi likapitisha habari ambazo ni za kuchochea. Kwa hiyo, kwa upande wangu napendekeza kwamba, hii sheria irudishwe na iangaliwe upya na iondolewe hapa Bungeni, sheria nzima iletwe na siyo kifungu kimoja.

Mheshimiwa Spika, kuonesha kwamba sheria hii inatungwa, *Attorney General* naye anatumia hili neno kwa hasira ni kweli kwa hasira kwa sababu imechukuliwa sheria hii baada ya kuwa ya kashfa imekuwa ya jinai na kwenda kubadilisha kanuni ya adhabu nayo ikafanyiwa tafsiri ya maneno *sedition* katika kifungu cha 51 na mara moja ikabadilishwa kuwa ndiyo makosa.

Mheshimiwa Spika, kweli kuna kashfa zinatolewa ambazo ni za moja kwa moja ni *sedition*, lakini *sedition* tayari iko kwenye *penal code*. Kwa hiyo, kwa yale ambayo watayawasilisha peke yao kwa mdomo wakamatwe huko kwenye maeneo hayo waliyotendea makosa, lakini kuleta kwenye gazeti, gazeti ikiwa *monitored* itakuwa imedhibitiwa sawasawa, lakini tukiendelea kama tutakubali sheria hii ipite magazeti mengi yatafungiwa kila siku, waandishi wengi watafungwa na fani hii itakuwa imenyamazishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia pia juu ya filamu. Filamu nyingi hapa Tanzania tunazoziona zinatoka nje, sasa hizi za hapa ndani kama utazidhibiti kwenye hii, je, zile zilizotoka nje wanazozindika nani anazidhibiti? Utawakamata kutoka wapi? Kwa hiyo, hata hii sheria nayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. B. AKUNAAAY]

pia haijaangaliwa, inaelekea kuna mtu mmoja huko Serikali amekashfiwa sasa wakaona dawa ni kuja kuleta sheria na kuweka adhabu ya juu. Hatutungi sheria kwa namna hiyo, hii itakuwa ni sheria ya ku-*revenge* au kulipiza kisasi. Sheria inatungwa, watu wanaadhibiwa ili wawe *reformed*, siyo kwa jinsi hii, bora tutunge sheria nyingine za maana kuliko hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nitazame juu ya *Civil Aviation*. *Civil Aviation* kuna Bodi na watendaji ambao wanaambiwa kwamba katika miezi 18 wasifanye kazi na *industry*. Ni kweli sehemu nyingine inafaa kwamba, wale ambao walikuwa na vyeo wasifanye kazi hiyo, lakini nimegundua karibuni tu, nimesoma kwamba, *technicians* kama *pilots* au *air navigations* na kadhalika, wakihama na utaalim wao wakaingia katika kampuni nyingine, sioni kama wanaweza wakadhuru ile *authority* waliyotoka.

Mheshimiwa Spika, ni sawa kifungu kinalinda kampuni ya awali unapotoka usitoke na siri zake, lakini katika hili wale wataalam hawatatoka na jambo ila wanatoka na utaalim wao, kwa hiyo, kufanya kazi sehemu nyingine ningeomba waruhusiwe na hicho kifungu kiangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, niangalie upande wa Mfuko wa Elimu, kwa hakika Mfuko wa Elimu kupitisha fedha ya *Loans Board* kwenye Mfuko wa Elimu tunaweka urasimu wa bure kwani *loans* hizo zitachelewa zaidi, ni bora mfumo wa sasa uendelee, hizo fedha zipelekwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wanafunzi wanalalamika kwamba, mikopo yao inachelewa, sasa tena tukianza kupeleka kwenye Mfuko wa Elimu na Mfuko wa Elimu tena uangalie ndiyo upeleke kwenye *Loans Board*, mikopo hiyo itachelewa sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache. Ahsante sana. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante sana. Nilisema atafuatia Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah ambaye pia atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Mhita.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kifungu hiki sehemu hii ya pili ni kukidhi mahitaji ya Kimataifa katika usafiri wa anga, lakini nataka nisaidiwe kidogo, sijui sheria hii imezingatia nini kuhusiana na usalama wa raia wanaosafiri nchini, kwa sababu mara nyingi tunapopanda ndege kwenda sehemu nyingine kunakuwepo na rubani mmoja tu, rubani yule ni binadamu na anaweza akapata matatizo wakati wowote. Sasa sijui sheria hii inazingatia nini? Inazingatia mambo ya Kimataifa tu au inazingatia zaidi mambo ya ndani ya nchi? Kwa hiyo, nadhani kwamba sheria hii ingezingatia zaidi mambo ya nchi halafu baadaye ikaenda Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachokisema hapa ni kwamba, raia hawana uhakika wa usafiri wanaotumia kwa sababu ile ni ndege na inaweza kutokea *fault* yoyote na wakati wowote na yule ni rubani yuko peke yake. Kwa hiyo, ni vizuri ndege kama zile kuwe na rubani wawili, sijui sheria hiyo inazungumza vipi.

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie Mfuko wa Jimbo yaani *CDCF*. Sheria hii sehemu ya tatu lengo kubwa ni...

SPIKA: Kuna mtu simu yake iko *on*, sijui ni wewe mwenyewe msemaji au?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. A. ABDALLAH]

Mheshimiwa Spika, Kifungu hiki cha (3) kinazungumzia CDCF. Kuna ukaguzi hapa, Mkaguzi wa Mfuko wa Jimbo kwa Bara na Mkaguzi wa Mfuko wa Jimbo kwa kule Visiwani. Sasa Sheria hii inataka kuwaunganisha, Mkaguzi wa Hesabu za Matumizi ya Mfuko wa Jimbo Bara, wasaidiane na Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko wa Jimbo kule Visiwani. Sasa sheria ipi inayowaunganisha; yaani Bunge linamwambia Mkaguzi afuate sheria ipi Mkaguzi wa kule; kule wana sheria zao na sisi Wabunge tuna sheria zetu?

Yule Mkaguzi atakuwa *committed* namna gani kushirikiana na huyu Mkaguzi wa Bara? Anaweza kusema washirikiane au wasishirikiane. Sasa hebu tuweke *commitment* ya hawa Wakaguzi wawili, tunawaamrisha vipi wafanye kazi hizi za Ukaguzi kisheria.

Mheshimiwa Spika, nadhani hii itaweza kuleta mgogoro zaidi kama hatukulipatia ufumbuzi. Lazima Mkaguzi wa Hesabu kule Zanzibar awe na sheria ambayo ina *commitment* na huyu Mkaguzi wa Mfuko huu wa Jimbo hapa Bara awe na *commitment* ili waweze kufanya kazi hizi vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Sehemu ya VI, hii Bodi ya Mikopo. Wapo *Members* kama tisa hivi ambao wanaingizwa kwenye Bodi hii ya Mikopo. Kuna hiki Kifungu cha (f) ambacho kinasema; a *State Attorney of rank of senior or above, representing office of the Attorney General*. Hii hapa haiku-*specify*, kule Zanzibar hatuna Ofisi ya *Attorney General*, hapa tuna ofisi ya *Attorney General*. Sasa *Attorney General* ni ofisi ipi ambayo itapeleka Mjumbe katika Bodi hii ya Mikopo? Nilitaka iwe wazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuongezea ni kwamba, huyu Mwanasheria ni muhimu sana katika Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo, naomba na kule Zanzibar kuwepo na Mwanasheria ili aingizwe katika Bodi hii ya Mikopo, ili mambo yote ya kisheria yatakayokuwepo pale, waweze kuyajadili kwa pamoja, kwa sababu hiki ni chombo cha Muungano.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. A. ABDALLAH]

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni hizi hotuba za chuki ambazo zimetolewa adhabu katika *Penal Code*. Mimi nashindwa kuelewa na ninapenda amani sana, lakini unapokuta kwa mfano kitendo kilichotokea hivi karibuni, watu wameua ng'ombe wa wakulima na wafugaji, wameua watu, kwa hiyo, kiongozi asiende jukwaani akatoa hotuba akaseme nini! Hebu tuichuje ile hotuba aseme nini. Matukio kama haya ambayo yametokea si ya kibinadamu ni ya kinyama. Hivi unategemea mtu apande pale aseme nini? Hii tafsiri ya uchochezi mmeiweka namna gani?

Nilitaka tuiangalie katika mazingira haya, tafsiri ya uchochezi itakuwaje kwa sababu hatutasita kusema. Mnapofanya vitendo ambavyo si vya kibinadamu, tutasema kwa nguvu yoyote ile bila kujali sheria hii, kwani tuna sababu na Wananchi wapo wanaonekana. Kwa hiyo, hili mlizingatie vizuri, kuhusu uchochezi iletwe tafsiri nzuri iweze kueleweka.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine nazungumzia uhuru wa vyombo vya habari. Uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu sana. Kwa kweli kama tutawabana waandishi wa habari, tunabana demokrasia ya Taifa hili. (*Makofi*)

Habari ni haki ya kila raia, *provided* habari ile ina ukweli. Mimi nadhani waandishi wa habari hebu tuwaachie uhuru kabisa; yule ambaye ameguswa na mwandishi wa habari, sheria zipo za kwenda kulalamika kwamba, mwandishi wa habari wa gazeti fulani, redio au TV, amenifanya moja, mbili, tatu na kwa maana hiyo atadai *remedies* za kulipwa kulingana na yale ambayo amefanyiwa na chombo hicho cha habari. Sasa leo tutatoka adhabu kubwa maana yake nini?

Mimi sielewi tafsiri hii. Tunaogopa nini? Mahakama zipo, wakienda kinyume mtu ameshitakiwa ana haki ya kwenda mahakamani; sasa kwa nini tunawafinya sana waandishi wa habari? (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. A. ABDALLAH]

Waandishi wa habari ni watu ambao wanasaidia Taifa hili. Waandishi wa habari ni watu ambao wanaibua mambo yote ya aibu ambayo yanafika hapa. Kuna watu ambao wanajihusisha na dawa za kulevya, fedha haramu, wizi, ujangili, lakini waandishi wa habari wanasaidia sana. Kwa hiyo, nasema waandishi wa habari wasiogopeshwe na sheria hii. Nawaambia kabisa, waandishi wa habari msiogopeshwe na sheria hii, fanyeni kazi zenu, toeni habari, tuelimisheni, *provided* mnaweza kuthibitisha ambacho mmekisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, isiwe kuna kundi la watu ambao wanaji-*protect* na sheria hii. Nasema waandishi wa habari ni watu ambao wanategemewa katika Ulimwengu huu; wanaelimisha, wanafundisha na wanaibua mambo mbalimbali katika Taifa na Taifa linapata mwongozo juu ya nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, sheria hii kwa upande wangu imegusa mambo mengi. Suala la mwisho ambalo ningependa nilizungumzie kidogo ni kima cha malipo cha wanafunzi wa elimu ya juu hasa wanapokuwa hawajapata ajira. Wapo wanafunzi wetu wamepata *degree* ya kwanza, ya pili, lakini bado hawana ajira, sijui sheria hii inazungumza nini katika kipindi ambacho hawana ajira kuhusu mkopo? Pia mme-*consider* vipi hii asilimia ambayo mnataka kuitoa kulingana na hali ya maisha itakavyokuwa, kwa sababu sheria hii ipo lakini maisha yanavyokwenda huko mbele hatuelewi? Inawezekana gharama za maisha zikapanda, kwa hiyo, kuweza kulipa kwa mwanafunzi inakuwa ni tabu.

Mheshimiwa Spika, ninasema kwamba, ingezingatiwa zaidi kipato ambacho anakipata yule mfanyakazi ili aweze kujikimu katika maisha yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nashukuru sana.
(*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Zabein Mhita, *of course*, Mheshimiwa Zambi nilimtaja kabla, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nikiwa kama mzazi, niweze kuchangia Sheria ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, niishukuru Serikali kwa kuweza kuongeza fedha kwa ajili ya mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mimi nipo katika Kamati ya Huduma za Jamii, tulipokuwa kwenye Kamati Dar es Salaam, walikuja vijana wa kike na kiume, ambao walikuwa na sifa za kujiunga na Vyuo Vikuu lakini hawakuweza kupata mikopo. Kusema kweli walitia huruma sana, walikuwa wakilia mbele yetu. Wale ambao mko kwenye Kamati ya Huduma za Jamii mtakumbuka na hasa niki kumbuka wasichana.

Mheshimiwa Spika, kama ninakumbuka vizuri, lengo kuu la kuanzisha hii mikopo kwa ajili ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu lilikuwa ni kuongeza idadi ya udahili kwa ajili ya wanafunzi katika Vyuo Vikuu vya hapa nchini. Kwa sababu idadi ya udahili nchini ilikuwa ni ndogo sana ikilinganishwa na udahili wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu vingine katika nchi za Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo ikaonekana kwamba, ili tuweze kuongeza idadi basi, ianzishwe hii Bodi ya Mikopo iwasaidie wanafunzi wenye uwezo wa kiakili, lakini wanaotoka katika familia ambazo hazina uwezo wa kifedha; ndiyo lilikuwa hasa lengo kuu. Tukasema wale watoto wanaotoka katika familia ambazo zina uwezo wa kifedha, ziwali pie watoto wao kwa ajili ya masomo ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati Muswada huu ulipoletwa Bungeni ulipita kiulaini sana. Ulipita kamanyola bila jasho, kwa sababu Waheshimiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. Z. M. MHITA]

Wabunge, walipoelezwa kwamba mikopo hii itatolewa tu kwa watoto ambao wazazi wao hawana uwezo, waliona tutakuwa tunawasaidia wazazi ambao hawana uwezo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, huu ni mkopo, sasa sisi wazazi wenye uwezo wa kifedha kwa nini umuweke mtoto wako katika mazingira ya kulipa deni baadaye wakati unaweza kumwondolea mzigo huu sasa? leleweke kwamba, huu ni mkopo, sasa wazazi wenye uwezo na wanaowapenda watoto wao kwa dhati, wanapaswa wawalipie watoto wao ada ili mtoto akianza kazi asiwe tena na mzigo wa kulipa deni. Huku ndiyo kumpenda mtoto. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Sawa!

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, kumpenda mtoto wakati una uwezo siyo kumwachia achukue mikopo, ili imsaidie mtoto wa mzazi ambaye hana uwezo. Hilo ndiyo lilikuwa lengo kuu na kama nilivyosema, ilipoelezwa hivyo Waheshimiwa Wabunge walielewa na Muswada ulipita, narudia, kamanyola bila jasho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika Jedwali la Tatu la Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu, imebainishwa wazi kuwa, asilimia 64 ya makusanyo ya Mfuko wa Elimu yataelekezwa kwenye Bodi ya Mikopo. Sasa nasema kuna haja ya hii sheria kuweka kipengele cha sheria ambacho kitaonesha na kubainisha ni asilimia ngapi katika asilimia ile 64 itakayotengwa kwa ajili ya watoto ambao wanatoka katika familia maskini, bila kujali wanachukua masomo gani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani? Tunapotoa kipaumbele kwa wanafunzi waliochukua kwa mfano, masomo ya sayansi kwamba ndiyo walipiwe mikopo hii; hii mikopo itakwenda kwa watoto ambao ndiyo walewale waliosoma *pre-school* katika *private school*, waliosoma *primary* katika *private school*, waliosoma

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. Z. M. MHITA]

secondary katika *private school* na ambako ndiyo kuna ada kubwa. Sasa unashangaa; mtoto aliyelipiwa katika *private school* tangu *pre-primary* mpaka anafanya *A-level* yake anakuja sasa kupata mkopo Chuo Kikuu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiieleweki, yaani huwezi kuieleza hii pamoja na kwamba, natambua inawezekana kabisa mzazi akaweza kumsomesha mtoto wake katika *private schools* lakini baadaye pengine akafariki, lakini hawa ni wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa watoto wanaotoka katika familia maskini, mfano nichukue kwangu Kondo, ndiyo ambao wamesoma katika shule ambazo hazina walimu wa sayansi, hazina maabara za sayansi; hawa watoto wanafaulu vipi masomo ya sayansi mpaka wapate *priority* ya kupata mikopo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza kwamba, Muswada huu ulipoletwa ulilenga hasa watoto ambao wanatoka katika familia maskini, lakini hakuna kifungu chochote cha Sheria Mama wala marekebisho yake, kinachoonesha na kubainisha kwamba, Bodi hii ya Mikopo ilianzishwa au ipo kwa ajili ya kuwawezesha watoto wanaotoka katika familia maskini, ambao hawawezi kugharamia masomo ya Vyuho Vikuu; yaani Sheria ipo kimya! (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, sasa nasema, sheria ioneshe kwamba, Sheria hii imetungwa ili kuwalenga watoto ambao wanatoka katika familia maskini. Kama haioneshi siyo rahisi hata kuwasaidia hawa watoto, maana unaangalia sheria imemlenga nani; haijaoneshwa! Kwa hiyo, napendekeza sheria nayo ioneshe kabisa kwamba, inalenga watoto ambao wanatoka katika familia maskini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. Z. M. MHITA]

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa nikiwa na masikitiko makubwa kwamba, lengo la mikopo limebadilika, sasa linalenga watoto wachache ambao wengi wao wazazi wao wana uwezo. Naomba hili liangaliwe na litiliwe maanani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikiwa kama mama, naomba nikushukuru tena kwa mara nyingine, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii hoja iliyo mbele yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Haya ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Godfrey Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mambo machache kwenye Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali, ambao umewasilishwa asubuhi hapa Bungeni.

SPIKA: Hiyo *microphone* yako sijui ina nini au kuna mwingine ameacha wazi?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mambo machache, kufuatia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, ambao umewasilishwa hapa Bungeni asubuhi. Pia naishukuru Serikali kwa kuleta mabadiliko haya ya Sheria hizi mbalimbali ambayo yalionekana kuwa na kasoro.

Mheshimiwa Spika, nianze na Sheria ya Magazeti. Wazungumzaji wengi wamekuja na mtazamo hasa waliozungumza kutoka upande wa pili, wakiona kwamba, watu wa habari au wa magazeti au vyombo vya habari, wanakusudiwa kupewa adhabu kubwa na Serikali pale wanapofanya makosa. Wanasema kufanya hivyo ni kubana uhuru wa habari au watu kutafuta habari au watu kutoa habari.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. W. ZAMBI]

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme kwamba, uhuru wowote ule, uwe wa mawazo, kupata habari au kutoa habari, kama hauwezi kuwa na mipaka basi hauwezi kuwa uhuru, kwa sababu hata demokrasia nayo pia ina mipaka yake. *(Makofi)*

Mimi sioni kwa nini mtu apate hofu tunapotunga sheria kali kwa wale watu ambao wanakusudia kuleta lugha za uchochezi, lugha za kugombanisha Serikali na Wananchi na lugha za matusi kwenye jamii. Watu wanapata wasiwasi na wanatetea kabisa kwamba, hapana tusiweke adhabu kubwa kwa sababu itakuwa ni kuua demokrasia. Hivi kuchochea matusi, watu wapigane, ndiyo uhuru wenyewe au demokrasia? Kama ndiyo uhuru au demokrasia yenyewe hio, mimi nitawashangaa sana na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tuhofie kwa sababu huyu mwandishi wa habari, awe mtoa habari au mtafuta habari, ninamtegemea awe Mtanzania, awe mzalendo, ambaye anapotoa habari, anatoa habari ambazo siyo za kuchochea ugomvi, siyo za kutukana viongozi. Anatoa habari za kujenga nchi, anatoa habari ili kuhakikisha kwamba, jamii ya Watanzania inaishi vizuri na kwa amani muda wote. Mimi ndiyo mtazamo wangu, maana kama unatetea tuache watu watoe habari kama wanavyotoa leo, sijui tunataka tujenge Tanzania ya namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hao wenzetu ambao wanazungumza kwamba tuache hili jambo liwe hivyo hivyo; hivi ni nchi gani ambayo inaweza ikaendeshwa inavyotaka?

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumza asubuhi hapa mambo ambayo nimeshindwa kuyaelewa. Anazungumzia kwamba, tusitunge sheria kuwadhibiti wachochezi wanaotoa habari za uongo na wanaogombanisha watu; lakini yeye mwenyewe leo kuonesha kwamba anataka tuendeleo na lugha za uchochezi, ameanza kukumbusha mambo ambayo yaliwapata Watanzania, mambo ambaya ambayo nina hakika Serikali imeyashughulikia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. W. ZAMBI]

Amezungumzia eti Serikali ya CCM inang'oa watu macho, Serikali ya CCM inatoa watu kucha, mambo hayo yako wapi na tulishasimama hapa Bungeni tukayakataa? Leo bado anaendelea kuyazungumza, hizi ndizo lugha za uchochezi. Hatutegemei kiongozi, *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani, atoe hotuba ambayo ni ya uchochezi. Sasa kama tunaweza kuwahamasisha watu waendeleo kutoa habari za uchochezi kwamba huu ndiyo uzalendo, huu ndiyo Utanzania, nadhani hata Watanzania watatushangaa sana huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme ninaunga mkono hoja au mapendekezo yaliyotolewa na Serikali kwamba, ili kudhibiti watu wenye mienendo mibaya, nami ninaamini siyo wanahabari wote ni wa hovyoy, hapana, wapo wachache, hawa ndiyo tuwadhibiti. Maana mtu afanye akijua kwamba, kuna faini, kuna kifungo. Eeh, lazima iwe hivyo; vinginevyo, hatuwezi kuacha hivi hivi likawa Taifa linalojienda tu.

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, hili wala tusiwe na hofu, wale ambao wana hofu, nadhani wanataka waendeleo kutumia vyombo vya habari vibaya kwa manufaa yao wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhuru wowote bila demokrasia siyo uhuru ni fujo. Uhuru wowote bila demokrasia ya kweli ni fujo na Katiba yetu imezungumza, unapokuwa na uhuru pia ujue kwamba na wewe una wajibu. Sasa wajibu wetu ni kwamba, una uhuru wa habari, lakini ujue wajibu wako ni kuhakikisha unakuwa na tabia ya Kitanzania, lakini pia unatoa habari ambazo siyo za uchochezi, siyo za kufanya watu waendeleo kutukanana katika nchi ambayo inapigiwa mfano katika Bara la Afrika, lakini pia duniani kwa amani iliyopo katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ninaliunga mkono na ninaomba tuendeleo nalo kama lilivyo. Tuseme kwamba ni vizuri sasa kama walivyoshauri wengine, tuje na Sheria nzima ya Vyombo vya Habari. Kwa sababu hii Sheria pia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. W. ZAMBI]

imezungumzwa kwa muda mrefu sana. Sasa sielewi maana hii Sheria tuna-*amend* kipande kipande, tunaleta *miscellaneous* leo, nilitegemea inakuja Sheria yote ya Vyombo vya Habari.

Tunapoleta kipande wala haifurahishi. Inawezekana watu wakaelewa kwamba, Serikali labda ina nia mbaya juu ya jambo hili. Kwa hiyo, tunategemea Serikali ilete kwenye Bunge la Kawaida, Sheria ya Vyombo vya Habari ili tutunge Sheria ambayo inasimamia Tasnia ya Habari ambayo itakuwa inamaliza kila kitu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala dogo ambalo na wenzangu wamelizungumzia pia la mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia Kifungu cha 29 ambacho kinataja Wajumbe wa Bodi, pamoja na mabadiliko au *Schedule of Amendment* ambayo imepitishwa. Naomba nipendekeze, kwa sababu mikopo hii sasa haipo *restricted* kwa ajili ya Vyuo Vikuu vya Serikali pekee au Taasisi za Serikali pekee, hata Shule Binafsi na Vyuo Vikuu Binafsi navyo watoto wanapata mikopo. Nataka niishauri Serikali ikubali walau iwe na mtu atakayekuwa anatoka kwenye Vyuo Binafsi au Taasisi Binafsi, ambaye ataingia kwenye Bodi ya Mikopo. Maana yake ilivyo yote ni Serikali au Vyombo vyote ni vya Serikali. Kwa hiyo, ni vizuri pia Taasisi Binafsi zikawakilishwa kwenye Chombo hiki ili nao waweze kutoa uzoefu wao wanapokuwa wanakutana kwenye Mikutano hiyo. Hili naomba Serikali ilione kwamba ni jambo muhimu na linafanywa kwa nia nzuri. Hii itakuwa pia inaendeleza utamaduni wa Serikali wa kushirikiana na Taasisi Binafsi katika masuala muhimu kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda niseme, hii asilimia 64 ya fedha ambazo zitakuwa zinakwenda kwenye hii Bodi ya Mikopo siyo hela kidogo. Tabu yangu ni akina nani hasa wanafaidika na mikopo hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. W. ZAMBI]

Mheshimiwa Spika, tulishazungumza hapa Bungeni kwamba ni vizuri tungeiangalia Bodi yenyewe yote ifumuliwe upya, ianze upya, maana malalamiko yaliyopo ni makubwa sana kwenye Bodi ile. Kwa hiyo, nataka tuwe na mtazamo huo pia. Mikopo itakayokuwa inatolewa kuanzia sasa ni vizuri Serikali ingekubali, tupate orodha ya vijana wote na ikiwezekana orodha hiyo iwasilishwe hapa Bungeni ili tuone vijana ambao wanachaguliwa na wanastahili kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tulisema itakuwa ni jambo la ajabu sana, mtoto wa Waziri, mtoto wa Mbunge, mtoto wa Katibu Mkuu wa Wizara, anapata mkopo, lakini mtoto wa mkulima kule kijijini anashindwa kupata mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwa dhati ya moyo wangu kabisa, nilishawahi kuwa Mkurugenzi kwenye Bodi ya Baraza ya Chuo Kikuu Mzumbe, ni kweli watoto wa vigogo wengi tu wanapata mikopo, lakini watoto wa maskini wamebaki nje hawana mikopo. Tulishasema humu ndani hivi Mbunge gani leo, Waziri gani leo, Katibu Mkuu yupi wa Wizara au Mkurugenzi gani wa Shirika, ambaye anashindwa kulipa ada ya mtoto wake Chuo Kikuu, lakini watoto wa maskini wale ambao wamesoma shule hizo hizo za Kata wanakosa mikopo, kwa sababu tu eti hajasoma masomo ya Sayansi, hajasoma masomo ya Uhandisi. Hatutaki kuwa na sheria ya ubaguzi ambayo inabagua baadhi ya watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nipendekeze hapa, wakati tunapitishwa sheria hiyo tuhakikishe kwamba, Serikali inaleta orodha ya vijana wote watakaokuwa wanachaguliwa kwenye Vyuo Vikuu ili tusome, kama ni mtoto wa Zambani anakwenda Chuo Kikuu na amepata udhamini, lakini watoto wengine wa maskini wamekosa, tujue na tuelezane kwamba tunajenga Taifa la namna gani. Maana wakati mwingine tuache na wale ambao hawawezi kabisa, basi waweze kuangaliwa vizuri zaidi na waweze

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. W. ZAMBI]

kusaidiwa, basi hapo tutakuwa tunajenga Taifa la watu ambao wana usawa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kwangu, nashukuru tu ile hoja ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kukagua Hesabu za Jimbo. Mimi nilishakaa kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), tuliona lipo tatizo la matumizi ya pesa ya Mfuko wa Jimbo. Lipo tatizo, Wabunge wanaweza wakakubali wasikubali, lakini lipo tatizo. Wakati mwingine kunatokea ubishi kati ya Mkurugenzi na Mbunge nani hasa ambaye anastahili kutumia fedha zile. Sasa hili na kwa Wabunge wenzangu, naomba nitahadharishe kwamba, tusipoangalia linaweza likatuchafua. Nimesikia wakati mwingine Mbunge mwingine anasema hizi bwana ni hela zangu, mwingine zikija anasema mimi naziomba!

Sasa kama hatuwezi kuwa na udhibiti, Wabunge tunaweza tukaingia kwenye kashfa ambazo Wabunge wa Kenya waliwahi kuingia kwa sababu ya fedha za Mfuko wa Jimbo. Kwa hiyo, kama tunataka tuwe *safe*, ni vizuri Mkurugenzi akajua kwamba, yeye ndiye mwenye wajibu wa fedha zile, yeye ndiye atakayekaguliwa, kazi ya Mbunge ni kuhakikisha kwamba, anasimamia tu, hizi fedha zinapaswa ziende mahali fulani. Nadhani Mbunge atakuwa amefanya kazi yake yeye akatambua matatizo ya Wananchi wake, lakini watu wengine wakazitoa zile pesa na Mbunge utakuwa *smart* na wala hutapata shida yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme ninaunga mkono Sheria hii ambayo imewasilishwa na Serikali na hasa lile la magazeti nililolisema, ni vizuri Serikali isirudi nyuma wala isitetereke, tunataka tujenge Tanzania ya watu ambao wana nidhamu, tunataka tujenge Taifa la kizalendo, Taifa la watu wanaoheshimiana, Taifa la watu ambao wanatumia lugha za Kitanzania zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Mawaziri, mtaitwa baadaye, kwa sababu Miswada hii ipo katika maeneo mbalimbali ya Wizara zenu. Kwa hiyo, wengi mnaoniomba nitawaachieni mpaka mwishoni kusudi muwasakilize Waheshimiwa Wabunge kwanza.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Chistowaja Mtinda, Mheshimiwa Moses Mchali pia ajiandae na Mheshimiwa Rajab Mohamed ajiandae.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, nami niweze kuchangia machache. Awali ya yote, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, aliyowasilisha hapa Bungeni, kwa sababu imekuwa na mambo mazito na kweli Serikali inatakiwa iyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nami nijikite moja kwa moja kwenye Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa hiyo, huu Mfuko unanihusu na tumeufanyia kazi kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, wameongea wenzangu Wajumbe wa Kamati kwa masikitiko makubwa sana, wakionesha ambavyo madhumuni ya kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo yalivyobadilishwa kinyemela, yakawa sasa hayawalengi watoto waliokusudiwa, watoto wa maskini lakini wenye uwezo kiakili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna upotoshaji mkubwa sana wa kuonesha kwamba, watoto wanapokosa mkopo, wanapokwenda kudai wanaonekana kama vile hawana uwezo wa kiakili ila wametoka katika familia za kimaskini.

Mheshimiwa Spika, ameongea Mheshimiwa Mhita hapa, walikuja vijana wengi sana, vijana hao wote walikuwa wana sifa za kupata mkopo na wote walitoka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. G. MTINDA]

katika familia zisizo na uwezo au maskini, lakini kwa bahati mbaya sana walikosa mkopo huo.

Mheshimiwa Spika, sasa niunge mkono hoja ya kwamba, Sheria hii ya Bodi ya Mikopo ambayo imeletwa hapa ipo kimya kuelezea ile asilimia 64 ambayo itawekwa kwenye Mfuko wa Elimu kwenda kwenye Bodi ya Mikopo; ni asilimia ngapi ya hiyo asilimia 64 sasa itawafaidisha watoto wa maskini bila kujali masomo wanayochukua, itamke wazi. Kwa kweli Sheria ipo kimya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapata shida sana wamesema wenzangu, tunafahamu mazingira ya Sekondari zilizopo sasa hivi, Sekondari za Kata siyo rafiki kwa masomo ya sayansi. Mazingira hayo siyo rafiki kwa watoto wa maskini; hakuna maabara, hakuna vitabu, hakuna walimu wa sayansi na hata walimu wa masomo mengine. Mimi ni mwalimu, hata kama wana akili kiasi gani, ni kwa namna gani watoto hawa wataweza kufaulu masomo ya sayansi ikiwemo hisabati bila kuwa na walimu, bila kuwa na maabara wala bila kuwa na vitabu?

Mheshimiwa Spika, kwa huzuni kubwa kabisa ameongea Mheshimiwa Mhita; tulipoiuliza Wizara ni lini vilibadilishwa vigezo ambavyo vililetwa Bungeni na vikapitishwa vizuri sana ili wanafunzi waweze kupata mikopo? Tuliambiwa ni Baraza la Mawaziri, hatuwezi kukataa, ndiyo ambao walitoa vigezo ambavyo sasa vipo vinalega wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, tuwe wakweli, sasa sisi Viongozi ambao tuna uwezo wa kuwasomesha watoto wetu, tumekuwa wabinafsi. Baraza la Mawaziri lina-*involve* Mawaziri, Mawaziri ni Wabunge, Mawaziri ni Viongozi wa Juu, watoto wao wanasoma shule ambazo ni bora, shule ambazo wanafunzi wanafaulu masomo ya sayansi vizuri sana. Tukasema vigezo hivi sasa vipaumbele viwe ni sayansi, hisabati, *engineering*, siyo *art*, biashara, sheria wala masomo mengine ila iwe ni sayansi, tukijua kuwa watoto wetu ndiyo wanaotoka katika shule hizo na watoto wetu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. G. MTINDA]

ndiyo watakaofaidika na mkopo kwa asilimia 100; huu siyo ubinafsi ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Sera iko wazi kwamba, mtoto anayetoka katika familia yenye uwezo alipiwe masomo asilimia 100. Sasa kwa sababu mtoto wangu amesoma shule nzuri, amefaulu sayansi amepata *division one*, huyu mtoto wangu anapewa mkopo asilimia 100 na mimi siwezi kukataa, kwa sababu ndivyo Sera inavyotamka. Huu ni ubinafsi.

Mheshimiwa Spika, hebu sasa Serikali kupitia Sheria hii, itamke wazi asilimia 64 amependekeza Mheshimiwa Mwenyekiti wangu Mama Margaret Sitta kwamba, katika hiyo asilimia 64, basi asilimia 60 na mimi ninaunga mkono, asilimia 60 iende kwa watoto maskini wenye uwezo kiakili ili iweze kuwalipia mikopo yao na hiyo nyingine inayobaki iende kwa watoto wengine. Hiyo asilimia 60 isiangalie mwanafunzi anachukua masomo gani; awe anachukua *art*, awe anachukua sayansi, masomo yoyote ndivyo ambavyo Mfuko huu au Bodi hii ya Mikopo ililenga. Kwa hiyo, tusipoteze malengo mahususi, tunaweza kabisa sisi kuwasomesha watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niungane na Mheshimiwa Margaret Sitta kwamba, tusikatae kuchangia elimu. Sisi ambao tuna uwezo tusikatae, tuchangie kwa sababu ni mojawapo ya kuleta maendeleo katika nchi yetu, lakini kwa mzazi maskini hawezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda nilizungumzie ambalo naona litakuwa la mwisho ni uwakilishi wa wanafunzi katika Bodi ya Mfuko wa Elimu. Hotuba ya Kambi ya Upinzani imependekeza kwamba, huu Mfuko wa Elimu ambapo hela za wanafunzi sasa zitapelekwa kwenye Bodi ya Mikopo ni asilimia 64. Bodi yake haina wawakilishi wa wanafunzi ambao ndiyo wadau. Nami ninapendekeza kwamba, wadau kutoka Vyuo Vikuu vya *Private* na *Government*, wawe wawakilishi katika hii Bodi ya Mfuko

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. G. MTINDA]

wa Elimu ili waweze ku-*monitor* hela yao na waweze kutoa maamuzi sahihi ambayo sasa yatawasaidia hata katika kurekebisha mambo mengine yanayohusu mikopo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru tena, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Christowaja ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Machali, halafu nilisema Mheshimiwa Rajab Mohamed na Mheshimiwa Mbarouk atafuatia.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa, nami nichangie katika Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, siku moja wakati nazungumza na wanazuoni na wanaharakati mbalimbali, Hayati Profesa Seth Chachage, alituasa Watanzania na Dunia kwa ujumla kwamba, naomba nimnukuu: "*You can burn organizations, you can liquefy people, but revolution ideas will not die.*" Unaweza ukaamua kuua au kuzuia Taasisi mbalimbali zisifanyie kazi na hata pengine kuweza kuwaua watu, lakini kamwe mawazo ya kimapinduzi ama mawazo ya mabadiliko hayawezi yakafa yote, waliobaki nao pia wataendelea tu kufanya kazi yao.

Kwa nini ninaanza kumnukuu huyu bwana; ni kwa sababu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali unaonesha wazi umetungwa kwa hasira na Ofisi ya *Attorney General*.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali mara nyingi na kwa nyakati tofauti ...

SPIKA: Hebu hama hiyo mashine inapiga kelele.

MHE. MOSES J. MACHALI: Kwa nyakati tofauti amekuwa anatuasa Wabunge tujaribu kuzungumza kwa busara na tujaribu kuangalia wakati huo tunasema nini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J. MACHALI]

Muswada ambao umekuja hapa ulioletwa na Serikali ambao ofisi yake ni *main custodian*, ni wazi unaonesha kwamba, una hasira na Waandishi wa Habari. Adhabu au hatua ambazo zinazopendekezwa kuchukuliwa dhidi ya Vyombo vya Habari na Waandishi wa Habari, ni wazi inaonekana kuna watu watakuwa wameguswa mahali pabaya na ndiyo maana huwezi ukasema unatoka kwenye adhabu ya shilingi 150,000 unasema watu watozwe milioni tano; huku ni kuminya uhuru wa mawazo, jambo ambalo nafikiri Ofisi yako Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, angalieni na mtafakari uamuzi wenu. Jambo hili halikubaliki.

Kifungo kilikuwa miezi sita, sasa mnataka kupeleka sijui mwaka moja. Ofisi ya *Attorney Geneal*, katika hili naomba mwende mkakae mliangalie. Nakushukuru, nakuona, ahsante sana, lakini *message sent*.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Kifungu cha 55(1), Ofisi ya *Attorney General* pia imeandika vibaya, kuna matumizi mabaya ya ile *interrogative pronoun "who."* Huwezi ukasema kwamba, ukitoka hapo ukaenda kuangalia kwenye Sheria kwamba *anyone who to ...*; naomba uende ukaangalie vizuri. Ndiyo maana jana tulizungumza pia suala la matumizi ya lugha na nadhani katika hilo pia uende ukaangalie ili kuweza kusahihisha lugha ambayo inakusudiwa kutumika katika Kifungu hicho cha 51(1).

Mheshimiwa Spika, ukienda kuangalia pia katika Sheria ya *Penal Code*, Sheria ya Kanuni za Adhabu, katika vifungu mbalimbali, unakuta wazi kabisa kwamba, Muswada umekusudia kuwaadhibu watu. Wakati mwingine tumekuwa tunapiga kelele tunashauri, kumfunga mtu kwa muda mrefu ni kuongeza gharama kwa Serikali kumhudumia huyu mtu akiwa gerezani. Mnatoa baadhi ya adhabu kutoka kwenye kifungo cha miezi mna-*suggest* iwe miaka miwili, mwaka mmoja; vitu gani hivi? Inaonesha wazi kabisa kuwa, kuna watu mmewakusudia mnataka kuwaadhibu,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J. MACHALI]

mnafanya kazi kwa chuki, mnafanya kazi kwa visasi; Serikali gani hii?

Ukweli ukisoma kwa makini huu Muswada hasa katika kipengele hiki cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, utaona kuwa kuna *targeted group* au kuna watu wamekusudiwa. Watu wanataka kuminya uhuru wa watu kuzungumza, jambo hili Mheshimiwa Waziri amezungumza, leo baadhi ya watu mnaona kwa sababu ndiyo mnaunda Serikali, kesho mnaweza mkaja mkakaa huku, Sheria hizihizi zitakuja kuwatafuna na ninyi; maana ninyi mnaangalia leo hamwangelii kesho, inawezekana ngoja subirini wakati wenu utakuja kufika. Kiboko ambacho mnataka kuwatandika watu hicho kiboko kitatumika kuwapiga na ninyi.

Nina imani kuwa, AG utaweza kuangalia pengine ni kitu gani mfanye, kutunga Sheria mtu ukiwa katika *state* ambayo siyo nzuri, kuna haja ya kufikiria. Hebu fikirieni vizuri halafu wenyewe mtaangalia mnaendaje. Suala ambalo nimezungumzia kuhusiana na kuwafunga watu, tumeshauri ukiangalia magereza yamejaa, yamefurika kweli mahabusu na hata bajeti, Serikali mmeshindwa kupeleka fedha kwa ajili ya chakula cha wafungwa, lakini bado leo mnakuja na Miswaada ambayo inakusudia kwenda kujaza magereza, mnakuja na Miswaada ambayo mnakusudia kwenda kujaza mahabusu zilizopo kwenye vituo vya polisi huku huduma zikiwa ni *poor*; mambo gani haya?

Mheshimiwa Spika, watu wanafanya kazi huko, wameingia porini wameenda kuanzisha mashamba, mnawakamata mnataka kuwarundika. Bado mnataka kuwazuia watu wasiseme yale ambayo watu wamekusudia; mambo gani? Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulikuwa umelewa au ilikuwaje sijui?

(Hapa Wabunge fulani waliguna kuonesha kutofurahishwa na maneno aliyotumia mchangiaji)

SPIKA: Sasa unazidisha, Machali unazidisha sasa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, ninaliondoa neno hilo.

SPIKA: Ahsante, endelea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, wakati mwingine mtu unafikia hatua ya kuweza kunanii kwa sababu ukisoma Muswada na kuangalia adhabu ambazo zimependekezwa, ni wazi watu inaonekana wana hasira na watu; badala ya kusema waangalie pengine sasa tunatokaje. Mimi nilifikiri kuwa ingekuwa ni vyema kwa Serikali kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukapunguza adhabu za kuwarundika watu magerezani. Tufikirie adhabu mbadala watu kwenda kufanya kazi kwenye maeneo mbalimbali.

Tunapokuja na Sheria kandamizi, Sheria za kuminya mawazo ya watu, Sheria za kuwafanya watu wawe ni watumwa wa kifikra, Sheria ambazo haziwezi kuwafanya watu wakafikiri kwa namna nyingine na pengine kuhakikisha Tanzania panakuwa ni mahala ambapo fikra za watu zinaheshimiwa.

Sasa tunakuja na Sheria za kuendelea kuwatisha watu, jambo hili siyo jema sana, wakati mwingine ninaamini Serikali imeteleza kwa wale wote ambao walihusika katika kuja kuandaa Muswada huu ambao unahusisha Mabadiliko ya Sheria mbalimbali.

Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia kuhusiana na masuala ya mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kama dhamira ya Serikali ilikuwa ni kuwasaidia watu, kuna haja ya kuachana na mtazamo ambao imekuja nao leo hii ili kuwawezesha vijana hawa waendeleo kupata fursa ya kupata Elimu ya Juu.

Vinginevyo, itakuwa ni kuwa-*discourage* watu na kuwafanya wazidi kuichukia Serikali na unaweza ukakuta mawazo mengine ambayo yameletwa ndani ya Bunge hili, ni ya watu wachache wamekaa huko wana *interest* zao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J. MACHALI]

na matokeo yake wanakuja kuleta mambo ambayo wakati mwingine yanakuja kuleta kero na chukizo kwa watu.

Mheshimiwa Spika, katika mambo ya msingi ningeshauri masuala ya itikadi tuyaweke pembeni na tuangalie *best approach* au *best practice* itakuwa ni nini; vinginevyo, jiandaeni kuendelea kujenga magereza, watu hawataacha kupiga kelele, watu watawaambieni. Kuna watu pengine hawako tayari kuona fikra zao zinaminywa katika misingi ya ugandamizaji, watu wataendelea kusema na wengine tutaendelea kusema pale ambapo tunapata fursa.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Nitasubiri wakati wa kukamata vifungu tuweze kuona ni namna ambavyo tutaweza kushauri na pengine Serikali ifikirie upya kuona ni jinsi gani inaweza kurekebisha baadhi ya vifungu ambavyo imetuletea hapa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada ambao tunaendelea nao. Ninataka nianze na suala la usafiri wa anga. Usafiri wa anga, Bodi ile imepewa nafasi ya kukopa, nilitaka hapa AG aende mbali zaidi, ni lazima hawa wawekewe kikomo cha huu mkopo. Tunajua sasa hivi nchi yetu imekopa sana, hebu tusiendeleo kukuza Deni la Taifa, ni lazima hawa wawekewe kikomo cha mkopo; hilo ni moja.

Kuhusu Mfuko wa Jimbo; ninakubaliana na ninaipongeza Serikali, AG ninakupongeza sana kwa hili, kwa kuona kuwa ipo haja ya Mfuko wa CDCF kwa upande wa Wabunge wa Zanzibar kuweza kukaguliwa. Hili ninakubaliana na wewe, ila ninachoomba, katika Sheria inaonesha kuwa, Ofisi ya CAG itashirikiana na Ofisi ya CAG Zanzibar kufanya hii kazi. Ninaomba kidogo hapa paangaliwe upya, isiwe ni kushirikiana bali siyo Ofisi ya CAG Zanzibar, iwe ni *agent* wa CAG wa Serikali ya Muungano,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED]

yaani afanye kazi kwa niaba na siyo kushirikiana. Ninaomba hilo kama mtaliona linafaa basi liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la asilimia 50 kwenda kwa ajili ya Elimu ya Juu; ni lazima tukubali kwamba, elimu hapa nchini kwetu hususan ya msingi na sekondari, ndiyo elimu ambayo ina matatizo na ina changamoto nyingi kuliko Elimu ya Juu. Hivyo, ni vyema fedha hizi mkabadilisha mwelekeo ili zaidi ya asilimia 50 ziende katika elimu ya msingi badala ya kuzipeleka juu kwa wanafunzi ambao watakuwa wameshaelimika kwa kiasi fulani. (*Makofi*)

Niende sehemu ya tano ya Muswada huu, ambayo inapendekeza Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza. Nafikiri Serikali hapa ilitakiwa kwanza ikae ifanye tathmini, wasilete Sheria nusunusu. Kuleta Sheria nusunusu itatusumbua sana, kwa sababu hapa yeye anazungumzia tu filamu na michezo ya kuigiza, lakini angetoa tafsiri yake filamu na michezo ya kuigiza, kwa sababu sasa hivi kuna *internets*, kuna mitandao, kuna mambo ya *whatsapp*, yote inatoa, tena ni hatari kubwa. Mkiangalia hata baadhi ya simu humu ndani, ukiangalia *whatsapp* utaona picha zilizomo au picha wanazorushiana watu ni hatari. (*Kicheko*)

Tusitunge tu Sheria ya kuadhibu hawa wengine na tukaacha *loophole* kwingine, ni lazima hii Sheria iangaliwe kwa undani zaidi. Mnaweka adhabu kwa hawa ambao tunawaona katika televisheni au katika magazeti, lakini tunasahau na upande wa pili wa shilingi kuwa hawa wapo, sitaki kuwataja wengine akina Mheshimiwa Kombo, kabisa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niende sehemu ya nane, ambayo inapendekeza Sheria za Magazeti, sikutegemea kuwa AG ataleta Sheria ya kuzidi kuwabana au kuzidi kutaka kuwakandamiza waandishi wa habari. Lazima tukubali kuwa, waandishi wa magazeti wamefanya kazi kubwa sana katika nchi hii, hilo ni lazima tulikubali. Wao ndiyo ambao tunawatumia kwa kutoa habari zetu, wana matatizo mengi na wameshayaeleza, waajiri wao wanavyowabana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED]

waandishi wa habari hawa wa magazeti, lakini tumetia pamba! Leo tunakwenda kuwaongezea faini; ni sawasawa na kuwapiga msumari wa moto.

Lazima tunapoleta Sheria tuziangalie katika pande zote, tusiweke faini kubwa, wana matatizo ya mishahara, wana matatizo ya kupata fedha nyingi zaidi hawa, mazingira mabovu ya utendaji kazi, lazima hayo tuyaangalie. Hizi Sheria zisije nusunusu, hawa wanadai Sheria ya Vyombo vya Habari, imedaiwa siku nyingi sana hapa, lakini hadi leo haijaletwa, badala yake tunakuja kungeza faini.

Jamani hawa ni Watanzania wenzetu, unapoweka viwango vikubwa vya faini hivi lengo lako ni nini; unataka kuwadhibiti tu wasiandike habari za uchochezi; huna njia nyingine ya kuwadhibiti kweli? Hii kweli ni *simple way* ya kudhibiti? Mimi ninafikiri Serikali ichukue muda, hebu itafakari upya haya masuala, leteni hii Sheria ya Vyombo vya Habari na wao hawa wanahabari watoe maoni yao, wazungumze ya kwao, baada ya wao kuleta ya kwao, tuwawekee adhabu ya kuwapa pale watakapokengeuka au watakapokwenda kinyume na yale ambayo tumekubaliana nao, lakini tusiwawekee adhabu kali namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende sehemu ya kumi ambayo inapendekeza marekebisho katika Sheria za Kanuni za Adhabu, Sura ya 16. Mheshimiwa AG, nchi yetu hivi sasa ni ya kidemokrasi, ni nchi ambayo sasa hivi kila kitu kipo wazi, nilitegemea sana kuwa badala ya kuweka adhabu katika Sheria hizi, utaondoa Sheria hizi. Waarabu wana msemu wanasema kuwa; "*Alhimaru rayamshi - fil - magongo.*" Punda haendi bila ya kupigwa magongo. Tatizo lenu Serikali ya CCM hamsikii, tena mmeshakaa miaka mingi mmeshazeeka. (*Kicheko*)

Sisi wanasiasa hatuwezi kutumia lugha nyepesi, ni lazima tutumie lugha nzito ili make sawa. Leo kwa sababu ninataka kutumia lugha nzito unaniwekea faini kubwa; *what is that?* Hunitendei haki wala demokrasi huitendei haki hii,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED]

kuweka adhabu kubwa namna hii haitasaidia. Kitu muhimu kwa sasa ni kukaa chini na wadau mkatafuta njia ya kupita, siyo kusema tu lugha ya uchochezi faini milioni tano hiyo haisaidii kitu.

Kaa na wadau zipitie upya hizi Sheria, *almost* hizi ni Sheria za ukandamizaji kabisa. Kuna sheria ya mambo ya dini hapa kuwa hata sauti, *it means* tutafika mahala kwa sababu umeshaweka faini milioni tano, mimi nikisimama nikasoma adhana, mwingine ikamkera adhana yangu, atakwenda kushitaki kwa sababu anajua kuna faini ya milioni tano. Lazima hili tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, hebu tukaeni na wadau tuziangalie hizi Sheria siyo kuweka faini tu, tutaleta zogo zaidi ya hapa ilipokuwa shilingi 1,000 mtu alikuwa hashughuliki, sasa hivi ni shilingi 5,000 atasema wewe Ustaadhi leo nitakukomoa kwa anajua akienda mahali anapigwa milioni tano. Ipo haja hizi Sheria kuziangalia upya na siyo kuziongezea adhabu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninakushukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. MARTHA J. MLATA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Ninafahamu kabisa kuwa, Chama changu cha Mapinduzi ni sawa na maji ya bahari, ambayo yalikuwepo, yapo na yataendelea kuwepo na kwa sababu hiyo, hayazeeki; hivyo Chama changu hakizeeki. (*Makofi*)

Ninashukuru kwa Muswada huu uliokuja mbele yetu ili tuweze kuboresha. Mimi nitakuwa na machache sana, nitaongelea kuhusu Sheria ya Marekebicho ya Sheria ya Filamu kwa adhabu ambazo inaonekana kuwa zilikuwa ni ndogo sasa ziongezwe. Kwa masikitiko makubwa, ninaona Serikali inajipendelea yenyewe; inakuwaje unaleta Sheria unapokosewa wewe lakini usimwangelie yule atakayekukosea haki yake ya msingi? Kwa muda mrefu sana tumekuwa tukilia kutokana na kukosewa kwa kazi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J. MLATA]

zinazotokana na sanaa hasa za filamu na hizo za maigizo, lakini Serikali bado hamjaja na Sheria yoyote ya kuweza kurekebisha au kuhakikisha kazi hizo au wanaofanya kazi hizo, wanatendewa haki.

Leo hii mnatuletea marekebisho kuwa lugha zitakazotumika kwenye kazi hizo za filamu kama ni kudhalilisha au ni za uchochezi, basi hukumu yake iwe kama ilivyo. Mimi sina matatizo, lakini ninachelea sana kuunga mkono, kwa sababu ni kwa nini Wizara isije na mpango kamili wa Sheria kamili kwa sababu hakuna Sera yoyote inayohusiana na tasnia hii ya filamu, kama tutakuja na suala la Sera ambayo itatunga Sheria ambayo itatupatia Kanuni ili tuweze kwenda sambamba.

Ninaomba sana Waziri atakaposimama anihakikishie kama yuko tayari kuliondoa suala hili ili aje na mpango kamili wa kuwa na Sheria kamili itakayoweza kutenda haki kwenye pande zote. Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Vijana, inatambua kuwa Shirikisho la Filamu Tanzania, lilitafuta mfadhili, mfadhili ambaye aliwafadhili na kupata mtaalamu wa uchumi wa mambo ya filamu, ambaye alitoka Hollywood Marekani na pia Afrika ya Kusini na Mshauri Mkuu wa hapa Tanzania. Wakapita kufanya utafiti, wakaenda katika Taasisi na Idara mbalimbali kutafuta maoni. Wizara ya Habari na Utamaduni na Michezo inalifahamu hilo na wakaja na mikakati ya kuwa na Sera ambayo itakusanya mambo yote; mambo ya maadili na mambo mengine kadha wa kadha yatakayotokana na yatakayoteleza kuwa na Sheria ambayo mojawapo ni hii mmeileta.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Mheshimiwa Waziri uondoe hii ili uandae Sera kamili itakayopelekea tupate Sheria kamili na pia tuwe na Kanuni zinazoweza kusimamia tasnia hii ya filamu Tanzania. Pia ni vizuri sana kuwasikiliza wadau, maana wadau ndiyo wahusika, kwa hiyo, ninaomba hilo sana.

Tumezoea siku hizi wakimwona Msama wanamwambia bwana mimi sina kazi za wizi hapa, kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J. MLATA]

sababu hakuna Sheria yoyote inayosimamia suala la kazi za sanaa hata ya filamu ili kuweza kufikishwa mahakamani na kupatiwa adhabu iliyo kubwa. Wanaachwa huko mitaani, kwa hiyo, kila mtu anaona kama ni mchezo fulani wa kuigiza. Serikali inapofika kwenye kuguswa basi inaona iweke Sheria. Tunaomba sana pande zote mbili zitendewe haki.

Mheshimiwa Spika, suala la waandishi wa habari kupatiwa adhabu sina tatizo kwa sababu ninapenda sana nchi yangu kuwa na amani. Uchochezi tumeona ni sawa na moto unaotoka kwenye kibiriti, lakini unaweza ukaunguza pori kubwa sana. Sina tatizo na Sheria hiyo, lakini bado ni sambamba kama nilivyosema, kwenye upande wa tasnia ya filamu hivyo hivyo mmefanya kwenye upande wa habari. Kwamba, mmekuja na suala la adhabu peke yake, lakini mmemshau huyu mwanahabari mwenyewe. Je, yeye mazingira yake, mwongozo wake anapokuwa kwenye ajira yake ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, tumewasahau wamiliki wa vyombo vya habari wenyewe; je, Serikali inatumbua haki zao hawa waandishi wa habari; ni kweli wanalipwa vizuri? Ni kweli wanapatiwa haki zao za msingi? Ni kweli wanaelimishwa vya kutosha au unakuta Mhariri kwa sababu ana *certificate* basi anaona asimwendeleze anamwacha aendelee na ile *certificate* yake ndiyo anamfanya kuwa Mhariri Mkuu ili amlipe kidogo kwa kutokumwendeleza? Je, Serikali ina mwongozo gani ili kusaidia jambo hili?

Mheshimiwa Spika, naomba mnyonge mnyongeni haki yake mpeni; ni kweli kabisa waandishi wa habari wamekuwa wakitumika vibaya lakini je, tumewahi kujiuliza ni kwa nini wanatumika vibaya? Wanalipwa sawasawa? Masilahi yao yapo sawa sawa? Nao wanahitaji leo. Tumepitisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, waandishi wa habari nao wanatakiwa wawe mle, wajiunge na waajiri wao wapeleke kule mafao yao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J. MLATA]

Mheshimiwa Spika, je, bima ya afya wanayo? Je, bima tu ya kuumia kazini wanayo? Vitu kama hivyo ni kama watumishi wengine. Kwa hiyo, naomba sana niwaunge mkono wenzangu waliosema ile Sheria kamili ya Habari ije hapa ili tuje tuyaweke bayana mambo haya. Naungana mkono na Mheshimiwa Jenista Mahagama, ambaye ndiye Mwenyekiti anayesimamia mambo haya, Sheria hiyo iletwe ili tuje twende sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Spika, nataka kumalizia kwa kusema kuwa, ndugu zangu waandishi wa habari ninyi ni watu muhimu sana katika Taifa hili. Tanzania haiwezi kujulikana kama siyo ninyi ni nani atakayepaza sauti? Ni ninyi wenyewe lakini ninawaomba msitumike vibaya, kuweni wazalendo, ni bora ufe maskini lakini uwe mzalendo. Sisi wanasiasa tusiwatumie vibaya, tuwatumie kwa manufaa ya Taifa hili.

Ninaamini kabisa hata waandishi wa habari mnaonisikia, ninawaomba sana mumwogope Mwenyezi Mungu, kila mtu kwa dini yake, tuachane na mambo ya uchochezi. Taifa hili likipata msukosuko hakuna atakayepona. Hutaweza kuandika, hutaweza kupata chochote, kila mtu atakimbilia kivyake. Kwa hiyo, si la mtu mmoja bali litakuwa ni la wote.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mwenyezi Mungu, awasimamie ndani ya nafsi zenu ili mfanye kazi ambayo Mungu amewaitia kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante Mchungaji Martha, hapa sasa unatuhutubia. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mbarouk, yupo? Haya Mheshimiwa Sakaya!

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nami kunipa fursa niweze kuchangia Muswada huu wa Marekebicho ya Sheria Mbalimbali uliopo mbele yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja niende kwenye Muswada wenyewe, nitachangia vipengele vichache tu kwa sababu vingi vimechangiwa na wengine.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu, Sura ya 412, Kifungu cha 4(3) cha Muswada unaeleza kwamba, fedha ya Mfuko wa Elimu zitumike kwa ajili ya kuboresha Elimu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Jedwali, Elimu tumekuja kwenye Elimu ya Juu tu, kwenye Elimu ya Chini tumeacha. Uboru wa Elimu unatakiwa uanzie chini kwenye *grassroot* kwenda juu. Tukiacha huku chini tunaenda kuangalia kwenye Mikopo ya Vyuo Vikuu, tunakosa watoto wanaotaka huku chini wenye uwezo wa ku-*perform* vizuri kufika huko juu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwanza kabisa Mfuko huu kwa kiasi kikubwa ungeangalia huku chini kwenye matatizo lukuki, kuanzia *primary school* na *secondary school*. Tunalo tatizo kubwa la Kitaifa kwenye Elimu ya *Primary* na Elimu ya Sekondari. Tumeona tangu mwaka juzi tunapiga kelele kwa jinsi ambavyo Elimu ya *Primary* na Sekondari inavyozidi kushuka chini. Tumeona jinsi ambavyo mazingira ya kufundishia yalivyokuwa magumu, kuanzia *primary school* watoto wanakaa chini, mpaka leo ndani ya miaka 51 ya Uhuru.

Mheshimiwa Spika, tumeona sasa mazingira ya watoto wa sekondari, vifaa vya kufundishia, hakuna vitu mbalimbali, maabara, walimu wamekata tamaa. Naomba sana Mfuko huu lazima uangalie kwanza kwenye msingi kabla ya kwenda juu?

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kutenga fedha ninakubaliana kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kwenda Vyuo Vikuu, asilimia 64. Lazima tuambiwe fungu gani linakwenda kwenye kuboresha na kuwezesha shule ambazo zipo chini ambazo ni za *primary school* na *secondary school*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa Serikali itulettee hapa Bungeni ni jinsi ya kuboresha mfumo wetu wa elimu kwa ujumla. Nimekuwa najiuliza; sijaona utaratibu mahali anapotokea Kiongozi ni Waziri au ni Katibu Mkuu au ni yeyote Mtendaji, kubadilisha mfumo kwenye elimu, utaratibu gani unafuatwa? Je, anaweza kuamua tu mwenyewe na kukaa leo na kusema nibadilishe mtaala fulani? Kwa sababu tumekuwa tunaona Waziri anaweza kuingia kwenye Wizara akaamua kwamba naondoa mtaala wa sayansi, mwingine anasema naondoa michezo na mwingine atasema naondoa *arts*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna mfumo, lazima tuletewe Sheria turekebishe kwamba asiruhusiwe kiongozi wa aina yeyote kubadili mfumo wowote wa Elimu bila kushirikisha Wadau wa Sekta zote.

Mheshimiwa Spika, hili limekuwa ni tatizo kwa sababu juzi nilikuwa namsikiliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, alipokuwa anahojiwa na *TBC 1 Taifa* ni kwa nini walikuwa wameondoa sifuri kwenye mfumo wa kupanga madaraja. Alichosema yeye namsikia kwa masikio yangu wala sikuambiwa na mtu akasema kwamba: Unajua mwandishi wa habari ile sifuri ilikuwa na ukakasi sana, kwa hiyo, tukaona njia ya kuitoa ilikuwa inakatisha tamaa watoto tukaona ili kuirekebisha tuweke daraja lingine ili kuiondoa sifuri. Sasa nikawa najiuliza palepale kwamba hivi tatizo ni sifuri, tatizo ni ukakasi wa sifuri au ni kwa nini watoto wanapata sifuri?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikaona kuna *loophole*, kuna udhaifu mkubwa kwenye Sheria nzima ya elimu kwamba, Katibu Mkuu au Waziri mwenye dhamana, anaweza kubadilisha mfumo wowote ndani ya elimu kwa sababu tu hakuna mwongozo unaomkataza kufanya hivyo. Kwa hiyo, naomba sana tuletewe Sheria ya kuweza kuwa *very strict* kwamba, asiruhusiwe mtu kubadili chochote. Elimu ni moyo wa Taifa lolote, tukikubali kila mmoja aje abadilishe anavyotaka, tutazalisha Taifa la wajinga, watu watafika Vyuho Vikuu hawawezi kwenda kuajiriwa. Kama ambavyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

sasa hivi tumeleta madaraja mengi, tumeshusha gredi za elimu kutoka *grade one* badala ya kuanzia 81 tumekuja 78 ni tatizo. Badala ya kuangalia chanzo cha tatizo tunakwenda kuongeza madaraja yasiyokuwa na tija, eti kupanua wigo. Tunapoteza msingi wa elimu yetu ambao lazima watoto wapambane wafikie maksi ambazo tulikuwa tumeziweka na siyo kupunguza kwa ajili ya kufurahisha watoto wakati tunaharibu elimu ya watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni marekebisho ya Sheria za Bodi ya Mikopo. Mimi nakubaliana na Bodi ya Mikopo, Wajumbe wa Bodi ninakubaliana na mapendekezo yaliyoletwa. Wajumbe wa Bodi kwanza waongezwe, kwa sababu kwenye Sheria kwenye Muswada wenyewe walikuwa wamesema wawepo watoto wawili, *I mean* Wajumbe wawili; mmoja kutoka Vyuo Vikuu vya Umma na mmoja kutoka Vyuo Vikuu vya Binafsi. Kwenye jedwali la mapendekezo lililoletwa na Serikali wameondoa, wameweka Mjumbe mmoja kutoka kote; yaani atakayewakilisha Vyuo vya Umma na Binafsi. Kwa hiyo, naomba irudi ile iliyokuwa kwenye Muswada wenyewe, lazima wawakilishi kwenye Vyuo vya Umma awepo na kwenye Vyuo vya Binafsi awepo mwakilishi wao kama ambavyo Kamati imesema kwamba, mahitaji yao ni tofauti. *Private* ni tofauti na Vyuo vya Umma ni tofauti. Kwa hiyo, naomba yale mapendekezo ambayo yalikuwepo mwanzoni yarudi kuhakikisha kwamba, Bodi inakuwa na uwakilishi mzuri.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la utendaji wa Bodi ya Mikopo. Kiukweli lazima tuyafanyie marekebisho makubwa, kwa sababu malalamiko ni kila siku na wanafunzi mpaka waandamane ndiyo wapate mikopo. Hili ni tatizo kubwa. Kumekuwepo na minong'ono na najua kuna tetesi kwamba, inawezekana fedha za mikopo zinafanyiwa biashara na Watendaji wa Bodi yenyewe kabla ya kwenda kwenye vyuo husika.

Mimi nina mifano hai, wapo wanafunzi wa Mipango waliniletea taarifa kwamba, wamefuatilia mikopo yao ndani ya muda mrefu hawakupata. Wakaenda *Headquarters* Dar

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

es Salaam kufuatilia, wakaambiwa wiki tatu fedha zimeshaenda kwenye Mfuko wa Shule. Kwa hiyo, chuoni mkopo haujafika, lakini *Headquater* inaonesha fedha zimeshakwenda kwenye chuo. Sasa angalia wiki tatu, fedha ya chuo kizima, wanafunzi wengi, imekuwa inafanya kazi gani hapa? Kwa hiyo, kuna hisia kwamba, inawezekana mikopo hii inafanyiwa biashara na Watendaji kabla ya kwenda maeneo husika.

Kwa hiyo, naomba Serikali iweke jicho lake. Tuangalie mfumo mzima wa utoaji wa mikopo. Tuangalie utendaji, uelewa na uweledi wa Bodi ambayo tunaiweka kwa ajili ya mikopo, ili kuondoa minong'ono na migogoro ambayo imekuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii pia ya Bodi ya Mikopo, Kifungu cha 32A kinaeleza kwamba, Taasisi za Mashirika Binafsi na Umma, kutoa taarifa za watumishi wanaonufaika na mikopo ili waweze kurejesha. Jambo ambalo ni jema sana, kwa sababu tunapofuatilia mikopo na mimi nimeona Bodi ya Mikopo ina tatizo, ufuatiliaji wa mikopo unakwenda *very slow*. Ukiangalia hata hapa Bungeni tu, wapo Wabunge ambao walisoma kwa mikopo lakini hawajalipa mikopo. Sasa hapa ni Taasisi ambayo ni rahisi kufuatilia; je, huko mbali? Kwa hiyo, Bodi ya Mikopo kwenye suala la ufuatiliaji wa mikopo bado haijafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kufuatilia kwenye Sekta Binafsi na Taasisi za Umma; je, waliojijiri ambao walipata mkopo wa Serikali wakasoma mpaka Vyuu Vikuu wakajijiri wenyewe tunawapataje walipe mikopo ile? Kuna wengine ambao walisoma ndani ya nchi wakaenda kufanya kazi nje ya nchi au wakasomeshwa nje ya nchi kwa kutumia fedha za Watanzania wakazamia huko huko wanafanya kazi huko huko; je, tunawezaje kuwapata waweze kurudisha mikopo ile?

Sheria hapa ipo *blank* haijaweka wazi kwamba, wale wanaofanya nje ya nchi tunapataje mikopo yao, marejesho yao na wale ambao wamesomeshwa vyuo vya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

nje wamefanya kazi kule tunapataje marejesho ya mikopo yao? Kwa hiyo, naomba na hilo pia sheria ituambie inakuwaje.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Sheria ya Magazeti. Wengi wamelizungumzia tena kwa uchungu mkubwa; ukweli Sheria ya Magazeti, Sura ya 229, Serikali imeongeza adhabu, lakini ni muda mrefu hapa Bungeni, Mheshimiwa Spika, Wabunge na hata nje wadau mbalimbali, tumekuwa tukiiomba Serikali ilete Sheria ile ya Vyombo vya Habari, tuifanyie marekebisho. Ni muda mrefu kweli kweli, mimi nakumbuka toka mwaka 2009 tulikuwa tunapiga kelele haijawahi kuletwa na tunaona madhara ambayo yanawapata vyombo vya habari mbalimbali, waandishi wa habari, lakini Sheria haijafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, tunachona, tunaona kinaletwa kipengele kidogo cha kuongeza adhabu. Mimi najiuliza, Sheria ya Habari imempa Waziri mamlaka ya kuweza kufunga gazeti muda wowote na saa yoyote atakavyojisikia yeye bila hata kushauriana na chombo chochote. Sasa kwa hali ya kawaida tu, kwa mfano, Waziri anaandikwa kwenye gazeti kafanya kitu kibaya; je, ile habari kwake itakuwa nzuri? Haiwezi kuwa nzuri, lazima atachukia. Kwa hiyo, kwa kutumia habari ile na kwa sababu sheria imempa mamlaka ya kufunga chombo cha habari anaweza kufunga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kiukweli kuna udhaifu mkubwa, angalau ingekuwepo ashauriane na chombo chochote. Kitendo cha kumpa Waziri mwenyewe tu anasema ni habari za uchochezi; mimi niulize tafsiri gani ya habari ya uchochezi; nani anayetafsiri kujua hii habari ni ya uchochezi na hii siyo ya uchochezi? Tafsiri ya uchochezi ni *the way* unavyoisoma wewe mwenyewe. Kama habari iliyoandikwa ni ya ukweli na aliyeandika anaweza kupatikana popote; unaionaje ni habari ya uchochezi?

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida habari ya ukweli inapoandikwa, ya Taasisi, ya mtu au ya Serikali,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

inaonekana ni uchochezi. Waandishi wa Habari hawawezi kuandika mambo yanayowafurahisha watu, yanayoifurahisha Serikali au yanayofurahisha taasisi fulani. Wanaandika kile ambacho kimetokea kwenye jamii. Kazi yao ni kuwahabarisha umma, ndiyo wajibu wao wanaofanya. Kwa hiyo, wanaposema jambo la ukweli kikubwa ni kumwambia thibitisha na kama unajua kabisa kwamba hili ni uwongo limethibitika, achukuliwe hatua yule *individual* aliyeandika ile habari.

Mheshimiwa Spika, kuwanyima Wananchi habari ya gazeti fulani walilolizoea kwa sababu ya taarifa ambayo wewe binafsi haijakufurahisha, ni kubinya uhuru wa vyombo vya habari. Tunaomba sana, kuongeza adhabu hakutaondoa tatizo, lazima sheria nzima iletwe Bungeni tuiangalie, tutoe upungufu, tuweke *input* zetu na tuangalie kwa jinsi ambavyo tunafahamu kazi ya habari ilivyo, wanaoandika habari tumesema wapewe elimu. Serikali imesema inawapeleka nje, lazima tuhakikishe tunatenda haki, tusijiangalie sisi wenyewe.

Ninasema kwa mfano, Gazeti la Mwananchi lilifungiwa karibu wiki tatu, hatujaambiwa alifungiwa kwa sababu gani na kafunguliwa kwa sababu gani. Mwanahalisi alifungiwa mpaka leo hajafunguliwa, hatujui kwa sababu gani tunaambiwa ni uchochezi; mbona magazeti mengi tunaona yapo yanaandika habari zile zile?

Mheshimiwa Spika, ninaona kabisa lipo tatizo la msingi; Serikali iangalie tatizo lililopo tu-*deal* na msingi wa tatizo, tusiende tu kutunga sheria kwa ajili ya kuwafanya waandishi wa habari waogope kuandika habari ambazo zinatuhusu kwa sababu ni Serikali na kwa sababu tuna mamlaka hayo. Hapana, hii ni nchi ya Watanzania, tunahitaji vyombo vya habari na habari ziweze kusambaa kwa watu wote.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, yangu ni hayo mafupi. Ahsante. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchemba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, leo nimesimama hapa kwa jambo dogo sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie *Miscellaneous Amendment*. Nalitaka kuelezea kuhusu Sheria ya Magazeti, *The Newspaper Act, Cap. 229*, Namba 39, 40 na 41.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali hili la magazeti wangelitoa, badala yake walete Sheria. Mimi sipingi kuongeza adhabu, hata wakisema waweke adhabu mara tano ya hii aliyoweka hapa, sina tatizo nalo. Tatizo langu kwa nini kuwe kuna uharaka katika suala la adhabu peke yake? Uharaka huu unatoka wapi? Tuna-*send message* gani kwenye *public*? Tunawaambia nini waandishi wa habari?

Tulete sheria nzima ya habari ambayo itahangaika na mambo yote yanayohusu waandishi wa habari, mambo yanayohusu maisha yao, *responsibility* ya owners, *responsibility* ya kila mtu, halafu tuweke hizi adhabu hata mara tano. Kama tunataka tukae hapa, cha haraka cha kwetu ni kuweka adhabu peke yake, hapana. Mimi naomba wenzangu ambao nimesikia wengi wanasema, mnisamehe leo nitakuwa tofauti, lakini ukiangalia hapa unasema leo liko jambo kwa nini tusilete sheria yote, haraka ni ya nini? Kwa nini tunyofoe unaweka ambalo linakupendeza wewe? Tunachotaka tulete sheria nzima.

SPIKA: Mheshimiwa Lema, umesahau utaratibu? Naomba uendelee Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali wanielewe, tusinyofoe sheria hii. Ninajua Sheria ya Magezeti ipo tayari, leteni Sheria yote. Mle kwenye Sheria ya Magazeti ya vyombo vya habari, kuhusu waandishi wa habari na kila jambo, yote tunayaweke tutatue na yote yatawekwa. Tukisema tunanyofoa kitu kimoja ambacho kinakupendeza ndiyo unakileta, hapana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. SERUKAMBA]

Inawezekana nia ni njema, lakini kuwaambia watu nia ni njema ni ngumu sana hapa. Unaangalia Waandishi wa Habari ambao wanalipwa shilingi laki mbili, laki tano, mwenye mshahara wa milioni moja Mwandishi wa Habari ni mshahara mkubwa sana, leo unamwekea adhabu milioni tano, sawa basi weka na stahili zake azijue.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutunge sheria ambayo itaongelea magazeti na vyombo vya habari katika ujumla wake. Ninawaomba wenzangu tukubaliane leo, kifungu hiki wakiondoe wakaleta sheria nzima tuijadili. Bahati nzuri tunarudi Bungeni keshokutwa, kwa hiyo, nimwombe Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ondoa vifungu hivi na Kamati ipo, nendeni mkakae mjadili sheria mlete sheria yote, haya mnayotaka kuyaweka myaweke huko ndani, hili litaeleweka. Kama mnataka Bunge hili tukae hapa tunapitisha *Miscellaneous* hii kwa sababu tu ya adhabu ya Waandishi wa Habari, mimi nasema hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hakuna ambaye anapenda uchochezi hata kidogo na hakuna ambaye anaheshimu uchochezi hata kidogo. Nasema tujadili sheria yote kwa mapana yake ili watu wajue haki zao na kila mtu tuambiane, sisi ni wanasiasa, uchochezi mwingine tunautengeneza sisi wanasiasa. Waandishi wa habari hawa tunawatumia sisi wanasiasa. Mimi niwaombe wenzangu, kwenye hili tukubaliane tuondoe hivi vifungu vitatu halafu nendeni mkaleta sheria yote, haya mnayotaka kuwayaweka kawekeni kwenye sheria nzima ile. Mkiyaweka kule mimi sina shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli Sheria hii ni ya toka mwaka 1976, leo mwaka 2013, tuna kila sababu ya kuifanyia *review* Sheria yote. Tumefanya kwenye mambo mengine kwa nini hapa hatutaki kufanya? Mimi ninawaomba sana wenzangu Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili tuseme hapana, lakini tuwaombe waende wakaleta Sheria yote, hizi adhabu mnazotaka kuziweka kaziwekeni kwenye hiyo sheria kubwa, mimi hilo sitakuwa na tatizo nalo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. SERUKAMBA]

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa jambo moja tu hili, ninaomba sana Wabunge tukubaliane hii *part eight* yote tuiondoe. Tukiiondoa *part eight* tutawalazimisha walete sheria nzima, bila kufanya hivi sheria itakuwa haiji kwa sababu waliyoyataka wao wataona wameshayatekeleza. Tunataka kumwumiza nani; tunam-target nani hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nisiunge mkono mpaka tutakapokubaliana kuondoa vifungu hivi.

SPIKA: Vifungu vinaondolewa kwa *amendment* siyo kukubaliana. Tunaendelea Mheshimiwa Mwigulu Nchemba!

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nakiri kwamba, leo ni siku njema sana kwa wanafunzi wote Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa mwaka jana nilileta hoja binafsi iliyokuwa inahusiana na kuitaka Serikali kufanya marekebisho. Mwanzoni nilikuwa napendekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Elimu ya Juu, jambo ambalo baada ya makubaliano na Serikali, tulikubaliana kwamba, irekebishwe sheria badala ya kuja na sheria mpya ambayo badala ya kulenga elimu ya juu peke yake, ilenge pia na ngazi zingine.

Mheshimiwa Spika, leo hii nimekuwa nikipata maswali mengi sana kwa vijana wenzangu, wanafunzi wenzangu kwamba, Serikali iliridhia kuleta Muswada huo swali likawa sasa italeti lini? Leo hii Serikali kuleta Muswada huu kwangu ni faraja sana na ni siku moja nzuri sana na siku muhimu sana kwa wanafunzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja kwamba, kinachozingatiwa sana katika suala hili ni namna ya kupatikana kwa fedha kwa ajili ya kuendeleza elimu. Katika kuendeleza elimu, tusihangaike sana na suala la Bodi. Bodi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. N. MADELU]

ilikuwa inatumika kama *ATM* kwamba, fedha inazopata ndiyo hizo inahangaika kuzigawa. Niwaambie hali iliyokuwepo ilikuwa inasikitisha sana, kwa sababu wanafunzi wanakuwa wamefaulu na Bodi inagawa kile ilichokipata na haina uwezo wa kuongeza hata senti kwa namna zingine za kuweza kuhamasisha nyongeza yoyote ya fedha.

Kinacholetwa leo hii kina masilahi mapana zaidi, kwa sababu Bodi haiwezi ikaendesha harambee wala haiwezi ikafanya namna zozote zile ambazo zinapanua wigo wa upatikanaji wa fedha. Uwepo wa Mfuko huu unatuhakikishia upatikanaji wa fedha. Pia unatuhakikishia njia mbadala za kuweza kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza elimu yetu ya ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, habari kwamba, tunaongeza njia nyingine ya kuchelewesha fedha, kama fedha ipo hilo siyo la msingi sana, jambo la msingi ni upatikanaji wa fedha na fedha ikishapatikana na kwa namna ambavyo imepangiliwa itakavyogawanywa, itatumalizia matatizo.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka hata kwa namna ya Bodi ilivyo sasa, kuna wakati ilikuwa inachelewesha fedha, Kamati Kuu ya CCM ilipokaa ikaiagiza Serikali kulimaliza hili. Mtaona tofauti sasa, migomo imeisha ya watu kusubiria fedha tofauti na ilivyokuwa. Kama tutakuwa tumeshajihakikishia uwepo wa fedha kwenye Mfuko na Bodi ikawa imeshapewa kiasi chake kinachotakiwa, asilimia kama ilivyoelekezwa hapa, hii inatuhakikishia kulimaliza tatizo la Vyuo Vikuu, lakini pia inatuhakikishia kuendeleza miundombinu ya elimu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, uwepo wa Bodi wenyewe hauhusiki na miundombinu ya elimu. Kwa hiyo, hata kama tungekuwa na Bodi peke yake na ikapata fedha, hii haituhakikishii kuhusu miundombinu. Mnajua kwamba elimu si ada peke yake, leo hii tunahitaji sana miundombinu na hili ndilo ambalo limekuwa likigomba kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. N. MADELU]

kiwango kikubwa na uwepo wa Mfuko huu kama ilivyopendekezwa na mamlaka hii, utatusaidia kuweza kuwa na elimu bora kwa kila ngazi.

Uwepo wa Mfuko tunauhitaji sana kuliko kawaida, hii karne si ya Bodi. Nilisema wakati ule, ngojeni niwaambie tena; tullanza na bilioni tisa kwenye elimu ya juu wakiwa wanafunzi kama 16,000, awamu hii ya nne tumeenda kwenye zaidi ya bilioni mia tatu sasa hivi tunavyoongea. Niliwapeni makadirio tunakoenda mwaka 2015/16, tutaenda karibu bilioni mia sita, tutakapovuka bilioni mia nane Bodi haitaweza tena kuendesha suala la kuwalipia wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mfuko unahitajika kwa sababu Mfuko pekee ndiyo ambao utatuhakikishia uwezekano wa kuwa na vyanzo mbadala na namna ya kuendesha vyanzo hivyo kwa ajili ya kuendeleza elimu yetu. Tusiwe tunapiga hatua mbili tunarudi moja, tunapiga hatua tano tunarudi moja, tunapiga hatua moja tunarudi tano. Mashaka huwa yananiingia ninapooni watu wanajadili kurudisha nyuma hata jambo lililo jema hasa kwa wengine ambao wanacheza na habari zilizo mbaya kwamba kwao ni mtaji.

Mheshimiwa Spika, jamani tuwaangalie vijana, vijana ambao hawana ndugu, hawana watu wa kuwasaidia, anapofaulu halafu anakwenda hana uhakika wa kupata fedha ya kwenda shule wanapata shida mno. Kuna watu wengine hawajawahi kuonja hizi shida, watu wanapata shida, watoto wanapata shida mno. Leo hii limeshakuja jambo ambalo ni mkombozi, tusirudi nyuma ili tuweze kupiga hatua tuondokane na habari ya vigezo ambavyo ni ngumu sana kupima.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaweza tukawalaumu sana Bodi, tunaweza tukailaumu sana Serikali, lakini kwa ufinyu ule wa fedha zinazotokana na bajeti, yeyote ambaye angeweza kupewa azigawe angepambana tu na shida hiyo, utazigawaje? Kama wanafunzi elfu kumi na mbili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. N. MADELU]

wanaweza wakakosa fedha ingekuwa wewe ungezigawaje?

Hapa chanzo si kushughulikia mgawo ni kushughulikia vyanzo vya fedha zipatikane za uhakika, ugawanyaji utafanyika tu na utakuwa hautumii vigezo vya mtu awe amefiwa, kufiwa nako imekuwa CV ya kuombea fedha. Watu wasio waaminifu wanaweza wakaua wazazi wao wote ambao hawana uwezo ilimradi wapate cheti cha kwenda kupeleka kwenye Bodi ya Mkopo waweze kupata asilimia mia moja. Haya ni mambo ya aiibu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini uwepo wa fedha, yeyote anayefaulu akapata chuo, inamhakikishia kupata fedha za kuweza kuendea shule, lakini si kwa Bodi hii ni kwa ajili ya kutumia Mfuko.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaiunga mkono Serikali na kwa kweli mmedhihirisha kwamba ni Serikali sikivu, baada ya kupokea hoja binafsi iliyokuwa Azimio la Bunge, ilikuwa mlete Muswada huu Bunge lililopita tukabadilisha utaratibu wa kuendesha Bunge la Bajeti. Sasa mara baada ya Bunge la Bajeti mmeweza kuja na hoja hii. Niipongeze sana Serikali kwa hili na mmedhihirisha jinsi ambavyo ni Serikali sikivu.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo tunaliongelea la magazeti. Ndugu zangu niwaambieni na kwenye hili mimi niseme taratibu kabisa tofauti na mlivyozoea, habari ya aina yoyote ni biashara na habari kuwa biashara, habari nzuri si habari ila habari mbaya. Sasa kwa kuwa habari mbaya ndiyo biashara ni lazima tuweke sheria ambayo itakaweka *speed governor* kidogo kwa watu iwapunguzie uhuru wa kuweka masilahi ya biashara yao zaidi kuliko ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaambieni tu kwamba, tunahitaji sana hizi habari kwa sababu kuna Taifa, hata kwenye siasa tunahitaji hizi habari kwa sababu kuna Taifa. Inapotokea habari zinatishia uwepo wa Taifa, yeyote yule mwenye mamlaka, yeyote yule mwenye dhamana na Taifa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. N. MADELU]

ni lazima achukue hatua tena bila kusita hata sekunde.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, unaweza ukasema utafanya jambo hilo mwaka kesho, mimi niwaambieni habari iliyo mbaya ya kuchanachana Taifa hata wiki moja tu ni kubwa. Kuna mambo mengi tunaendelea nayo, unaweza ukasubiri kidogo tu usifike hata huko unakosubiria kwenda kutengeneza jambo lingine; kwa sababu lazima tutangulize Taifa. Leo hii siwashangai Upinzani wakisema kwa sababu hawana dhamana na mambo yote yakienda vibaya kwao ndiyo tija kuonesha kwamba wengine waliopo wameshindwa. *(Makofi)*

Kule Misri, wale waliokuwa wanaendesha lile vuguvugu wakaliita *M4C*, wakaandamana wakamtoa yule wakasema alikaa kwa muda mrefu sana. Walipoingia wao walizuia vyombo vya habari hata kutaja neno Serikali. Kwa hiyo, ukishafika pale unakuwa na namna unavyoona kwamba ni lazima umeshapewa dhamana. Kwa hiyo, hivi vitu tunavyoongelea, tunaongelea dhamana ya Taifa, hatuongelei masilahi binafsi, watu wanasema eti unapimaje kitu kinachokuhusu wewe tu; huwezi ukaongoza halafu kitu kilicho cha Taifa kisiwe cha kwako. Unapoongoza kitu cha Taifa ndiyo cha kwako.

Mheshimiwa Spika, leo hii sisi hatuna kitu kingine zaidi ya Taifa na adui yetu mkubwa ni yule aliye adui wa Watanzania wenzetu. Ndiyo hivyo; adui yetu mkubwa ni yule anayetaka kuharibu Taifa letu na tunapaswa kuchukua hatua mara moja bila kuchelewa hata sekunde moja. Hili si jambo la kuchelewa, jambo linalohusu Taifa si la kuchelewa, ni lazima tuchukue hatua mara moja.

Mheshimiwa Spika, Serikali niwaambieni hata inapotokea mmebadilisha leo mkiona kuna kasoro na wiki ijayo leteni badilisheni, mkiona kuna kasoro wiki ijayo badilisheni. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. N. MADELU]

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kumekuwepo na kasumba ya watu kuambizana maneno ya kupendeza hivi, Taifa haliendi kwa kuambizana maneno ya kupendezana tu; inapohusu suala la Taifa ni lazima tuoneshe njia na tuwaambie watu kuna tope ili wajiandae kwenda na viatu. Hivi kweli hapa Tanzania mnataka kuniambia hamjaona kabisa kuna sehemu tumeenda vibaya kwenye haya mambo ya habari? Ubaya wengine wanaochangia nao wana magazeti na wengine wana vyombo vya habari, kwa hiyo, kubwa kwao ni biashara, mimi kwangu lililo kubwa ni Taifa. Hilo lina *surface above all other businesses*. Kwa hiyo, ni lazima tukubaliane kwenye mambo ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, tangu nianze siasa sijawahi kuona jambo hata moja la Kitaifa ambalo Upinzani nao linawahusu; wenzetu mna Taifa lingine? Hebu Serikali fuatilieni *passport* za hawa watu, hamna hata siku wanayoguswa na mambo ya Kitaifa! Fuatilieni *passport* za watu hawa, utakuta wengine wana nyumba zingine ziko Italia, wengine Dubai, wengine wana *passport* mbili mbili. Sisi wengine wazazi wetu hawajui hata Kiswahili watakimbililia wapi? Hapa leo pakivurugika watakimbililia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazazi wangu leo hii hata haya ninayoongea mpaka awepo mtu wa kuwatafsiria, leo hii paharibike hapa watakimbililia wapi? Kisa demokrasia! Wale waliotufundisha demokrasia, wana mambo chungu nzima yanayofunga uhuru usio na mipaka. Ninyi mliitoa wapi hii isiyo na mipaka? Wamezoea wao kuendesha mambo kinguvunguvu, sisi tunataka tuendeshe mambo kisheria, watu wajue kwamba nikifanya hili ni kosa. Lazima tuweke hayo tusiendeshe kinguvunguvu tu.

Watu wanavyochangia hawa, lakini siyo makosa yao tuendeleo kuwaelekeza tu, ukiwa na chama hata Mwenyekiti anaruka kichwa, hata kapteni wa mpira hawezi kupiga wachezaji wenzake, unategemea kwenye mambo ya sheria wataridhia basi hata muweke sheria, wao wanaendesha kinguvunguvu tu kila jambo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. N. MADELU]

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuweke sheria, nchi iongozwe kisheria na mtu ajue kwamba, nikifanya hili nipo nje ya mipaka, huo ndiyo utawala wa kisheria na hapo ndiyo mambo yataweza kunyooka. Mimi napendekiza endeleeni kuboresha ikiwezekana tuwe na sheria ambayo ni kali zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kutolea mifano wenzetu wanaofuata sheria wamefanikiwa, tunapenda kutolea mfano mafanikio lakini hatupendi kutolea mfano njia walizopitia mpaka wakafanikiwa; ni lazima twende sambamba na haya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninawatakiwa kila la kheri Serikali, chukueni hatua kila mara mnapoona kwa masilahi ya Taifa kuna jambo linaweza likaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni, nadhani dakika hizi zinakutosha.

MHE JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika ahsante. Mimi naomba nichangie Muswada huu katika vipengele vichache.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nianze na suala la *Wildlife*.

SPIKA: *Order, order please!* Endelea.

MHE JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nichangie *amendment* za *Wildlife Conservation Act*.

SPIKA: *Wildlife* imeondolewa hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa hilo kwa sababu ingetugusa sisi wote.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninaomba katika sehemu ya tano upande filamu na upande wa maigizo, tungerekebisha kwa sababu hata kwenye Mataifa mengine, mahali ambapo wanatengeneza filamu mbalimbali kunakuwa na *copyright*. Mahali hapo kunakuwa na Bodi ambayo inapitia, ndiyo maana wanaweka *rating* kwamba, hii inafaa kuangaliwa na watu ambao ni zaidi ya miaka 18, miaka 16, miaka 13 na sisi pawe na mfumo huo, kwa sababu ukisema lugha ya uchochezi unamaanisha nini, kwa sababu kuna neno fulani mtu mwingine inaweza kuwa ni uchochezi lakini kwa mwingine ni kitu cha kawaida.

Kwa hiyo, tungeweka mambo ya *copyright* ili tasnia hii ya filamu iendeleo kukua, ndiyo maana katika nchi zingine wanakuwa na *ratings*. Kwa hiyo, kwa hilo ningepomba lifanyike hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo, naipongeza Serikali kwa kuleta haya mabadiliko na ninaamini kwamba, tutakuwa na mafanikio. Hofu yangu ni moja tu kwamba, wakati inapopita katika sehemu mbalimbali, hiyo fedha ikikusanywa na Hazina inaenda *TEA* halafu ndiyo iende kwenye Bodi na kwingineko; je, Serikali itatuhakikishia kwamba haitachukua muda na ucheleweshaji hautatokea? Kutakuwa na mfumo ambao utahakikisha ile fedha inatoka mara moja na inaenda kwa wahusika, lakini pia pawe na uwazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine pia kwenye suala la mikopo tungeangalia namna ya kubadilisha mfumo wa kupitisha, yaani wale ambao wanatakiwa kupata mikopo. Mimi najua wanafunzi wengi sana, pamoja na walimu wengi ambao hawakupenda kuwa walimu lakini wameamua kwenda huko kwa sababu ndiyo mahali wanapopata mikopo na hawana namna nyingine ya kupata elimu. Kwa hiyo, anaenda kusomea elimu, hapendi kuwa mwalimu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. V. SONI]

lakini tayari ni mwalimu, ndiyo maana wakirudi sasa huko mashuleni *interest* zao ni zingine. Ndiyo maana wengi wakifika Chuo Kikuu badala ya kusomea ualimu wanaomba sasa kubadilisha waende katika sekta nyingine ambapo wanaweza kujiendeleza. Kwa hiyo, tungeweka mikopo kwa watu wote ambao wanapenda kusomea ualimu au masomo mengine kama sheria na masomo mbalimbali, wote wapewe mikopo sawa, isipokuwa tuangalie wale ambao kweli wanahitaji na siyo kwa wale ambao wana uwezo. Tuangalie mfumo bora ambao Wananchi wasio na uwezo kabisa waweze kupatiwa hiyo mikopo.

Mheshimiwa Spika, pia katika sehemu ya uandishi wa habari, Sheria ya Magazeti tuiangalie upya kwa sababu ina pande zote mbili; kuna upande ambao unawaminywa hawa waandishi wa habari; lakini pia kuna upande wa pili ambapo unatumika vibaya na ndiyo maana hii sheria Serikali inapendekeza. Tungeangalia kwa undani na pia tuangalie namna ya kuboresha ili waandishi wa habari waweze kufanya kazi yao kwa uhuru zaidi. Pia huko wanakopata mafunzo, Serikali iweke jitihada, iwe shule za binafsi au shule zile za Serikali, kuwafundisha kwamba, wenzetu katika nchi zingine hasa nchi za Magharibi wanafanyaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule huwezi kukuta wanaandika vitu ambavyo vinaumiza masilahi ya nchi yao. Mambo ya usalama ya nchi yao hawayaandiki, lakini kwetu kitu chochote kinaweza kikaandikwa. Ni vizuri Serikali ingeingilia mambo kama hayo na kuwapa mafunzo nini kinafaa kwa masilahi ya nchi kiandikwe na nini kisiandikwe. Yale mengine ambayo ni ya masilahi ya wananchi ya kawaida, nasema waandishi wa habari wameweza kusaidia sana na kuleta mambo ambayo ilikuwa hayawezi kujulikana na wameweza kuleta haki kwa watu wengi hasa wa huko vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi ambayo yanafanywa katika sehemu mbalimbali; waandishi wa habari wameweza kusaidia na mambo mengi yakaweza kujulikana. Kwa hiyo, ningepia pia hapa Serikali iangalie namna ya kuingilia na kutoa mafunzo vizuri zaidi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. V. SONI]

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, katika suala la *Penal Code*, suala la uchochezi na lugha ya kashfa, kwa sehemu mbalimbali ile adhabu imeongezwa; mimi kwa hilo nitashukuru sana ikipitishwa. Mimi ni mmoja katika watu walioathirika na sikuweza kufanya lolote kwa sababu hiyo sheria ilikuwa haitaji mambo ya ubaguzi wa rangi, udini, kabila, hayo yote yalitokea na mimi ni mmoja katika watu hata ungeenda mahakamani hiyo sheria haikuwepo. Naipongeza Serikali kwa kuleta hiyo Sheria, wale watu ambao ni *minorities* na haki na utu wa mtu itakuwa sasa inalindwa na watu ambao walikuwa wanajisemea ovyo hasa katika mambo yetu ya siasa watakoma, kwa sababu hii sheria itambana, ina kifungo na faini itakuwepo na ni kubwa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuwapa pole Wananchi wa Babati Vijijini kwa msiba na ninaamini kwamba, hii Sheria ya *Wildlife* baada ya kuondolewa marekebisho yatakapoletwa, itakuja kwa sehemu kubwa na mabadiliko ambayo yatawanufaisha Wananchi ambao wanakaa jirani na hizi hifadhi za wanyama na hifadhi mbalimbali. Naendelea kutoa rambirambi kwa Mwananchi wangu mmoja ambaye mke wake aliuawa hivi majuzi katika *operation* ya kusaka majangili. Tunasikitika kwamba, bado hatua za kumsitiri marehemu hazijafanikiwa kwa sababu tunasubiri haki itendeke. Kwa hiyo, tunaomba hiyo haki ipatikane mapema ili tuweze kumsitiri mwenzetu na baada ya hapo wahusika wachukuliwe hatua stahili dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, zimeletwa *amendments* mbalimbali hapa, kwenye Mfuko wa Jamii wa kuchangia kuna mabadiliko katika viwango, wale ambao hawafikii *threshold* ya milioni 40 watakuwa wanasamehewa mpaka ufike hapo ndiyo utaendelea kuchangia. Ningependa pia kuchangia kwamba, ule mfumo wa kuweka viwango maalum wa ile fedha kwenda kila sekta ni mfumo mzuri kabisa, ambapo utasaidia hizi taasisi za elimu kwa upande wa bodi na kwa upande wa vyuo vya ufundi kuweza kujiendeleza. Ninaomba kama kuna namna fedha ikipatikana zaidi hivi vyuo vya ufundi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. V. SONI]

ndiyo vingepewa msukumo zaidi, kwa sababu Watanzania wengi ambao kielimu kwa sababu ya mfumo mzima wa elimu yetu ambapo kuanzia Msingi na Sekondari bado haujakaa vizuri, njia pekee ya wao kuendelea na masomo ni kujiunga na hivi vyuo vya ufundi ambapo wanaweza wakajiendeleza na pia wakaweza kupata kazi ya *u-technician* ambayo inaweza kuwasaidia katika maisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, ninaunga mkono hoja na yale machache ambayo yanatakiwa kufanyiwa marekebisho, ninaamini Serikali itaendelea kuyaangalia vizuri na tutapata mafanikio makubwa. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naona huu Muswada tumejadili vizuri na jioni imefika, nina tangazo moja tu.

Waheshimiwa Wabunge, *Caucus* ya Chama cha Mapinduzi, mnatakiwa kwenda kwenye Mkutano mlioambiwa saa mbili kamili. Kwa hiyo, ni vizuri mkawahi.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kesho; kutakuwa na kipindi cha maswali kama kawaida na ninaamini kwa Waziri Mkuu kutakuwa na kipindi kwa sababu yupo, halafu tutakuwa na maswali yetu ya kawaida, halafu tutamalizia Muswada huu kabla ya saa saba. Baada ya hapo, tutakwenda kupata chakula lakini saa tisa na nusu, Waheshimiwa Wabunge muwe ndani na mavazi ni *smart dress*, siyo kuvaa vyovyote vile. Saa kumi ndiyo Mheshimiwa Rais, atakuwepo lakini sisi tuwe tumekaa saa tisa na nusu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1. 35 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 7 Novemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)